# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 24 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt.Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu, sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini.

**SPIKA:** Mheshimiwa, samahani sana, naona hawa waandishi hapa wamekosea nami sikufikiri vizuri. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Idadi ya wapiga kura imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka tofauti na watu wanaokwenda kujiandisha kwenye daftari la wapiga kura. Kwa mfano, mwaka 2010 kati ya waliojiandikisha, walioenda kupiga kura ni 42.7%, mwaka 2015 kati ya waliojiandikisha, walioenda kupiga kura ni 65.3%, mwaka 2020 kati ya wale waliojiandikisha, waliojitokeza kwenda kupiga kura ni 50.7%.

Mheshimiwa Spika, yote hiyo imetokana na sababu mbalimbali ikiwemo wananchi kupoteza imani kwa vyombo vinavyoandaa uchaguzi na vinavyosimamia uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Je, Serikali haioni haja ya kukaa na wadau wa uchaguzi, kuwasikiliza na kuondoa dosari ambazo zinalalamikiwa ili kuruhusu uchaguzi huru na haki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutupa afya ya kutekeleza majukumu yetu kama ambavyo tunaendelea na tunaamini Mwenyezi Mungu atatupa neema zote ili tutekeleze majukumu yetu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu, kila Mtanzania anayo haki ya kuchagua, kuchaguliwa kupitia chaguzi mbalimbali ikiwemo uchaguzi mkuu. Majukumu yote ya uchaguzi yako chini ya Tume Huru ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali ni wadau, miongoni mwa wadau wote wanaoungana na tume katika kutekeleza wajibu wetu na Serikali. Wajibu wetu ni kutekeleza yale maelekezo ya tume kulingana na ratiba yao na wanayo ratiba ambayo inaonesha matukio mbalimbali kufikia siku ya upigaji kura. Moja, kufanya kazi ya maboresho ya kujiandikisha kwenye daftari la wapiga kura, ambapo kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura anayo haki ya kwenda kujiandikisha; lakini pia anayo haki ya kuhakikisha kwamba yuko kwenye daftari tayari kwa kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali kama wadau tunalo jukumu kama wadau wengine kushiriki pamoja na tume katika kutoa elimu kwa watanzania ya umuhimu wa uchaguzi na umuhimu wa

kujitokeza kwenda kupiga kura, lakini sisi kama wadau pia tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba nyakati zote za ratiba hiyo, kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa salama, hao wanaokwenda kujiandikisha tunao wajibu wa kuhakikisha usalama wake anapojiandikisha na hata siku ya kupiga kura tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba usalama wa mpiga kura unakuwepo.

Mheshimiwa Spika, tunalo pia jukumu la kuhakikisha kuwa tunahamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi kutoka kujiandikisha, kuhakiki mpaka siku ya kupiga kura ili kila mmoja atumie nafasi yake ya kidemokrasia ya kupiga kura kwa maana ya kuchagua kiongozi ambaye unaamini ataleta maendeleo kwenye maeneo yako.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jukumu hilo kwetu kama Serikali ambalo linafanana na majukumu ya wadau wengine kama vyama vya siasa, taasisi ambazo zinajikita katika kuhamasisha tutaendelea na kazi hiyo ili hayo mapungufu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza yaweze kutoweka na kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie na nitumie nafasi hii kuwahamasisha Watanzania kwamba, mwaka huu 2025 ni mwaka wa uchaguzi mkuu ambapo wale wote wenye sifa za kupiga kura ni wakati wetu kwenda kuchagua Rais, Wabunge na Madiwani kwenye maeneo yetu na pindi Tume Huru ya Uchaguzi itakapotangaza ratiba yake basi niwaahidi kwamba Serikali itasimamia na kuhakikisha kwamba uchaguzi huu unakuwa salama na kuhakikisha kwamba mpiga kura anakwenda kupiga kura na kurudi nyumbani akiwa salama.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo wajibu wa Serikali kama wadau wengine na kwa hiyo, nitoe wito kwa wadau kushirikiana kwa pamoja kutekeleza maelekezo ya tume ili kuwafanya watanzania wote waliojiandikisha wote waende kupiga kura. Hayo ndiyo malengo ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kumekuwa na wimbi kubwa sana la vitendo vya ukatili dhidi ya binadamu katika makundi mbalimbali ndani ya nchi yetu. Nataka kujua ni upi mkakati wa Serikali kuandaa vitengo maalum kwenye shule, vyuoni, ngazi ya jamii, ofisini na katika maeneo mbalimbali ili kusaidia kukabiliana na changamoto za ukatili zinapokuwa zinatokea katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Fiyao, Mbunge kutoka Mkoa wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo na tunashuhudia matukio ya ukatili dhidi ya watoto, wanawake, wazee, walemavu na makundi mbalimbali kwenye jamii yetu. Serikali inao utaratibu na tumejiwekea mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapunguza kwa kiasi kikubwa ukatili wa makundi haya. Moja ya utaratibu huo, kwanza Rais wetu wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameunda Wizara Maalum inayosimamia jamii na kuhakikisha kwamba inasimamia kupunguza na kuondoa au kumaliza kabisa ukatili juu ya makundi mbalimbali. Wizara hiyo ni Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Wizara hii imeweka mifumo ya kisheria inayomlinda kila mmoja ndani ya nchi na kumlinda dhidi ya ukatili wa aina yoyote ile ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kupitia sheria hizi, pia tumeshirikisha wadau, jamii kwenye maeneo yetu kwamba kila mmoja anatakiwa kuwa mlinzi wa kuhakikisha kwamba matendo yote ya ukatili yanayofanywa dhidi ya yoyote kwenye makundi haya ambayo yametajwa tunayachukulia hatua dhidi ya wale wote wanaotenda matendo haya na tumeandaa utaratibu mzuri wa

kuandaa madawati, tumeweka madawati kwenye taasisi zote za umma kama vile shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya elimu ya kati mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, tunayo madawati maalum ambayo yanatoa fursa ya yeyote anayetendewa ukatili kwenda kutoa taarifa na pindi anapotoa taarifa hatua kali zinachukuliwa. Pia, tumetanua wigo hata kwenye taasisi zinazotoa huduma za kiulinzi kama vile Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza nako pia tumeanzisha madawati maalum yanayomwezesha yeyote kutoa taarifa kuhakikisha kuwa pale anapotendewa ukatili basi kupitia zile sheria ambazo tumeziweka, yale madawati yanaweza kuchukua hatua kwa kumsaidia huyu mtu ambaye ametendewa ukatili.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ambao sasa tunaufanya ni kuhakikisha kuwa tunaendelea kutoa elimu kwa jamii, kushiriki kikamilifu kutoa ulinzi kwa kila mmoja, pale ambapo mtu anaona kuna tukio la kikatili basi achukue hatua mara moja ili kuwezesha jamii kila mmoja kutimiza haki yake ya kupata huduma na kufanya mambo ambayo yanamletea maslahi kwenye maisha yake. Kwa hiyo, Serikali na mkakati huu wa kuanzisha madawati ndiyo unaotoa nafasi kwa wale wote wanaotendewa ukatili.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa jamii, matukio haya ambayo yanajitokeza baadhi ya maeneo yanaondoa haki ya msingi ya kibinadamu pale anapotendewa ukatili dhidi yake. Kwa hiyo, kila mmoja awe mlinzi wa matendo haya popote katika jamii yetu kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji na maeneo yote. Pale ambapo kunajitokeza jambo hili basi tuchukue hatua dhidi ya wale ambao wanatenda matendo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana, wote tunaweza tukapunguza kwa kiasi kikubwa na kukomesha ukatili dhidi ya wale wote ambao wanatenda matendo haya. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali tutaendelea nao na tutaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhakikisha kwamba jamii inatambua umuhimu na inatambua wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kushirikiana na wadau ambao wameanzisha taasisi zinazosimamia kupinga ukatili dhidi ya makundi haya na pale ambapo kutakuwa na umuhimu wa kuona namna nzuri ya kuhakikisha kwamba jamii inaishi ikiwa inatendewa haki ikiwemo na taasisi ya haki za binadamu tutaendelea kushirikiana nao tuweze kupunguza au kukomesha kabisa ukatili dhidi ya makundi mbalimbali ambayo tunaishi nayo kwenye jamii.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Pamoja na jitihada kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha Watanzania wanaishi katika mazingira safi na salama. Je, ni upi mkakati wa kina ambao Serikali imejiwekea kuhakikisha inawasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, hususan watoto wa mitaani, kuhakikisha watoto hawa wanapata elimu, wanasaidiwa ili kuishi katika mazingira bora, lakini pia wanapata fursa nyinginezo zitakazo wawezesha kuweza kupata au kutimiza ndoto zao na malengo yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Malleko, Mbunge kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mbunge amezungumzia mwenendo wa watoto wa mitaani ambao wanastahili kupata haki yao ya msingi na wanaikosa kwa sababu wapo mitaani. Nataka nieleze tu kwamba jamii inatambua kwamba tunao watoto ambao wapo mitaani kwa sababu mbalimbali. Moja, vifo vya wazazi, kuwaacha watoto wakihangaika na jamii iliyobaki kutowaratibu vizuri.

Mheshimiwa Spika, pili, kutengana kwa baba na mama kwenye familia na kuwaacha watoto au kumwacha mzazi mmoja akihangaika na watoto naye pia akatelekeza, lakini wapo ambao wanatupa watoto wao. Matendo ambayo hayatendi haki kwa watoto wetu na kusababisha vijana hawa kwenda mtaani.

Mheshimiwa Spika, watoto wa mitaani kwa upande wetu wa Serikali tumeratibu vizuri, kama nilivyojibu swali lililopita kwamba tumeunda Wizara Maalum inayoratibu na kusimamia mwenendo wa jamii inayoitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Wizara hii imetoa maelekezo thabiti kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako watoto hawa ndiko waliko kwenye halmashauri, vijiji, halmashauri za manispaa mpaka majiji na kule tuna Kitengo cha Ustawi wa Jamii ambacho kazi yake kupita na kuona.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jukumu lake la kwanza ni kuwatambua hawa watoto mahali walipo, sababu za kuwepo kwao na mahitaji yao. Tunajua yapo mahitaji ya msingi, elimu, afya na chakula. Kazi ya Wizara hii ambayo inaendelea nayo hata sasa ni kuhakikisha kwamba inawatambua hawa, lakini pia kushirikiana na wadau ambao wamejitokeza kuokoa mazingira ya hawa watoto ambao wamezagaa mtaani na kuwaweka pamoja na tumeshuhudia mara kadhaa. Wapo Watanzania ambao wameguswa na watoto hawa kubaki mitaani, wanawakusanya pamoja na kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali, kwanza tunashirikiana na wadau kuhakikisha kwamba tunaweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha watoto hawa wanapata haki zao za msingi ili wafikie ndoto ambayo Mheshimiwa Malleko anaieleza. Pili, mifumo yetu ya kisheria ya huku ndani ya kumlinda mtoto huyu inatoa mwanya wa kumfanya mtoto huyu aweze kuishi kama wengine; moja hata ile sera ya elimu bure imewezesha sana watoto hawa kutoka mtaani na kwenda shuleni bila malipo yoyote. Vilevile, kuiwezesha jamii ambayo imekubali kuwatunza watoto hawa na kuweza kukaa nao na kuwapeleka shule bila gharama yoyote. Kwa hiyo, haya ni miongoni mwa yale ambayo tunayafanya katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee tu kuitaka jamii kwamba, uko umuhimu wa kuwabaini watoto wetu walioko mitaani na ambao wanazagaa, hawana mwelekeo na pia hawana huduma maalum na kuweza kuwaweka pamoja na kuwapeleka kwenye Halmashauri. Idara ya Ustawi wa Jamii itaratibu kwa mujibu wa taratibu ambazo Serikali imejiwekea.

Mheshimiwa Spika, ninaweza kusema kwa ujumla kwamba, Serikali tutaendelea kushirikiana na wadau ili kuhakikisha kwamba tunawatambua watoto hawa kwa mahitaji yao na kuwapeleka katika maeneo ambayo watapata huduma muhimu za kimsingi kama vile elimu, afya, malazi, chakula ili tuweze kuwapunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwa jamii tuache tabia ya kuwatupa watoto, kuwatelekeza watoto na tuache tabia ya kuacha watoto wanajiendesha wao wenyewe bila kulelewa kwa sababu watoto hawa ndiyo ambao Taifa litakuja kujengwa nao na maendeleo yataletwa kupitia watoto hawa. Kwa hiyo, wanahitaji haki yao ya kimsingi ya kuhakikisha kwamba wanapata huduma bora ili waendelee kufikia ndoto ambazo wanazo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi kubwa la wafanyakazi wa Serikali katika baadhi ya Wizara, taasisi kuhama kwenda kwenye taasisi nyingine kwa ajili ya kutafuta maslahi bora hasa mshahara. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa kada fulani zinazofanana na elimu inayofanana wanapata mshahara unaofanana ili kupunguza kuhamahama ambayo inaacha baadhi ya taasisi kukosa wafanyakazi kwa muda mrefu? Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la utumishi wa umma linaratibiwa vizuri na Serikali, ikiwemo na maslahi yao (maslahi pamoja na mshahara). Serikali kupitia Wizara iliyopo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, lakini pia hata Ofisi ya Waziri Mkuu tuna Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana; zote hizi zinafanya kazi ya kufuatilia mwenendo wa watumishi wetu wa umma. Si watumishi tu wa umma hata kwenye *private sector* (sekta binafsi) kuwa wanapata maslahi yao ambayo yanawawezesha kuwa na utulivu mahali pa kazi bila ya kuhamahama kutoka eneo moja mpaka eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, ingawa hatuzuii mtumishi kufuata maslahi popote na tunajua mishahara inatokana na majukumu ambayo anatakiwa kuyatenda, ndiyo yanayoweza kueleza kupitia mshahara huu unatakiwa kupata mshahara wa kiasi fulani. Vilevile elimu aliyonayo na ujuzi ambao anao mtumishi wa umma unamsaidia kupata mshahara wake. Pia hali ya uchumi, iwe ni taasisi au Serikali ndiyo inaweza kutengeneza mazingira mazuri ya mishahara hiyo.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kuweka sheria na ukomo ambao mtumishi wa umma hapaswi kupata kiwango cha chini zaidi ya kiwango ambacho kimewekwa na Serikali (sisi tunaita kiwango cha chini). Pia, huku Serikali tumeunda idara inayoshughulikia posho, mishahara, marupurupu ambayo inafanya mapitio kila mwaka na kuona mabadiliko ya kiuchumi ya nchi yanakwenda sambamba na pato ambalo angalau linaweza kumwezesha mtumishi wa umma kutekeleza majukumu yake katika familia.

Mheshimiwa Spika, mtumishi anapofanya kazi kwenye ofisi A iwe ya umma au binafsi hazuiliwi kuhamia taasisi B kama tu anaona kwamba, huku kulingana na majukumu na hali ya uchumi wa taasisi hiyo inaweza ikamletea maslahi. Kwa hiyo, jukumu letu Serikali ni kukaa pamoja na wadau hasa waajiri na ndiyo sababu tunafanya kazi na vyama vya wafanyakazi, vyama

vya waajiri, pamoja tunazungumza na kuhakikisha kwamba tunafanya mapitio ya maslahi yao wakati wote. Inatokea wakati mwingine tunawaweka pamoja wafanyakazi wote tunapata maoni yao. Hii siku ni ile siku ya Mei Mosi ambayo inajumuisha wafanyakazi duniani na mwaka huu tutakuwa Mkoani Singida, tutasherekea kitaifa.

Mheshimiwa Spika, tutakwenda kupokea maoni ya wafanyakazi, ujumbe wa wafanyakazi, lakini pia na waajiri watakuwepo wa pale, wa sekta ya umma na sekta binafsi ili kuona namna nzuri ya kufanya maboresho.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jukumu hili la kuhakikisha kwamba tunasimamia upatikanaji wa maslahi mazuri ya mtumishi wa umma na mtumishi kwenye sekta binafsi anapotekeleza majukumu yake kulingana na vigezo ambavyo vimeelezwa pale awali.

Mheshimiwa Spika, niwaahidi watumishi wa umma, lakini niwaahidi pia watumishi wa sekta binafsi kwamba Serikali itaendelea kusimamia maslahi ya watumishi kuanzia mishahara, lakini madai mbalimbali kuwa yanalipwa kwa wakati ili yamwezeshe mtumishi wa umma kuendesha maisha yake kutokana na majukumu anayoyatekeleza ambayo ni halali ikiwa ndiyo wajibu wake mahali pa kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghilla, Mbunge wa Kyela.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Hapa nchini kumekuwa na ongezeko kubwa sana la maji kwenye mabonde mbalimbali. Ongezeko hilo la maji linatokea kwenye mabonde ambayo mfano wake mzuri ni Bonde la Mto Songwe. Madhara ya hilo ni kutokea kwa mafuriko na yakitokea yanakuwa na madhara kwa jamii, lakini na kuhamahama kwa mpaka kati ya nchi yetu na nchi nyingine mfano ukiwepo ni Malawi. Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na changamoto hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu suala la Mheshimiwa Ally Jumbe, maarufu Mheshimiwa Kinanasi, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la mafuriko ni ongezeko la maji zaidi ya maji ambayo yanapaswa kuwepo kwenye maeneo hayo. Hii ni kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambapo tumeendelea kushuhudia kuwepo kwa mvua nyingi sana. Miaka ya hivi karibuni hapa kumekuwa na mvua ambazo hazitabiriki na tumepata adha kubwa ya mafuriko kwenye maeneo yote ikiwemo Kyela ambayo kuna bonde kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Waziri wa Ujenzi pamoja na Mbunge wa kule Ifakara wako kule Ifakara kwenye Bonde la Ifakara ambalo limejaa maji na hivyo kuwa na mafuriko. Haya ni mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, sasa, Serikali ina mkakati kukabiliana na haya? Moja, tumeunda mamlaka za mabonde haya. Tuna Mamlaka ya Bonde la Ifakara, tuna mamlaka ya Bonde la Mto Rufiji, tuna Mamlaka ya Mto Rufiji, tuna Mamlaka ya Bonde la Mto Ruvuma na mabonde mengine, tumeyaundia mamlaka. Malengo yetu ni kwamba; moja, wafanye ufuatiliaji wa mwenendo wa upitishaji maji kwenye mabonde hayo ili kuona pale ambapo kuna namna yoyote inayoweza kusababisha madhara, basi mamlaka hiyo iweze kuchukua hatua; kama vile watu wanachepusha maji, kusababisha ukame, wengine wanaziba njia na kusababisha kujaa kwa maji na mafuriko yanatokea. Sasa mabonde haya yanafanya kazi hiyo. Pia, yanaratibu namna nzuri ya matumizi ya maji hayo kwenye mabonde.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeona kwenye Bonde la Mto Rufiji, tumeamua kuanzisha Mradi mkubwa sana wa umeme. Yale ni matumizi mazuri na ni mapendekezo ya mamlaka ya Bonde la Mto Rufiji. Hata juzi nilifanya ziara Ruvu Mkoani Morogoro, pale ambapo tunachimba bwawa kubwa sana,

bwawa lile linategemea maji ya Mto Ruvu. Hayo ni miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Bonde la Mto Ruvu, kuhakikisha kwamba tunachimba mabwawa ambayo yataleta maslahi kwa Watanzania, kilimo, nguvu za nishati (umeme) na aina nyingine yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba mabonde haya tunayatumia vizuri na mafuriko haya tunayatumia vizuri kama tuna uwezo wa kuhakikisha tunaratibu mwenendo wa mafuriko hayo ili maji haya yasipotee na badala yake yatumike kwa namna ambayo inaweza kusaidia katika kupanua wigo wa sekta ya kilimo, nishati, matumizi ya mifugo na maji ya kunywa; tunaweza kuyatumia kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaongeza bajeti kwenye Wizara kama vile Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili kuhakikisha kwamba tunaratibu maeneo haya kwa kupanda miti na kuhakikisha kwamba hakuna mzagao wa maji. Pia kuchimba mifereji ambayo inaweza kupeleka maji kwenye mashamba mengine na mambo kama hayo. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuratibu mabonde haya vizuri na kuona kwamba mafuriko haya na maji haya mengi yanayopatikana kwenye mito hii tunayatumia vizuri kwa fursa kwenye maeneo ambayo nimeyaeleza.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea na uratibu huo, tutaimarisha mamlaka zetu ili ziweze kuwajibika na kupata ushauri pia kutoka kwa wadau namna bora ya kutumia maji ambayo yako kwenye maeneo haya, ikiwemo na Kyela ambapo kule kilimo kimejikita sana. Tumefanikiwa sana na Kyela ni miongoni mwa wilaya zinazotoa zao la mpunga bora kabisa nchini na umeweza kupata soko zuri kwa hali hiyo. Kwa hiyo tunataka tuliimarishe bonde lile kwa kuweka mifumo ya umwagiliaji ili maji yale yatakapokuja basi yakae yakiwa tayari kwa kutumika. Kazi hiyo tumeipa mamlaka, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Maji; waratibu ili wananchi wa Kyela wanufaike kwanza na maji hayo ambayo yako pale. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge wengine walikuwa wameorodhesha majina yao ili kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini muda wetu umetutupa mkono kwa sababu waliotangulia wameuliza maswali marefu na kwa hiyo tumeweza kujibu maswali machache.

Sawa, tunaendelea, Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya Kawaida, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake.

Na. 130

**Kuboresha Mazingira ya Kazi kwa Walimu**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango upi wa kuboresha mazingira ya kazi kwa Walimu hususani kuwajengea nyumba za kuishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetoa shilingi bilioni 13.79 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 263 katika shule za msingi nchini. Vilevile shilingi bilioni 14.82 imepokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya nyumba za walimu 741.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 54 *(2 in 1)* katika maeneo yenye changamoto ya uhaba wa nyumba za kuishi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha za kujenga na kufanya ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kutoa kipaumbele kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika nyumba hizo ambazo zinatarajiwa kujengwa na Serikali. Je, ni nyumba ngapi zitajengwa katika Jimbo la Segerea kwa walimu wanaofundisha kwenye Jimbo la Segerea?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mazingira mazuri ya kufundishia ni pamoja na kuboresha malimbikizo ambayo yapo kwa walimu, lakini pia kufuatilia malupulupu ambayo walimu wanadai. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa jambo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kuhusianana mipango ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inaendela kujenga nyumba za walimu ili kutengeneza mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa walimu wetu, Serikali imeweka mipango ya kutumia jumla ya shilingi bilioni 5.5 katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa ajili ya kujenga nyumba hizo 54 za walimu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaangalia; katika jimbo lake na tutaweka kipaumbele cha kipekee kabisa ili kwenye jimbo lake aweze kupata nyumba hizi za walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, ninaomba nitumie nafasi hii kutoa maelekezo mahsusi kabisa kwa wakurugenzi wote. Ninatoa maelekezo haya kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa, kwamba Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa waweze kutengeneza mchanganuo ili waweze kubaini ni watumishi wapi ambao wanadai malimbikizo yao ya mshahara na yasiyo ya mshahara na waweze kuyawasilisha utumishi ili Wizara ya Utumishi waweze kufanya uhakiki na wapeleke Hazina kwa ajili ya malipo. Kwa hiyo, naomba nitoe msisitizo huo.

Mheshimiwa Spika, jana katika bajeti ya Wizara ya Utumishi maelekezo hayo yalitolewa na Wizara hiyo, kwamba mpaka itakapofika tarehe 31 Mei wakurugenzi wote wawe wamekamilisha kuwasilisha majina hayo ya watumishi ambao wanadai malimbikizo yao. Kwa hiyo, wakurugenzi waweze kufanya hivyo ili watumishi hawa waweze kupata madai yao haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 131

**Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Vyumba vya Madarasa Shule za Msingi Mshikamano B, Mwabuzo, Mwambiti, Bukundi, Malugala ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali ilitenga shilingi milioni 975 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 43 katika shule 28 za Halmashauri ya Meatu zikiwemo shule 18 za Jimbo la Meatu. Hadi Machi, 2025 Serikali imetoa shilingi milioni 125 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 21 katika shule 12.

Mheshimiwa Spika, katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi milioni 975 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 50 katika shule 23 za Halmashauri ya Meatu zikiwemo shule 12 za Jimbo la Meatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule zenye mahitaji zaidi kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambapo tunatambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kuwa vyumba hivi vimelenga kupunguza mlundikano wa wanafunzi darasani:-

(i) Je, Serikali haioni haja ya kukamilisha maboma 90 yaliyopo Jimbo la Meatu ili kupunguza upungufu wa vymba vya madarasa hususani madarasa ya awali pamoja na darasa la kwanza?

(ii) Je, Serikali haioni haja ya kuigawa Shule ya Msingi Mwabuzo ili kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi na kuwasaidia anafunzi wanaotembea kilometa nane kutoka Vitongoji vya Songambele na Mwanzugi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali Awamu ya Sita chini ya

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, maboma 7,735 yamekamilishwa kwa gharama ya shilingi bilioni 87.9.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuendelea kuunga mkono jitihada za wananchi pale wanapokuwa wameanzisha maboma katika Sekta ya Afya na katika Sekta ya Elimu. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada hizi za wananchi kwa kupeleka fedha na kuhakikisha kwamba maboma yanaweza kukamilishwa na itafanya hivyo hata katika Jimbo la Meatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, lengo kuu la kuendelea kujenga miundombinu ya shule zetu hizi za msingi na sekondari pamoja na mambo mengine ni pamoja na kupunguza umbali mrefu ambao wanafunzi wanatembea kufika shule, lakini pia kupunguza msongamano. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Shule hii ya Mwabuzo Serikali itazingatia msongamano lakini itazingatia umbali mrefu ambao wanafunzi wanatembea kufika shule ili sasa iweze kujenga shule nyingine ambayo itaweza kuwanufaisha zaidi wanafunzi kwa kupunguza umbali na msongamano.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa kifupi. Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Shule 19 kati ya 31 za msingi Babati Mjini zimechakaa sana. Je, ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya kujenga shule hizo upya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Gekul Pauline kwamba Serikali inafahamu kwamba kuna shule ambazo zimejengwa zamani kidogo na ni chakavu na zinahitaji kufanyiwa ukarabati ili ziweze

kuwa katika hali nzuri na shule hizi za msingi nyingi tayari Serikali imeshafika kwa ajili ya kufanya ukarabati. Ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali itafika katika jimbo lake kwa ajili ya kuendelea na kazi hiyo ya kuboresha na kukarabati shule hizi kongwe ili ziweze kuwa katika hali nzuri na ziweze kuwanufaisha wanafunzi wetu kwa kusoma katika mazingira mazuri zaidi. Vilevile, walimu wetu pia wawafundishe wanafunzi katika madarasa mazuri zaidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge shukrani zenu zote za kupewa nafasi ya kuuliza maswali nimeshazipokea, kwa hiyo, msianze na hizo. Mheshimiwa Luhaga Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wilaya ya Meatu ikiwemo Jimbo la Kisesa milioni 925 katika mwaka wa fedha 2024/2025 hazijatolewa zote. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa *commitment* gani ya kwamba kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha fedha hizo zitakuwa zimetolewa kwenda kumalizia maboma yote yaliyoanzishwa na wananchi? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Luhaga Mpina kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuendelea kuboresha miundombinu katika Sekta hii ya Elimu na imekuwa ikifanya hivyo kwa kutenga fedha kila mwaka wa bajeti kuboresha miundombinu hii muhimu kabisa katika shule zetu. Ninaomba niendelee kumhakikishia kuwa kazi kubwa tayari imefanyika nchi nzima kwa kuzingatia mahitaji, lakini kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha Serikali itaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba inafika katika majimbo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu hiyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Luhaga Mpina hata katika Halmashauri ya Meatu ikiwemo katika jimbo lake Serikali itafika na italeta fedha kwa ajili ya kuendelea kuboresha miundombinu hii muhimu katika sekta ya elimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, Shule ya Utengule iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga yenye wanafunzi zaidi ya 1500 ina uhitaji wa vyumba vya madarasa 32 lakini vyumba vilivyopo ni saba tu. Je, Serikali iko tayari kulichukua jambo hili kama jambo la dharura ili kuwasaidia wanafunzi hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Sylivia Sigula kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuendelea kuboresha miundombinu hii katika Sekta ya Elimu na katika Shule hii ya Utengule ninaomba nikuhakikishie kwamba Serikali kwa sababu ina nia ya kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule zetu, lakini kupunguza umbali ambao wanafunzi wetu wanasafiri kufika shule, basi Serikali kupitia Serikali Kuu, lakini kupitia fedha za mamlaka zetu hizi za Serikali za Mitaa kwa maana ya mapato ya ndani ya halmashauri itafika katika shule hii ya Itengule kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu hii muhimu kabisa ili kuboresha mazingira ya wanafunzi wetu kusomea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi Sabasaba, Azimio na Mapinduzi zilizopo Halmashauri ya Mji wa Tarime zinatumia eneo ambalo lingefaa kutumika kwa shule moja kwa sababu ya uhaba wa ardhi ambayo inapelekea msongamano wa wanafunzi. Je, Serikali haioni kuna haja sasa kwa shule zile kujengwa kwenye mfumo wa ghorofa ili kuweza kuruhusu wanafunzi kusoma kwa *continuation?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, ni kweli Serikali inatambua idadi ya watu inazidi kuongezeka na ardhi bado ni ileile. Kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu mkubwa

sana wa matumizi bora zaidi ya ardhi na kwa wakati huu tayari Serikali imeanza ujenzi wa majengo ya darasa kwenda juu kwa maana ya maghorofa na Serikali itaendelea kutumia utaratibu huo katika maeneo yale yote ambayo yana uhitaji wa kujenga majengo yetu ya miundombinu ya shule kwa ghorofa.

Mheshimiwa Spika, siyo tu miundombinu ya shule, lakini miundombinu ya kutoa huduma nyingine kwa kutumia maghorofa kwa sababu ndiyo zama tulizokuwa nazo na tunahitaji kupanga matumizi bora zaidi ya ardhi ili tuweze kujitosheleza zaidi kuwasaidia wananchi wetu. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mawazo yako ni mazuri na tayari Serikali imeyapokea lakini imeshaanza kuyatekeleza na itaendelea kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, katika Shule ya Mtakuja, Kata ya Mabogini Jimbo la Moshi Vijijini mpaka sasa wanafunzi hawana pa kusomea kwa sababu madarasa matatu yameezuliwa na upepo kutokana na uchakavu. Je, ni lini Serikali itachukua jitihada za makusudi kurekebisha shule hizi lakini kuezeka madarasa haya yaliyoezuliwa na upepo ili watoto waweze kusoma vizuri? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Felista Njau kwamba katika Shule hii ya Mtakuja ambayo anasema madarasa matatu yameezuliwa paa, ninaomba nichukue nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi aweze kufika yeye pamoja na timu yake katika shule hii na waweze kufanya tathmini na tuweke kwenye mipango na bajeti kwa ajili ya kuhakikisha shule hii inaweza kukarabatiwa ili wanafunzi wetu wapate sehemu nzuri ya kuweza kujifunzia na walimu pia wapate sehemu nzuri ya kuweza kuwafundishia wanafunzi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, sasa aulize swali lake.

Na. 132

**Hali Mbaya ya Masoko Vijijini**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mindombinu ya masoko ya vijijini nchini ikiwemo sakafu na paa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025, Serikali imejenga na kukarabati jumla ya masoko 264 kati ya masoko 1,056 yaliyoko katika halmashauri za Wilaya kote Nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya masoko ya vijijini kwa kujenga na kukarabati mapaa na sakafu ili kuwawezesha wakulima na wafanyabiashara kuuza bidhaa zao katika mazingira salama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya shilingi bilioni 12.2 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa masoko ya vijijini, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.5 zimekwishatolewa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Masoko ya Vunjo pale kwenye Masoko ya Mwika, Kisambo, Marangu, Yamombi, Rindima, Himo, Chekereni na Oria ni masoko makongwe sana na vitovu vya ajira kwa vijana na wanawake; na kusema kweli masoko haya hayana miundombinu yoyote. Tunaomba sasa kwamba Serikali kwa vile imetenga shilingi bilioni 12.2 na Halmashauri ya Moshi Vijijini haina mapato ya kutosha ni mapato madogo sana. Basi katika fedha hizi zitakapoanza kutolewa sehemu yake ielekezwe kuboresha masoko haya ambayo pia Waziri wa Kilimo ameona kwamba kuna uwezekano wa kuyaboresha na kuyawekea miundombinu ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ndani ya *BBT*. Kwa hiyo, ninaomba wanipe kauli kwamba TAMISEMI itafanya nini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mji wa Himo kihistoria umekuwa ni mji wa kimataifa uliojulikana kimataifa kwa soko la nafaka ambapo ilikuwa wenzetu wa jirani wote walikuwa wanapata hapo *quotations* za mazao ni kubwa kuliko Kibaigwa pale lakini baadaye lilikufa. Sasa kuna eneo la Lokolova ambalo kuna hekta 140 ambazo Serikali imepewa na ushirika pale na tumekuwa tunafuatilia tuone kwamba…

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI**: Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali sasa itaanza mchakato wa kujenga pale soko la kimataifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, uliza swali lako.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatenga fedha au mkakati wa kutengeneza soko kubwa la kimataifa pale kwenye eneo la Lokolova? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua sana umuhimu wa kukarabati na kujenga masoko

katika maeneo ya vijijini ikiwemo katika Halmashauri ya Moshi vijijini. Katika maeneo ya Moshi kuna masoko ya aina mbili: aina ya kwanza ni yale masoko ya kawaida ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja ambayo tayari halmashauri imeanza kutenga fedha kwa ajili ya kuyakarabati kwa maana ya kujengea mapaa na sakafu na katika mwaka uliopita walitenga shilingi milioni 20 na mwaka huu wa fedha imetengwa milioni 20 na tayari fedha hiyo imekwishapelekwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, aina ya pili ya masoko ni yale masoko ambayo yako mipakani ni masoko ya kimataifa liko Soko la Himo, Mwika na Lyamombi. Masoko haya tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tulikwishapokea *BOQ* na michoro kwa ajili ya Wizara ya Kilimo kuanza utekelezaji wa ujenzi wa masoko hayo kwa ajili ya biashara ya nafaka kati ya nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, tatu, Soko la Lokolova liko mpakani pia na soko hili limeshapata eneo la ekari 140 ambalo Halmashauri ya Moshi inatafuta hati na baada ya hapo kutaanza ujenzi kwa kushirikiana na kituo cha uwekezaji *TIC*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba masoko yote aliyoyataja tunakwenda kuyatekeleza kwa utaratibu huo kwa halmashauri kutenga fedha Serikali Kuu, lakini pia kwa kutumia Mfumo wa *PPP*.

**SPIKA:** Maswali mafupi. Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, pale Kamsamba ni eneo maarufu sana na lina mkusanyiko mkubwa sana wa watu hivyo kupelekea biashara nyingi kuwa na mwingiliano. Kwa kuwa Ofisi ya Mbunge imewachangia pesa kidogo ni upi mkakati wa Serikali kutupatia pesa ili kujenga soko Kamsamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, maeneo yote ya kimkakati ambayo yanahitaji masoko Serikali ilishatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuainisha maeneo hayo, lakini pia kuanza kuandaa fedha katika bajeti za kila mwaka kwa ajili ya ujenzi, lakini pia kuandaa maandiko ya kimkakati kwa ajili ya Serikali Kuu na wadau kujenga masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Momba kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa maana ya kuleta andiko maalumu lakini pia kuanza kutenga fedha kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri ili Serikali iweze kujenga na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itakwenda kujenga soko hilo ili kuboresha huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda ilikuwa imeanzisha Soko la Manjebe kwenye Kata ya Nyasura, lakini miundombinu yake haifai na kusabaisha wananchi wa Bunda kutokwenda kwenye Soko la Manjebe. Serikali haioni haja sasa ya kutupatia fedha za kutosha kwa sababu halmashauri yetu ni changa na mapato yetu madogo watusaidie tujenge miundombinu rafiki ili wananchi waweze kwenda kwenye soko hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali na Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya masoko yote ili kuwezesha wafanyabiashara kupata eneo bora zaidi la kutoa huduma. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumechukua hoja hiyo na sisi pamoja na Halmashauri ya Mji wa Bunda tutalifanyia kazi ili kuboresha mazingira kwa ajili ya biashara kwa wananchi hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Kharumwa ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale na lile soko lililoko pale lina muda mrefu, limejengwa kabla ya mimi kuzaliwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea soko la kisasa kwenye Mji huo wa Kharumwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia Wakurugenzi na Mabaraza ya Madiwani kutambua maeneo yenye uhitaji wa masoko kama ambalo amelitaja Mheshimiwa Amar na kuanza kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ili kuhakikisha kwamba masoko hayo yanajengwa na yanaboreshwa kwa ajili ya kutoa huduma. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nyang'hwale kuanza kufanya tathmini ya mahitaji ya fedha lakini pia kuanza kutenga bajeti katika mapato ya ndani kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa soko hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, akinamama wanaouza mbogamboga na matunda katika Mji wa Mbulu huweka chini bidhaa zao wanazouza. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuharakisha ujenzi wa soko katika mji huo? Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaelekeza kwamba masoko yote ambayo wananchi wanafanya biashara akina mama na wananchi wengine yaendelee kuboreshwa kwa awamu katika kila mwaka wa fedha. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge tumeichukua hoja hiyo na tutakwenda kuifanyia kazi kuhakikisha kwamba soko hilo linaboreshwa zaidi kwa ajili ya mazingira ya ufanyaji biashara kwa akinamama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kutengeneza Soko la Keko na hasa ukizingatia ni soko kubwa ambalo linatoa pia sofa katika nchi nzima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Soko la Keko ni soko kubwa ambalo linatoa huduma kubwa katika nchi yetu, lakini pia katika Mkoa wa Dar es Salaam na ni wajibu wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kuweka kipaumbele katika ukarabati na ujenzi na maboresho ya soko hilo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti lakini pia kutafuta wadau kwa maana ya *PPP* kwa ajili ya kuboresha Soko la Keko ili biashara ziweze kufanyika katika mazingira mazuri zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava nimekuona isipokuwa sijakupa kwa sababu una swali la msingi huku mbele.

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

Na.133

**Hitaji la Maafisa Afya – Hanang**

**MHE. MOHAMED L. MONNI. K.n.y. MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa kibali cha kuajiri Maafisa Afya Wilaya ya Hanang'?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hutoa vibali vya ajira mpya baada ya kupokea mahitaji ya ikama toka kwa waajiri.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali inatarajia kutoa nafasi tatu za ajira mpya za Maafisa Afya Mazingira zilizoidhinishwa katika Ikama na Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Kwa msingi huo, Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya hii unashauriwa kutenga nafasi zaidi za Maafisa Afya - Mazingira katika ikama na bajeti zao kwa miaka ya fedha ijayo iwapo bado wana uhitaji wa watumishi wa kada za Maafisa Afya -Mazingira. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa kushukuru majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ina changamoto pia kama ilivyo Hanang. Ninataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuajiri Maafisa Afya hao katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Monni kwa namna anavyofuatilia masuala yahusuyo Jimbo lake la Chemba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za Maafisa Afya katika Jimbo lake ninaomba nimwarifu kama jana alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwamba Mheshimiwa Rais ameridhia kutoa kibali tena cha ajira 33,212. Kwa hiyo, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mkurugenzi wa Halmashauri yake fursa ziko hapa aombe na sisi tutampa kipaumbele kwa kumpatia maafisa afya hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay nimekuona, lakini sasa sijajua vizuri maana niko mbali kidogo hiyo ni kanzu ama ni suti? Ni kanzu ama ni suti Mheshimiwa? Fungua kisemeo. Ni kanzu ama ni suti?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ni suti ya Nigeria hiyo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge si mnazijua Kanuni zetu ukivaa kanzu sharti uweke na koti hapo, uweke na baraghashia na uvae makubazi. Ndiyo Kanuni zetu zinasema kwa hiyo lazima nimwulize ili nijue kama nimtambue au hapana.

Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Vijana nchini wanasubiri ajira mpya. Serikali imefikia hatua gani katika kutoa kibali au kutangaza nafasi mpya za ajira nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la Mheshimiwa Zacharia juu ya ajira mpya, kama nilivyosema jana

tulipokuwa tunahitimisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Waziri Simbachawene alisema Mheshimiwa Rais ameridhia kutoa vibali vya ajira 33,212. Hizi ni jitihada na hii ni bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Pia kwa bajeti tuliyopitisha jana kuna ikama imetengwa, kwa ajili ya ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaajiri Maafisa Ugani wa kutosheleza katika Jimbo la Kalenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Grace Tendega kwamba, katika hizi ajira 33,000 mpya nilizozisema hapa, kuna nafasi zimetengwa kwa ajili ya Maafisa Ugani. Ninakushauri uwasiliane na Mkurugenzi wa Halmashauri alete barua ya maombi Ofisi ya Rais, Utumishi. Sisi tutazingatia kulingana na uhitaji wenu katika Jimbo la Kalenga. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SWAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kuajiri watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuwa, tumeshakamilisha ujenzi wa vituo vinne vya afya na zahanati nne ambazo sasa tunashindwa kuzifungua kwa sababu, tunahitaji watumishi kama 119?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma kuhusu suala la wataalam wa kada ya afya; katika hizi ajira mpya nilizozisema kuna takribani zaidi ya ajira 9,000 zitailenga kada ya afya. Kwa hiyo, kama

nilivyosema kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, naye awasiliane na mkurugenzi, aombe na sisi tutazingatia maombi hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Tume ya Utumishi wa Umma, ambayo Mheshimiwa Simbachawene aliipokea, 40% ya watumishi wa Tanzania hawafanyi kazi licha ya kwamba, wanalipwa mshahara. Wamejipangaje kutatua changamoto hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, ni kweli changamoto hiyo Mheshimiwa Waziri aliisema, lakini tumeanza kuchukua hatua mbalimbali. Kwanza, kuweka mifumo ya kufanya *performance improvement* ya watumishi kwa kupima *KPI* kupitia Mfumo wa *PEPMIS*.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umewapa watumishi masharti maalum. Yule ambaye hatafikisha alama kadhaa, tumeweka zaidi ya 60%, hataweza kupandishwa cheo wala kuongezewa mshahara.

Kwa hiyo, hii inawafanya watumishi wawe na *commitment* kubwa kufanya kazi akijua kwamba, baada ya hapo atakosa stahiki zake kwa kutokutimiza hizo asilimia alizowekewa kwenye *PEPMIS*. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 134

**Kupeleka Umeme Vitongoji Visivyo na Umeme, Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vitongoji visivyokuwa na umeme Wilayani Nanyumbu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu ina jumla ya vitongoji 526 ambapo kati ya hivyo, vitongoji 306 vimekwishapatiwa umeme. Vitongoji 115 Wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa miradi na vitongoji 37 zabuni ya utekelezaji wa mradi imetangazwa kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili B *(HEP IIB)*. Serikali itaendelea kutenga fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya kuvipatia umeme vitongoji 68 vilivyosalia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya. Kati ya vitongoji 526, karibu vitongoji 400 na kitu vina umeme, lakini nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza; umezungumza kwamba, vitongoji 37 mko katika hatua ya kutangaza tenda, ili mkandarasi aanze kufanya kazi. Ninapenda kufahamu, ni lini shughuli hiyo itaisha, ili mkandarasi awe *site*, kwa ajili kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ndani ya jimbo langu kumekuwa na changamoto ya kuongezeka nguvu ya umeme, *high voltage,* hasa nyakati za usiku na kusababisha ndani ya mtaa mmoja baadhi ya nyumba kuwa na umeme na nyingine kutokuwa na umeme. Je, Serikali ina mpango gani kurekebisha

hali hii, ambayo inasumbua kwa kipindi kirefu ndani ya jimbo langu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba nijibu maswali yake, kwa pamoja, kama ifuatavyo. Kuhusiana na mradi wa vitongoji 37 tumeshatangaza zabuni. Sasa tuko katika hatua ya kuelekea kufunguliwa zabuni, baada ya hapo tuweze kuanza mchakato wa kuwapata wakandarasi na mradi huu uweze kuanza. Kwa hiyo, hivi karibuni tutafungua zabuni hii katika hatua za kuelekea kupata wakandarasi, kwa ajili kutekeleza mradi huu wa vitongoji 37 katika Jimbo la Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusiana na kuongezeka kwa nguvu ya umeme; ni kweli, katika eneo la Nanyumbu tunatumia line inayotoka Makambako kupitia Songea, Tunduru hadi Nanyumbu na *line* ile kweli, inaleta tatizo la *high voltage*. Tumeshaweka mkakati wa kufunga *reactor* Makambako, kwa ajili ya ku-*control* suala hilo, ili wananchi wa Nanyumbu waendelee kupata umeme ambao unakidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, hatua za muda mfupi za kutumia *line* ya Mtwara, tunaweza kufanya hivyo kwa wakati wa usiku, lakini kwa kipindi hiki kwa sababu, kituo cha Mahumbika uwezo wake umefikia mwisho, tunaomba mtuvumilie tufanye taratibu hizi za muda mrefu za kufunga *reactor* Makambako, kwa ajili ya kutatua tatizo hili katika eneo la Nanyumbu. Niwahakikishie Wananchi wa Nanyumbu tunafanya mchakato kuhakikisha tunaondoa tatizo hili la *high voltage*. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe tena, maswali yawe mafupi na mliosimama nimewaona.

Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kubwa kwa Wizara, ninaomba kuuliza. Kwa kuwa, vitongoji vyote vilivyopangiwa kupata umeme awamu hii

kwa Mkandarasi *MF* na *CCC* hatuna hata kimoja kilichowashwa umeme. Kwa nini, hawa wakandarasi wasiondolewe wakapewa kazi watu wenye uwezo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mkandarasi anayetekeleza mradi huu wa vitongoji 15, *CCC* ni mkandarasi mzuri. Yuko katika hatua za kufanya manunuzi, atafika *site* muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mkandarasi *MF*, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba nimwelekeze *DG* wa *REA,* tulishazungumza, afanye utaratibu akae naye watafute ma-*sub contractors* kwa sababu, uwezo wake tayari unatia mashaka. Kwa hiyo, tutafanya suala hilo, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunatekeleza kazi hii na ikamilike kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migila, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, kila jimbo tulipewa vitongoji 15, baadaye tena tukaambiwa tutoe vitongoji vitano, kama kipaumbele, kwa ajili ya umeme jazilizi. Wananchi tulishawaambia kwamba, umeme unakuja, lakini mpaka hivi tunavyoongea mkandarasi hajafika *site* kuanza kazi. Sasa nini Kauli ya Serikali kuhusu hivi vitongoji vitano tulivyoambiwa ni vya kipaumbele? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Wakandarasi hawa tuliwapata mwishoni mwa mwaka uliopita na kwa utaratibu wa ukandarasi wa miradi ya umeme, huwa tukiwapata tunaanza suala la *survey*, baada ya hapo tunafanya *mobilisation* na tunakagua vifaa, kwa ajili ya wakandarasi kwenda *site*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni hatua za mwanzo ambazo zinachukua muda kidogo mpaka mkandarasi kufika *site*, lakini

kwa sasa niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tumeshamaliza suala la *mobilisation,* tumeshafanya ukaguzi na hivi karibuni wataanza kuwaona wakandarasi kwa kasi katika maeneo yao, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu wa vitongoji 15.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Ukwama imefikishiwa umeme, lakini haujawaka kwa takribani mwaka nzima, kata zaidi ya tatu umeme haujawaka. Ni yapi maelekezo ya Wizara kwa mkandarasi anayetekeleza mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Ninaomba baada ya hapa nikae naye kwa sababu, amezeungumzia suala la tarafa na kata. Sasa nitapenda kujua kwa mahususi ni maeneo gani, ili sasa tuweze kuyafanyia kazi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutakaa, tutazungumza na tutafuatilia ili wananchi waweze kuendelea kupata umeme katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya maswali yako.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 135

**Kupeleka Maji Ziwa Victoria Kata ya Usanda, Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka maji ya Ziwa Victoria katika Kata ya Usanda Halmashauri ya Shinyanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Asweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa awali, kwa ajili ya upanuzi wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria wa Tinde – Shelui kwenda zaidi ya vijiji 30 vya Wilaya za Shinyanga na Iramba. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 na utafanyika kwa kipindi cha miezi 12.

Mheshimiwa Spika, Mradi huo utatekelezwa kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga, yaani *design and build*, ambapo unatarajia kunufaisha wananchi 138,839 waishio kwenye Kata 12 za Wilaya za Iramba na Shinyanga, ikiwemo Kata ya Usanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, katika Mradi huo wa Tinde – Shelui awamu ya kwanza umeshaanza kutekelezwa na kuna tenki ambalo limejengwa katika Kijiji cha Jom, Kata ya Jom, lakini kinahudumia kijiji kimoja tu, tenki kubwa liko pale na Mheshimiwa Makamu wa Rais alikuja akazindua. Swali la kwanza; je, ni lini mtaanza kusambaza maji katika vijiji ambavyo vinazunguka Kata ya Tinde pamoja na Usanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kata ya Nsalala iko kati ya Tinde na Nzega, Nzega kuna maji ila Nsalala hakuna maji. Nini mkakati wa Nsalala kuhakikisha kwamba na Kata ya Nsalala inapata maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa kuyatoa maji ya Ziwa Victoria na kuyaleta katika Mji wa Shinyanga. Tumefanya huu Mradi wa Tinde – Shelui kwa awamu ya kwanza na sasa hivi tuko hatua za mwisho kumpata mkandarasi, kwa ajili ya usambazaji wa vijiji vyote katika

eneo hili la Tinde mpaka Didia. Ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hili jambo tutalifanya kwa sababu, fedha zake zipo. Eneo la Nsalala, katika ile awamu ya pili eneo hilo pia, ni wanufaika katika kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kata ya Kapalamsenga; kutoa maji Ziwa Tanganyika kuleta Kapalamsenga bado haujakamilika mpaka sasa. Hatua ya awali ya kuleta mabomba mpaka kwenye eneo husika ilishafanyika. Ni lini Serikali itajenga matenki na kuhakikisha maji hayo yanawafikia wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kutoa fedha, kusimamia na kufuatilia mradi huo kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama na kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtwara Mjini ni jimbo ambalo linakabiliana na uhaba wa maji. Kuna visima vitatu ambavyo vimechimbwa na Serikali takribani miaka mitatu sasa na mpaka sasa hivi havijamaliziwa. Je, ni lini Serikali watakuja kuvimalizia visima hivyo, ili wananchi wapate maji? Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, tumeshatoa maelekezo, maeneo ambayo yatachimbwa visima lazima ufanyike uboreshaji. Nimwelekeze Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira *(MTUWASA)* kuhakikisha kwamba, hiyo kazi

wanaianza na Wizara ya Maji tuko tayari kutoa fedha kuhakikisha kwamba, hii kazi inaanza mara moja.

**SPIKA:** Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Wilaya ya Muleba ilifanya upembuzi yakinifu, kwa ajili ya kupata maji kutoka Ziwa Victoria tangu 2009 hadi sasa. Nini kauli ya Serikali kuhusu upatikanaji wa maji, kwa ajili ya kata sita kutoka Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Wizara ya Maji ni kuhakikisha tunatumia rasilimali toshelevu za maji, ikiwemo maziwa na mito na tumeshafanya *design*, sasa hivi tuko hatua ya upatikanaji wa fedha. Ninataka nimhakikishie tumeanza utaratibu wa kuwa na *alternative fund* ya kutafuta *bonding* ambazo tumezianza kama Tanga, *UWASA*. Ninataka nimhakikishie Wizara ya Maji tumejipanga kuhakikisha kwamba, tunapata vyanzo mbadala vya utafutaji fedha kuhakikisha miradi hiyo ambayo tumeifanyia upembuzi yakinifu tunaanza kuitekeleza na wananchi waanze kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itasambaza maji yanayotoka katika visima vya Kisarawe II katika Jimbo la Mbagala, hususan Kata ya Toangoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie maeneo ambapo tumeshachimba visima hatua inayofuata ni utekelezaji. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira, tarehe nane tutakuwepo katika bajeti, mambo yote tutayaweka wazi katika kuhakikisha maeneo tunaenda kutekeleza miradi ya maji maeneo mbalimbali. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ilipanga bajeti ya kumalizia visima vya Endesh na Gendish. Ni lini mtapeleka fedha, ili mradi ule wa maji ukamilike?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi ya maji cha kwanza ni upatikanaji wa chanzo, tumechimba visima, kwa ajili ya vyanzo. Hatua inayofuata sasa hivi ni kumpata mkandarasi, kwa ajili ya utekelezaji. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Flatei Massay hiyo kazi tunaiweza, tutahakikisha kwamba tunaianza wananchi hawa waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Ziwa Victoria, tuna Ziwa Nyasa na Mji wa Tukuyu hauna maji. Ni lini Serikali wataleta fedha kuhakikisha maji yanatoka Ziwa Nyasa kufika Tukuyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, moja ya mikakati na maelekezo ya Bunge pia kuwa na *National Grid* kwa maana ya kutumia rasilimali toshelevu kuhakikisha kwamba, zinatumika, kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji. Kwa hiyo, maeneo ya Ziwa Nyasa ni moja ya mikakati ya Wizara yetu. Ninataka nimhakikishie tuko katika hatua mbalimbali za kufanya *feasibility study*. Ninaamini maeneo hayo pia, yatanufaika katika kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, sasa aulize swali lake.

Na. 136

**Kurejesha Kiwanda cha Chai kwa Wakulima wa Lupembe**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha kwa Wakulima wa Chai (MUVYULU) Kiwanda cha Chai Lupembe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Chai Lupembe kwa muda mrefu kinakabiliwa na mgogoro wa umiliki na uendeshaji kati ya wamiliki ambao ni *Dhow Mercantile (EA) Limited* wenye hisa ya 70% na Muungano wa Vyama vya Ushirika Lupembe (MUVYULU) wenye hisa ya 30%. Mgogoro huo ulianza Mwaka 2008 baada ya kiwanda hicho kubinafsishwa mwaka 2004 na iliyokuwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)*.

Mheshimiwa Spika, kufuatia makubaliano kati ya Serikali, *Dhow Mercantile* na MUVYULU, mwekezaji *Dhow Mencantile (EA) Ltd* amekubali alipwe fidia, ili kiwanda hicho kiweze kurejeshwa kwa wakulima wa MUVYULU. Serikali kupitia Msajili wa Hazina inakamilisha uthamini wa mali za kiwanda hicho, kwa ajili ya hatua za mwisho za majadiliano na mwekezaji huyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaishukuru sana Serikali kwa uamuzi mzuri wa kurejesha kiwanda hiki kwa wananchi wa Lupembe. Nina maswali mawili madogo ya

nyongeza; Swali la kwanza, kiwanda hiki kimefanyiwa tathmini zaidi ya mwaka mmoja sasa na mpaka leo bado hakijarejeshwa kwa wananchi. Mahakama Kuu ilitoa amri kwamba, Ofisi ya Hazina ndio wasimamie mchakato wa uthamini na kurejesha kiwanda hiki, lakini mpaka leo wananchi wa Lupembe hawajui hasa ni nini kinaendelea. Ninaomba kupata majibu ya Serikali, ni nani hasa anakwamisha mchakato huu, ni Hazina, ninyi Wizara ya Kilimo au ni Bodi ya Chai?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, wananchi wa Tarafa ya Lupembe, kwa maana ya Kata ya Idamba, Mfiriga, Lupembe yenyewe, Matembwe na Ukalawa wanalima sana chai na soko la chai bado pia, ni changamoto kubwa. Ninaomba kauli ya Serikali, ni upi mpango kabambe wa kutafuta soko la uhakika kwa wakulima wa chai wa Lupembe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikiri kwamba, Mheshimiwa Edwin Swalle, Mbunge wa Lupembe, ni moja ya Mbunge, ambaye amekuwa akipigania sana zao la chai hapa nchini. Hata hii hatua ambayo tumefikia ni pamoja na mchango wake mkubwa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na kuchelewa kwa mchakato huu hakuna yeyote anayekwamisha, sio Msajili wa Hazina, Bodi ya Chai wala sisi Wizara ya Kilimo, isipokuwa tu ni taratibu ambazo zinatumika katika ufanyaji tathmini wa hii kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nimeeleza katika jibu la msingi kwamba, tuko kwenye hatua za mwisho za tathmini na ninaamini kabisa hatutaki kufanya makosa yoyote, ili kile kiwanda tunapokirudisha kwa Chama cha MUVYULU tuwe tunalipa fidia bila kuleta mgogoro mwingine wowote. Kwa hiyo, tuko vizuri na tutamaliza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni mkakati wa Serikali katika zao la chai, hususani Jimbo la Lupembe. Mkakati wetu wa sasa ni kwamba, tunazishirikisha sekta binafsi pamoja na vyama vya ushirika na lengo letu ni kuviwezesha viweze kutengeneza

viwanda vidogovidogo, kwa ajili ya kuongeza thamani ya zao la chai, ili tuweze kuwasaidia wakulima hao. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati wa sasa, ili tuweze kulikabili soko la ndani pamoja na soko la nje. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ukiacha Kiwanda cha Lupembe bado kuna viwanda vingine vitano vinavyomilikiwa na Kampuni ya *DL* pale katika Mkoa wa Njombe ambavyo vimedorora. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha viwanda hivyo vimefanya kazi au mwekezaji ananyang'anywa viwanda hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema kwamba katika ile tathmini inayofanyika ukiacha katika Kiwanda cha Lupembe ni pamoja na viwanda vingine vitano ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviainisha hapo na baada ya tathmini tutatoa majibu ya jumla. Vipo viwanda ambavyo tutavichukua na viko viwanda ambavyo tutaviboresha ili viweze kusaidia wakulima wetu wa zao la chai.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kufufua Viwanda vya Pamba vya Nasa *Ginnery* na Ngasamo ambavyo vilikuwa vinamilikiwa na Nyanza Mkoani Simiyu, Jimbo la Busega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, mpango tulionao sasa hivi, tuna aina mbili za mipango. Moja; kuna viwanda ambavyo tutavipeleka katika vyama vya ushirika na sisi Wizara tutatoa fedha kwa ajili ya kuviboresha ili vitumike.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo mpango tulionao ni kutafuta wawekezaji ili waweze kuwekeza katika viwanda hivyo ambapo watakuwa wanunuzi wakubwa wa zao la pamba kwa ajili ya wakulima. Kwa hiyo, hiyo ndio mipango yetu ambayo tuko nayo sasa hivi na iko katika mkakati ambao upo katika utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 137

**Kulinda Soko la Matunda Nchini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kulinda Kilimo cha Matunda nchini ili kuokoa Soko la Matunda linalosuasua kutokana na uingizaji mkubwa wa matunda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kulinda soko na kudhibiti uingiaji holela wa matunda nchini, Serikali imechukua hatua mbalimbali zikiwemo kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(COPRA)* ambayo itaweka utaratibu wa kuwezesha uingizaji na usafirishaji nje wa mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko yakiwemo matunda, kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya kusindika matunda ili kuimarisha soko la ndani na kupunguza upotevu, kutoa ruzuku ya pembejeo kwa mazao ya matunda ikiwemo maembe, machungwa na parachichi ili kuongeza tija na kuimarisha utafiti na uzalishaji wa mbegu na miche bora ya matunda kulingana na mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo itaongeza uzalishaji wa matunda kutoka tani 6,530,302 mwaka wa fedha 2022/2023 hadi tani 7,065,139 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga ni maarufu sana kwa kilimo cha matunda na hasa machungwa, lakini machungwa yetu bado hayajapata soko zuri kwenye viwanda. Swali la kwanza; ni upi mkakati wa kuboresha kilimo cha matunda ili kuweza kukidhi mahitaji ya viwandani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; pamekuwa na changamoto kubwa ya kuoza kwa matunda kabla ya kufika sokoni. Ni upi mkakati wa kujenga vyumba baridi *(cold rooms)* kwa ajili ya kuhifadhi matunda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, moja; nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua kwamba Mkoa wa Tanga ndiyo moja ya Mkoa ambao tunautegemea sana kwa mazao ya mchungwa na tunakiri kabisa kwamba kuna changamoto kubwa vilevile katika kuoza kwa matunda hayo ambayo imekuwa ni moja ya jitihada kubwa ambayo tunayo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ambayo tumeifanya sasa hivi ni kuhamasisha Sekta Binafsi kuingia katika kujenga viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao hayo kama kutoka katika tunda kutengeneza *juice* na Tanga ndiyo mkoa wa kipaumbele ambao sasa hivi tumeuweka.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti upotevu wa mazao kutokana na kuoza ni kwamba sasa hivi tunao mpango madhubuti na tumepata fedha kutoka *African Development Bank* kwa ajili ya kujenga hizi *cold rooms* kwa ajili ya kuhifadhia haya matunda. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia ya kupeleka sokoni matunda ambayo hayajakomaa na hili lina athari katika ubora kutokana na kwamba yanakosa ladha na virutubisho vinakuwa havijakamilika kutengenezwa katika matunda. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni kweli na sisi kama Wizara kauli yetu ni moja tu. Kwanza, hilo jambo haliruhusiwi na kuna wakati palikuwa na mnunuzi alinunua parachichi kutoka Njombe ambazo zilikuwa hazijakomaa na matokeo yake zilienda zikatupwa zote pale Dar es Saalam kwa sababu zilioza kabla ya muda na kwa sababu zilikuwa hazijakomaa.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua ambayo sisi Wizara tulichukua ni pamoja na kumfutia leseni ya kutokushiriki katika biashara ya mazao hapa nchini kutokana na kuenenda kinyume na taratibu ambazo tumeziweka. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kufuatilia na kuwachukulia hatua wale wote wanaonunua matunda ambayo hayajakomaa kwenda katika masoko yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu na sasa nitaleta tangazo linalohusu wageni tulionao hapa Bungeni. Kwanza tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Hawa ni viongozi na watendaji wa Ofisi hiyo.

Yupo Dkt. Tausi Kida ambaye ni Katibu Mkuu. Hajapata nafasi ya kuingia ama hajaja, lakini nimewekewa jina lake hapa. Kwa hivyo sijajua amepatwa na changamoto gani. *(Makofi)*

Wapo pia, Dkt. Binilith Mahenge, Mwenyekiti wa Bodi Kituo cha Uwekezaji *(TIC);* Ndugu Gilead Teri, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania; Ndugu Charles Itembe, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje; Dkt. Lora Madete, Naibu Katibu Mtendaji, Biashara na Ubunifu; na Dkt. Mursali Milanzi, Naibu Katibu Mkuu Mtendaji Mipango ya Kitaifa, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Saalam wakiongozwa na Ndugu Nicole Mkame, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ambao ni watendaji wa Shirika la Kimataifa la *Christian Blind Mission (CBM)* kutoka Tanzania na Kenya wakiongozwa na Ndugu Nesia Mahenge ambaye ni Mkurugenzi Mkaazi *CBM* Tanzania. Pia wapo Ndugu Lulu Mshana, Meneja wa Miradi *CBM* Tanzania; Ndugu Richard Dalu, Afisa Miradi *CBM* Tanzania; na Ndugu James Kasombo, Mratibu wa Sera Mambo ya Ulemavu Duniani kutoka Kenya. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na wageni 120 wa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Hawa wageni wako makundi mengi kidogo, wamesimama wote pamoja; sawa basi endeleeni kusimama mpaka wote mtajwe. Haya wapo Wenyeviti wa UWT na Makatibu wa Kata UWT Jimbo la Ismani. *(Makofi)*

Wapo Wenyeviti, Makatibu na Makatibu Malezi wa Jumuiya ya Wazazi Kata, Jimbo la Ismani. Wapo Wenyeviti, Makatibu na Makatibu wa Hamasa Umoja wa Vijana wa CCM Kata Jimbo la Ismani. Wapo Maafisa Watendaji Kata wa Jimbo la Ismani na

Maafisa Tarafa wa Jimbo la Ismani. Haya karibuni sana Bungeni, tumefurahi sana kuwaona. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lukuvi hajamaliza bado wageni. Yupo mgeni wake ambaye ni baba mzazi wa mchezaji mpira; huyu baba anaitwa Cretus Luvanga, anatoka Ismani, Pawaga, karibu sana. Huyu ni mzazi wa mchezaji anayeitwa Clara Cretus Luvanga ambaye alitokea Timu ya Yanga Princess na sasa anacheza Timu ya Al Nassr ya Saudi Arabia ya Wanawake. Kwa hiyo, anacheza mpira wa miguu huyu. *(Makofi)*

Sasa hapa msisistizo umewekwa kwamba hii Timu ya Al Nassr ya Saudi Arabia ya Wanaume ni ile ambayo anachezea Cristiano Ronaldo ili kuonesha msisitizo na uzito wa hii timu anayochezea huyu binti kutoka Ismani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, huyu ni mpigakura wake kutoka Babati Vijijini Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni kikundi cha *Smart Group* kutoka Ihumwa Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ambao ni wapigakura wake na marafiki zake kutoka Bukoba Vijijini Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina ambao ni wapigakura wake kutoka Paje. Kama ni wapigakura wake mbona wanatoka Paje? Jamani siyo nyie waandishi hapa mmechanganya mambo? Hawa wanatoka Paje au wanatoka Makunduchi? Wanatoka Paje aah sawa, ni wageni wake wanatoka paje, lakini wapigakura wake ni wa Makunduchi, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. John na Chuo Kikuu

cha Dodoma wanaotokea Donge Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ambao ni watoto wake kutoka Muleba Mkoani Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo walimu sita na wanafunzi 50 wa Darasa la Saba kutoka Shule ya Msingi Hannah Bennie Iliyoko Kibuguru, Wilaya ya Kigamboni Mkoani Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi 65 wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Tawi la Chuo Kikuu cha Sokoine kutoka Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wananchi wawili kutoka Kata ya Nzuguni Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao hapa Bungeni na wengine tutaendelea kuwataja kadri watakapopata nafasi ya kuingia hapa ndani. Tunaendelea na ratiba yetu sasa.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni

na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo imechambua mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji - Fungu 11, Ofisi ya Msajili wa Hazina - Fungu 07 na Tume ya Taifa ya Mipango - Fungu 66 kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote tumeaswa kuwa kila tunapopata nafasi hatuna budi ya kumshukuru Mungu na kuwashukuru watu ambao wameleta tofauti katika maisha yetu. Ninamshukuru Mungu kwa wingi wa rehema, baraka na fadhili zake kwangu iliyoniwezesha kusimama hapa mbele kuwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji nafasi ambayo leo imenipa fursa ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambayo ni hotuba ya mwisho kwa Bunge hili la Kumi na Mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa utulivu na hekima za uongozi wake ambazo Mwenyezi Mungu amemjalia pamoja na juhudi zake za dhati alizoziweka katika kuendeleza nchi yetu ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea. Kipekee na muktadha wa majukumu ya ofisi yangu, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha diplomasia ya uchumi iliyochochea kuongezeka kwa mashirikiano baina ya nchi yetu na nchi mbalimbali duniani, kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuitangaza nchi yetu kuwa kivutio na mahali salama kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kutekeleza majukumu yake vyema, lakini kwa kipekee tumshukuru kwa jinsi ambavyo ametusaidia sana katika zoezi la maandalizi ya Dira ya

Taifa ya Maendeleo ambaye yeye alikuwa ni wa kwanza kuzindua kongamano la kwanza la Dira ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru na kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na jitihada kubwa ambazo anazifanya katika kuiendeleza Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tunamshukuru Dkt. Mwinyi kwa kuwa yeye ndiye aliyezindua rasimu ya kwanza ya Dira Mwezi Desemba pale Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake ya kuendesha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwani amekuwa nasi katika mwaka huu. Alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Maandalizi ya Dira na ametuongoza vizuri sana katika jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, niungane na Mawaziri wenzangu walionitangulia kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge letu kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vizuri sana, Bunge la Kumi na Mbili. Uongozi wako makini, umahiri wako katika kujua masuala mapana ya kibunge hapa nchini na duniani kwa jinsi ambavyo unapenda kutenda haki kwa Wabunge wote bila kujali hali na nafasi zao na upendo wako kwa Wabunge wenzako ni mambo ambayo yataacha alama ya kudumu ya uongozi wako katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna shaka kwamba Bunge hili linakuhitaji, Wabunge hawa wanakuhitaji, Watanzania wanakuhitaji, dunia inakuhitaji na muhimu zaidi wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini wanakuhitaji sana. Tunakuombea na

kukutakia kila la heri katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi mahiri na imara wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bunge na Makamu wake Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge kwa ushirikiano, maelekezo, maoni na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Wajumbe hawa kuwa ushauri na maelekezo yao yamezingatiwa kikamilifu na yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa hotuba hii. Kamati hii ni Kamati imara sana na Wajumbe wake ni watu muhimu. Tunawaombea sana wananchi katika majimbo yao wawarudishe katika Bunge lijalo la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, ninaomba sasa nilete mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni kutunga, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera na mikakati kuhusu mipango ya maendeleo ya nchi yetu, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji na kuratibu utekelezaji wa mikakati ya Serikali ya kuboresha mazingira ya biashara ya uwekezaji nchini. Katika kutekeleza majukumu haya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaratibu na kusimamia taasisi nne za Serikali ambazo ni Tume ya Taifa Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na Mamlaka ya Uzalishaji ya Mauzo ya Nje *(EPZA)*.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2024/2025. Bunge lako Tukufu liliidhinishia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji bajeti ya shilingi bilioni 121.33 kwa mgawanyo wa shilingi bilioni 1.25 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 21.08 kwenye matumizi ya miradi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi bilioni 82.36 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 17.89 kwa ajili ya mishahara. Aidha, matumizi ya miradi ya maendeleo yanajumuisha shilingi bilioni 15.59 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.49 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya mapitio ya bajeti ya nusu mwaka, bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliongezeka kwa njia ya uhamisho kati ya Mafungu na kufikia shilingi bilioni 275.03. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 253.74 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 21.29 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025, Mafungu matatu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji yamepokea na kutumia shilingi bilioni 171.47 sawa na asilimia 62.35 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango na bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 664.53 ikiwa ni maduhuli yanayotokana na gawio, michango ya 15% ya mapato ghafi ya taasisi yanazozichangia. Mapato yanatokana na uendeshaji wa mfumo wa usimamizi wa mawasiliano ya simu Tanzania, rejesho la riba na mikopo, ziara na malipo mengineyo hii ni sawa na 86% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 786.58 kwa kipindi kinachorejewa na 60% ya lengo la kukusanya la mwaka la kukusanya shilingi trilioni 1.113.

(ii) Kuendelea kuratibu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo. Maandalizi haya yapo katika hatua ya mwisho ambapo rasimu ya Dira 2050 inafanyiwa kazi katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali kabla ya kuwasilishwa Bungeni kwa hatua zaidi.

(iii) Kuratibu maandalizi ya kuandaa mpango elekezi wa muda mrefu *(long-term perspective plan - LTPP)*. Sambamba na maandalizi ya Dira ya 2050, Tume ya Taifa ya Mipango inaendelea na maandalizi ya mpango elekezi wa muda mrefu. Mpango huu ndiyo utakuwa mkakati mama wa utekelezaji wa dira 2050. Utakaotumika kama mwongozo wa maandalizi ya mipango ya taifa ya miaka mitano na mipango ya maendeleo ya Taifa ya kila mwaka.

(iv) Kuendelea kuratibu mikakati ya Serikali ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika mwaka 2024/2025. Serikali iliendelea na utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (MKUMBI) unaolenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuondoa changamoto mbalimbali katika taratibu za uwekezaji na ufanyaji biashara.

(v) Kuendelea kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji nchini unaoratibiwa na Kituo cha Uwekezaji, Mamlaka ya *EPZ* na Taasisi zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika sekta ya uwekezaji hupimwa kwa kuzingatia vigezo vikubwa vitatu. Vigezo hivi ni idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa, idadi ya ajira zinazozalishwa kupitia miradi hiyo na mtaji uliyovutiwa kutokana na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya kuhamasisha, kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa miradi ya uwekezaji nchini hufanywa na kusimamiwa na taasisi mbili *(TIC & EPZ)* pamoja na taasisi zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilisajili jumla ya miradi mipya 691 yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 7.997 na ambayo ilitarajiwa kuzalisha ajira mpya 298,257 hii ni sawa na ongezeko la 35.8% ikijumlisha na miradi iliyosajiliwa mwaka 2023/2024 ikiwa na thamani ya dola za Kimarekani bilioni 5.8.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Awamu ya Sita, idadi ya miradi iliyosajiliwa na *TIC* imeongezeka kutoka miradi 256 kwa mwaka yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 3.749 mwaka 2021 hadi kufikia miradi 901 yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 9.313 mwaka 2024. Sekta tano zinazoongoza kusajili miradi mingi ya uwekezaji ni uzalishaji viwandani 42%, usafirishaji 15.3%, ujenzi wa majengo ya biashara 10.1%, utalii asilimia 8.4 na kilimo asilimia 7.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yamepatikana pia katika uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi *(special economic zones)* ambapo huratibiwa na mamlaka ya *EPZ*. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita jumla ya miradi 45 imesajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini kupitia leseni za *EPZ* na *SEZ* miradi hiyo imevutia mitaji ya jumla dola za Kimarekani bilioni 1.172 na kuongeza ukuaji wa mauzo ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania na nje ya nchi yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 397.64 na kuzalisha ajira zipatazo 20,674.

Mheshimiwa Spika, rekodi zinaonyesha kuwa kabla ya sasa idadi kubwa ya miradi ya uwekezaji ilisajiliwa mwaka 2013 na kabla ya sasa mwaka 2013 ndiyo mwaka uliokuwa unajulikana kuwa ni mwaka bora kwa uwekezaji nchini ikiwa imesajili miradi 885. Hata hivyo, mwaka 2024 *TIC* ilisajili miradi 901 na hivyo kuvunja rekodi ya miradi iliyosajiliwa katika kipindi cha miaka 29. Kwa sababu hii tunaweza kuutangaza mwaka 2024 sasa kuwa mwaka bora zaidi katika sekta ya uwekezaji Tanzania tangu Tanzania ianze kusajili Miradi ya Uwekezaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa tathmini iliyofanywa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji mafanikio katika Sekta ya Uwekezaji yamechangiwa na sababu tano zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuhimarisha mifumo ya kisera na kisheria katika kuwezesha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Kwa mfano, katika kipindi cha Bunge la Kumi na Mbili, Sheria ya Uwekezaji imeshafanyiwa mabadiliko mara mbili.

(ii) Maono, hamasa na ushawishi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa makampuni aliyofanya, makampuni mbalimbali ya kimataifa kuja kuwekeza nchini kupitia ziara na mikutano mbalimbali aliyoifanya nje na ndani ya nchi.

(iii) Kampeni kubwa ya Kitaifa ya Kuhamasisha Uwekezaji Nchini iliyofanyika mwaka 2023 kwa ushirikiano mkubwa kati ya *TIC*, Taasisi za Sekta Binafsi pamoja na Vyombo vya Habari. Jumla ya wafanyabiashara 1,800 walifikiwa kupitia kampeni hii kutoka katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kampeni hii imeweza kuongeza idadi ya miradi iliyosajiliwa *TIC* na Watanzania na kubadilisha taswira ya *TIC* kwamba siyo taasisi ya kusajili miradi ya uwekezaji kutoka nje pekee lakini Taasisi ya Watanzania.

(iv) Kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma kwa wawekezaji katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania ambapo sasa kuna taasisi 14 zinazotoa huduma katika kituo cha pamoja na;

(v) Viongozi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuendelea kuhamasisha shughuli za uchumi na uwekezaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mafanikio tunayoyataja katika sekta ya uwekezaji siyo tarakimu tu katika kompyuta na makaratasi, mafanikio haya ni miradi halisi inayoendelea kutekelezwa katika Mikoa mbalimbali na ambayo inagusa maisha ya wananchi moja

kwa moja, kuchangia ukuaji uchumi, kutengeneza ajira na kuzalisha kodi za Serikali, katika kuonyesha hili ninaomba kutaja baadhi ya miradi ya uwekezaji kama kielelezo cha kuhadithia miradi ya uwekezaji ya kimkakati iliyoanzishwa katika kipindi cha miaka minne iliyopita (2021- 2024):-

(i) Mradi wa Kutengeneza Vioo vya Ujenzi wa Kampuni ya *KEDA Ceramics Company Limited* uliyopo Mkuranga Mkoani Pwani, mradi huu unazalisha vioo vya ujenzi na 80% ya vioo hivi huuzwa nje ya nchi na hivyo kuchangia upatikanaji wa fedha za kigeni na kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 620 na kuajiri watu 43,000.

(ii) Mradi wa kuzalisha mabati wa Kampuni ya *Lodhia Industries* uliyopo Wilaya ya Mkuranga Mkoani Pwani, unaozalisha jumla ya tani milioni 1.2 kwa mwaka ukilinganisha na mahitaji ya ndani ambayo ni takribani tani 600,000 kwa mwaka, na hivyo kuchangia mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi. Kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 52 na kuajiri watu 2,200. Kwa hiyo, kwa sasa mahitaji ya mabati nchi hii, nchi nzima ni mabati tani 600,000, tunazalisha kwa Kampuni moja tu tunazalisha tani milioni 1.2 kwa hivyo, sasa nchi yetu haina sababu ya kuagiza mabati kutoka nje tunajitosheleza kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

(iii) Mradi wa Kuzalisha Mabati wa Kampuni ya *Kinglion Steel Mill* iliyopo Kibaha, Pwani ambao unawezesha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vingine vya mabati na upatikanaji wa fedha za kigeni kutoka nje ya nchi. Kabla ya mradi huu tulikuwa hatuna malighafi ya kuzalisha mabati nchini ilibidi kuagiza kutoka nje, kwa mradi huu sasa ambao umewekezwa dola za kimarekani milioni 42. Sasa hatuhitaji kuagiza malighafi kutoka nje kwa ajili ya kutengeneza mabati na mradi huu umeajiri watu 2,000.

(iv) Mradi wa kongani wa viwanda wa Kampuni ya *Sino Tan Industry Park* uliopo Kikwara, Mkoani Pwani kule Kibaha, mradi huu una lengo la kuvutia viwanda vikubwa na vya kati 200 na viwanda vidogo 300. Kampuni hii inatarajia kuwekeza jumla ya dola za Kimarekani milioni 327 na mradi huu unatarajia kuajiri watu 100, 000 utakapokamilika katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Hadi sasa kampuni imeishawekeza dola za kimarekani milioni 36 na kuajiri watu 651.

(v) Mradi wa kuzalisha saruji wa Kampuni ya Maweni *Limestone Limited* uliyopo Tanga kwa ajili ya uzalishaji wa saruji, kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 170 na kuajiri watu 904.

(vi) Mradi wa kuzalisha vinywaji vya kileo wa Kampuni ya *Mati Super Brands* uliyopo Manyara pale Babati, Kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 2.64 na kuajiri watu 269.

(vii) Mradi wa kuzalisha vifaa vya ujenzi wa Kampuni ya Ziwa *Steel and Wire Product Limited* uliopo Jijini Mwanza, ambapo wakazi wa Mwanza na Mikoa ya jirani sasa wamehakikishiwa upatikanaji wa vifaa vya ujenzi kwa bei nafuu. Kabla ya hapo wakazi wa Ziwa Victoria walilazimika kuagiza vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam, kwa kampuni hii sasa wanapata vifaa hivi ndani ya Mkoa wa Mwanza na kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 3.4 na kuajiri watu 508.

(viii) Mradi wa uzalishaji wa vinywaji baridi wa Kampuni ya *A-One Product and Bottles Limited* uliopo Jijini Mbeya, kampuni hii imewekeza jumla ya dola za Kimarekani milioni 30 na kuajiri watu 150.

(ix) Mradi wa kuzalisha vinywaji baridi wa kampuni ya *Dew Drop Drinks Company Limited* uliopo Mkoani Rukwa,

Kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 20 na kuajiri watu 150 na;

(x) Mradi wa Kilimo cha Parachichi, ufungashaji na uchakataji wa mafuta ya parachichi wa Kampuni ya *Avo Africa Tz Limited,* uliopo Mkoani Njombe ambao umehakikisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima wa parachichi katika mkoa huu na mkoa wa jirani, kupatikana kwa bidhaa za mafuta na upatikanaji wa fedha kigeni. Kampuni hii imewekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 4.8 na kuajiri watu 650. Kabla uwekezaji huu kule Njombe, Iringa maparachichi yalikuwa yanatupwa na walikuwa wanalalamika wananunua kilo moja kwa shilingi 100. Kwa sasa, kuna furaha kubwa kwa wakulima akinamama kule, kiwanda kinanunua maparachichi yote, sasa bei imepanda kutoka kilo moja shilingi 100 hadi shilingi 900 huu mradi muhimu sana na wananchi wameupokea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimetaja miradi hii kama kielelezo kwamba tunapozungumzia mafanikio katika sekta ya uwekezaji, mafanikio ambayo Mheshimiwa Rais anaimiza wawekezaji kuja mafanikio haya siyo ya kwenye marakatasi ni hali halisi ambayo ipo kwa wananchi na wananchi wetu wanafaidika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi zingine ambazo zilifanywa katika mwaka wa fedha 2024/2025 ni pamoja na:-

(i) Kufanya tathmini ya thamani ya uwekezaji na athari za miradi ya kielelezo na mikakati katika kuendelea na kukuza uchumi.

(ii) Kukamilisha uandaaji wa sera mpya ya uwekezaji na mkakati wa utekelezaji.

(iii) Kukamilisha uunganishaji kituo cha uwekezaji Tanzania *TIC* na Mamlaka ya maeneo ya uzalishaji ya mauzo nje *(EPZA)*.

(iv) Kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa sera na miongozo ya uwekezaji wa sekta binafsi.

(v) Uendelezaji wa miradi ya kitaifa ya kielelezo ikiwemo maeneo maalum ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati ya Serikali katika kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini. Katika kupima hatua zilizopigwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, Tanzania ilishiriki katika utafiti wa urahisi wa ufanyaji biashara na uwekezaji uliofanywa na Benki ya Dunia ambao kwa sasa unatambulika kama *Business Ready* ukichukua nafasi ya *easy of doing business.*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya utafiti huu ya mwaka 2024 iliyohusisha nchi 50 duniani. Tathimini katika bara la Afrika, utendaji wa Tanzania katika taarifa hii ya mwaka 2024 ikiwa na maeneo matatu. Katika eneo la uboreshaji wa mifumo ya kisheria Tanzania ilishika nafasi namba saba ikipata alama 65 katika nchi 50 na katika eneo la huduma za umma Tanzania ilishika nafasi ya nne ikiwa na alama 51.56 na katika eneo la ufanisi wa uendeshaji wa biashara *(operation efficiency)* Tanzania ilishika nafasi ya saba ikiwa na alama 62.15. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi tumejipanga kuendelea kufanya vizuri zaidi katika awamu ya pili ya utafiti huo unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuimarisha mifumo ya usimamizi na tathmini ya utendaji wa taasisi za Mashirika ya Umma. Kampuni tanzu na makampuni ambayo Serikali ni mbia pamoja na Mashirika yaliyobinafsisha. Katika kutekeleza jukumu hili Ofisi ya Msajili ilitekeleza majukumu kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kwanza kukamilisha tathmini ya utekelezaji wa mikataba ya utendaji kazi ambao uliingiwa mwaka wa fedha 2022/2023 ya Taasisi na Mashirika ya Umma hadi Machi,

2025. Tathmini imefanyika kwenye taasisi na mashirika ya umma 34 kati ya 50 yaliyopangwa kufanyika sawa na ufanisi wa 68%, maandalizi ya kufanya tathimini kwa Taasisi za Mashirika ya Umma 16 yaliyosalia yanaendelea.

(ii) Kufanya ukaguzi wa kimenejimenti katika Taasisi na Mashirika ya Umma 36 sawa na 72% ya lengo la kukagua mashirika 50.

(iii) Kuendelea na ujenzi wa *dashboard* wenye lengo la kuboresha usimamizi katika uendelezaji Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma.

(iv) Kuandaa taarifa za fedha ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuiwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa sheria. Taarifa hiyo inaonesha kuwa uwekezaji wa Serikali katika Mashirika ya Umma 253 yanayomilikiwa na Serikali kama mbia mkuu pamoja na Makapuni 56 ambayo Serikali inamiliki hisa chache umeongezeka kwa 15.35% kutoka shilingi trilioni 75.79 katika mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia shilingi trilioni 86.29 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na ongezeko la thamani ya mizania ya kampuni ikiwepo Benki ya *NMB, NBC,* Kilombero *Sugar, TPC* na *Air Tanzania Limited (PLC)*.

(v) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa jili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo wa Taasisi za Umma. Ikiwemo Shirika la Nyumba Tanzania ambao ulipatiwa mkopo wa shilingi bilioni 269.33, Chuo cha Uhasibu Arusha bilioni nane, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* shilingi bilioni 27.58, Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro shilingi bilioni 266.68, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara *(MTUWASA)* shilingi bilioni 1.22.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kazi ambazo zilifanyika kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mafanikio yake sasa ninaomba kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2025/2026. Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ina utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa majukumu na vipaumbele katika Mafungu Matatu kama ifuatavyo:-

Maeneo ya vipaumbele kwa Fungu Na. 11 ni kama vifuatavyo:-

(i) Kukamilisha mchakato wa kuunganisha Taasisi za *TIC* na *EPZA* na kuunda Taasisi ya *TISEZA (Tanzania Investment and Special Economic Zones)* ikiwa ni sehemu ya utekeleza wa Sheria ya Uwekezaji na maeneo maalum ya kiuchumi ya mwaka 2025 ambalo Bunge lako lilipitisha katika Mkutano uliopita.

(ii) Kuendelea kuratibu maandilizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo, Mpango wa Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano kwa kuzingatia Dira Mpya ya Maendeleo ya Mwaka 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka kwa mujibu wa Mwongozo wa Dira ya Maendeleo wa Mwaka 2025.

(iii) Kuratibu ushiriki wa nchi na kusimamia majadiliano ya Mikataba ya Kimataifa ya uwekezaji baina ya nchi katika ngazi za kikanda na kimataifa;

(iv) Kuratibu na kusimamia uwekezaji katika Kanda Maalum za Kiuchumi na Kongani za Viwanda;

(v) Kuratibu na kusimamia uwekezaji wa umma;

(vi) Kuratibu uhamasishaji na wawekezaji wa sekta binafsi;

(vii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; na

(ix) Kuandaa mpango wa pili wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa na Tume ya Taifa ya Mipango, Fungu 66 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na mpango elekezi wa muda mrefu pamoja na nyenzo muhimu za utekelezaji wa Dira ya Mwaka 2050 na kutoa elimu kwa umma;

(ii) Kukamilisha maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2025/2026;

(iii) Kuanza maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2031/2032);

(iv) Kufanya tathmini ya matokeo ya miradi kuendelea na kukuza uchumi;

(v) Kufanya utambuzi wa maeneo muhimu ya vipaumbele vya kitaifa yenye matokeo makubwa ili kuainisha na matumizi yenye tija na rasilimali za nchi;

(vi) Kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi na kutoa miongozo ya mashirikiano kwa ajili ya kufanikisha upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa; na

(vii) Kuendelea kuimarisha utendaji kazi wa taasisi kupitia Mifumo ya TEHAMA na kuwajengea uwezo watumishi katika kusimamia uchumi, upangaji na utekelezaji wa mipango.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu Na.7 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukusanya Mapato ya Serikali yasiyo ya kikodi kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma;

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu Na.7 imepangiwa kukusanya na kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya shilingi trilioni 1.56 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasiyo ya kikodi kupitia gawio, michango ya 15% ya mapato ghafi yatokanayo na Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu, wezesho la riba na mikopo ziara na mapato mengineyo.

(ii) Kukamilisha na kuanza utekelezaji wa mapango wa muda mrefu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina;

(iii) Kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Mali za Serikali zilizo chini yya Ofisi ya Msajili wa Hazina Pamoja na ofisi zilizobinafsishwa ikiwemo mashamba viwanda viwanja;

(iv) Kuendela kuimarisha Mifumo ya TEHEMA, ili kuongeza ufanisi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina katika ya ukusaji wa mapato ya siyo ya kikodi.

(v) Kuimarisha usimamizi na tathmini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kampuni tanzu na kampuni ambazo Serikali ni mbia; na

(vi) Kuendelea kujenga uwezo wa Watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, ili kuimarisha utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kifedha mpya inayotarajia kuanza rasmi majukumu yake tarehe Mosi Julai, 2025 ikiwa ni matokeo ya kuunganishwa kwa Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZA)* na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*, imepangiwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kuzindua na kutangaza Mradi wa Bagamoyo (Special Economic Zone) kwa uwekezaji wa ndani na nje ya nchi, kwa nia ya kuendeleza mradi huu kwa njia mbalimbali

ikiwepo ubia na sekta binafsi kwa kufuata mpango uliorejewa;

(ii) Kubaini bidhaa na kutumia huduma za Soko la Mitaji kupata fedha za kuendeleza miradi ya maeneo maalumu ya kiuchumi;

(iii) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwenye maeneo maalumu ya kiuchumi kupitia dirisha la huduma mahali pamoja, kwa kutumia Mfumo wa Kidijiti;

(iv) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo ya viwanda vilivyokabidhiwa kwa Mamlaka ya Msajili wa Hazina;

(v) Kuendeleza maeneo maalumu ya kiuchumi kwa kushirikiana na TAMISEMI, sekta binafsi na wadau wa maendeleo;

(vi) Kutoa elimu kwa umma, kufanya utafiti, kufuatilia tathmini ya miradi iliyopewa leseni na Mamlaka;

(vii) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa;

(viii) Kuboresha mifumo ya kusajili na kuhudumia wawekezaji;

(ix) Kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kutoa majawabu, kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuibua fursa mpya za uwekezaji;

(x) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya uwekezaji; na

(xi) Kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuboresha mashirikiano kati ya kifedha na wadau wa umma na binafsi, ili kurahisisha jukumu la kuratibu uhamasishaji wa huduma kwa wawekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia kazi na majukumu ambayo nimeyataja hapo juu. Ninaomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na likubali kuidhinisha jumla ya shilingi 148,629,961,000/- kwa mgawanyo wa shilingi 122,122,685,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 26,507,276,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mchanganuo wa kimafungu kama ifuatavyo:-

Fungu 11, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, matumizi ya kawaida shilingi 22,392,185,000, matumizi ya maendeleo shilingi 15,475,308,000. Jumla kwa hili Fungu 11 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni shilingi 37,867,493,000;

Fungu 66, Tume ya Taifa ya Mipango matumizi ya kawaida inaomba kuidhinishiwa shilingi 39,145,399,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 9,361,277,000. Jumla kwa hili Fungu la 66 Tume ya Taifa ya Mipango, tunaomba kuidhinishiwa shilingi 48,506,646,000;

Fungu Na.7, Ofisi ya Msajili Hazina. Matumizi ya kawaida tunaomba kuidhinishiwa shilingi 60,585,131,000, matumizi ya miradi ya maendeleo tunaomba kuidhinishiwa shilingi 1,670,691,000. Jumla kwa Fungu namba 07 Ofisi ya Msajili Hazina, tunaomba kuidhinishiwa shilingi 62,255,822,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jumla kuu matumizi ya kawaida kama nilivyosema ni shilingi 122,122,685,000 na matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 26,507,276,000. Jumla inakuwa shilingi 148,669,961,000.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 tumeyaonesha kwa kina katika ukurasa wa 57 – 63 katika kitabu ambacho tumewasilisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hitimisho; hakuna shaka kwamba Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji imetekeleza kwa ufanisi mkubwa mpango na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu

kwa Mwaka 2024/2025. Mafanikio yaliyopatikana katika mpango wa bajeti hii ni pamoja na kuratibu kwa ufanisi maandalizi ya Dira ya Taifa ya maendeleo, kuongezeka kwa idadi ya miradi ya uwekezaji na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu iingie madarakani Serikali ya Awamu ya Sita iliweka suala la kusimamia ukuzaji uchumi kama kipaumbele mama. Katika kutekeleza hili, Serikali ya Awamu ya Sita iliweka mkazo katika kukuza uwekezaji katika sekta za uzalishaji na sekta ambazo zinatoa ajira kwa wingi. Serikali ilifanya hivi kwa kuzingatia kuwa, uwekezaji ndio msingi wa kukuza uchumi na ajira katika nchi yoyote. Kwa kutambua kuwa uwekezaji ni nyenzo muhimu katika kuingiza mtaji na teknolojia mpya kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Bi. Rosalynn Carter aliyeishi mwaka 1927 - 2023 alikuwa ni Mwanaharakati pia Mke wa Rais wa zamani wa Marekani Jimmy Carter, alikuwa anatafsiri na falsafa yake kuhusu maana ya kiongozi. Alisema ninaomba ninukuu:

*A leader takes people where they want to go. A great leader takes people where they don't necessarily want to go, but ought to be* (Kiongozi huwapeleka watu pale wanapotaka kwenda, hata hivyo Kiongozi Mashuhuri huwapeleka watu pale ambapo siyo lazima wawe wanataka kwenda lakini wanapaswa kwenda). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna shaka kwamba, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kiongozi anayetupeleka pale tunapopaswa kwenda kama nchi. Katika kuendeleza sekta ya uwekezaji Rais wetu ameweza kuhimili vikwazo bila kukata tamaa, bali amesimama imara na kusimamia misingi na malengo tuliyojiwekea kama nchi kwa sababu anajua kwa dhati tunapaswa kwenda wapi. Kutokana na maono ya uongozi wake thabiti nchi yetu kwa sasa ni miongoni mwa nchi 10 katika Bara la Afrika, zinazovutia uwekezaji kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo wa uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na usimamizi thabiti wa Chama Cha Mapinduzi chini ya Dkt. Balozi Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa CCM ni kwa sababu hii. Sifa hizi ambazo tumezieleza Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM nami nikiwemo hapo tarehe 18 – 19 Januari, 2025 walikuwa wepesi wa kupitisha kwa furaha kubwa jina la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea wake mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo vyama imara duniani hufanya, huandaa maandalizi mapema, vinapata wagombea wake mapema, vinaweka wananchi wanawajua na hizo ndiyo huwa dalili za ushindi wa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge walionitangulia na Watanzania walio wengi kuwapongeza sana kwa uteuzi wao huo. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya urais Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi. Hakika kazi ni utu, tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yetu. Hao ni pamoja na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Hayupo hapa leo, yupo Nchini Marekani kuhudhuria mkutano muhimu sana pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza na ninamshukuru pia Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dkt. Fred Matola Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango na yeye hayupo hapa leo kwa sababu wanahudhuria mkutano huo muhimu sana Nchini Marekani

pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Ndugu Nehemia Kyando Mchechu, Msajili wa Hazina na Ndugu Gilead Teri Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Nchini na ndugu yangu Charles Jackson Itembe, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawashukuru Menejimenti na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na wale wa taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwashukuru wadau wote waliochangia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu. Hawa ni pamoja na taasisi mbalimbali za sekta binafsi na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee kabisa, nichukue nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Ubungo Mkoani Dar es Salaam, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote tangu niwe Mbunge wa Jimbo la Ubungo. Aidha, ninakishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa imani kubwa kilichonipatia ya kupeperusha bendera ya chama kwa Mwaka 2020 kwa kuzingatia rekodi ya utendaji na matokeo yake katika Jimbo la Ubungo, ushirikiano ambao tumekuwa nao na kama ambavyo nimeshatangaza wazi kabla; muda ukifika *insha Allah* kwa furaha kubwa nitaomba tena ridhaa ya CCM, ili nipeperushe bendera ya chama na kuomba kura za ndiyo kwa wananchi wa Jimbo la Ubungo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha, ili kutekeleza vipaumbele vya Ofisi ya Taifa ya Uwekezaji ambavyo nimevieleza kwa mwaka 2026/2026, ninaliomba tena Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na likubali kuidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 148,629,961,000 kwa mchanganuo ambao nimeshaueleza awali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hii hotuba na Kitabu cha Hotuba ya Mpango wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji tuliyowasilisha, vyote viingie katika Kumbukumbu za Bunge. Aidha,

hii hotuba na kitabu chake vinapatikana pia katika Tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji planingivestment.go.tz.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (Makofi)

**HOTUBA YA WIZARA YA MIPANGO NA UWEKEZAJI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Sura ya Kwanza**

**UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2024/25 na kuidhinisha Mpango na Bajeti ya mafungu matatu (3) ya kibajeti ambayo ni Fungu 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Fungu 066 - Tume ya Taifa ya Mipango; na Fungu 007 - Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa Mwaka 2025/26.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika Mkutano wa 19 wa Bunge (Bunge la Bajeti) kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/25 pamoja na mapendekezo ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2025/26.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati kabisa, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini mimi pamoja na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika kutekeleza majukumu ya Ofisi husussan usimamizi wa Mipango ya

Taifa na Uwekezaji wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Tunapenda kumhakikishia kuwa, tutaendelea kusimamia kikamilifu jitihada zake katika kuimarisha uchumi kupitia Mipango thabiti na Uwekezaji wenye tija. Tunashukuru pia kwa maono na mwongozo wake katika maendeleo ya Taifa letu na jitihada zake binafsi katika kuimarisha diplomasia ya uchumi iliyochochea kuimarika kwa ushirikiano baina ya nchi yetu na nchi mbalimbali, kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini, na kuitangaza nchi yetu kuwa kivutio na mahala salama katika uwekezaji. Tunamwombea afya njema, ili watanzania waendelee kunufaika kupitia hekima na busara zake katika maridhiano, ustahimilivu, kubadilisha fikra, mifumo na mwelekeo wa Taifa letu kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya watanzania.

**4.** ***Mheshimiwa Spika***, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata tuzo maalum ya Kimataifa ya *Global Goalkeeper Award* kutoka Taasisi ya *Gates Foundation* kwa kutambua jitihada zake katika sekta ya afya na mafanikio ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupunguza vifo vya kina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano. Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji ikiwa ni msimamizi wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo tunatambua tuzo hiyo ina mchango katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDGs).

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninapenda pia kumshukuru Mheshimiwa *Dkt.* Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais na miongozo yake yenye kutia chachu na hamasa katika maendeleo ya Taifa.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na jitihada zake kubwa katika kuendelea kuijenga Zanzibar yenye maendeleo makubwa.

**7. *Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya kuendesha nchi yetu vema.

**8. *Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kutoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa msiba uliolipata Bunge kufuatia kifo cha Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kanda ya Afrika kilichotokea tarehe 27 Novemba, 2024 alipokuwa akipatiwa matibabu nchini India. Hayati Dkt. Ndungulile atakumbukwa kwa mchango wake muhimu katika kuboresha Sekta ya afya nchini na Bara la Afrika kwa ujumla. Tunawaombea marehemu wote pumziko la amani. Vilevile, kwa napenda kutuma salamu za pole pia ziwaendee kwa wote walikumbwa na misiba ya kuondokewa ndugu, jamaa na marafiki. watu wao wa karibu.

**Mwenyezi Mungu awalaze marehemu wote mahala pema peponi, Amina!**

**9. *Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kusimamia vema mhimili huu wa Bunge kwa umahiri mkubwa sana. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwa weledi wake katika kusimamia na kuongoza Bunge lako Tukufu.

**10. *Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi mahiri na imara wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Makamu wake Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge, Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili na kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/25 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka

2025/26. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa Hotuba hii ninayoiwasilisha leo.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yetu na kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii. Hawa ni pamoja na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb,) Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dkt. Tausi Mbaga Kida (Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji), Dkt. Fred Matola Msemwa (Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango), Ndugu Nehemiah Kyando Mchechu (Msajili wa Hazina), Ndugu Gilead John Teri (Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania) na Ndugu Charles Jackson Itembe (Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje). Aidha, ninawashukuru Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

***12.*** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kunipa ushirikiano na imani wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yangu ambayo yananilazimu muda mwingi kuwa nje ya nyumbani isingekuwa rahisi bila maombi na dua kutoka kwa familia yangu. Kipekee kabisa ninapenda kumshukuru Mke wangu kipenzi Bi. Prosista Prosper Laswai na watoto wangu Aggrey, Kelvin na Abigael kwa upendo, uvumilivu na utayari wenu unaonipatia ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na weledi wangu wote.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na utangulizi nilioutoa hapo juu, Hotuba yangu ina sehemu kuu nne: Maelezo mafupi kuhusu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Mafanikio ya Serikali ya awamu ya sita 2021 – 2025; Taarifa ya Utekelezaji wa kazi

zilizofanyika kwa Mwaka 2024/25; na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26.

**Sura ya Pili**

## 2. MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa Hati Na. 407 ya Mgawanyo wa Majukumu ya Serikali, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ina jukumu la kutunga, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera katika masuala ya Mipango, Uwekezaji na Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ina majukumu mahsusi yafuatayo:

(i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera kuhusu Mipango na Uwekezaji nchini;

(ii) Kuratibu na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi;

(iii) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;

(iv) Kuratibu Taasisi za kitaifa na kimataifa zinazohusika na uwekezaji; na

(v) Kusimamia Taasisi zilizo chini ya Ofisi ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA).

## 3. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2024/25

### 3.1. MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI HADI MACHI 2025.

#### 3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji iliidhinishiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi trilioni 1.113** kupitia Fungu 007 - Ofisi ya Msajili wa Hazina**.** Maduhuli hayo yanatokana na gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi zinazochangia, mapato yanayotokana na uendeshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS), rejesho la riba na mikopo, ziada na malipo mengineyo.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2025**,** jumla ya **Shilingi bilioni 664.53** zilikusanywa sawa na **asilimia 86** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 768.58** kwa kipindi kinachorejewa na **asilimia 60** ya lengo la mwaka. Sehemu kubwa ya makusanyo itapatikana katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2024/25.

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio haya yamechangiwa na uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA kwa kuunganisha mfumo wa Mpango na Bajeti (PlanRep) na mifumo ya ERMS na e-Watumishi pamoja na kufanya maboresho ya mfumo wa MUSE ambao umewezesha kupata taarifa halisi za matumizi katika Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za Umma. Aidha, kupitia uunganishaji wa mifumo imerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali ikiwemo mapato na matumizi ya Taasisi na Mashirika ya Umma.

### 3.1.2 Bajeti iliyoidhinishwa

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Mafungu matatu (3) ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji yaliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 121.33** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi bilioni 100.25** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 21.08** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **Shilingi bilioni 82.36** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 17.89** kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara. Aidha, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo yanajumuisha **Shilingi bilioni 15.59** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 5.49** fedha za nje.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, baada ya mapitio ya bajeti ya nusu mwaka, bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliongezeka kwa njia ya uhamisho kati ya mafungu na kufikia **Shilingi bilioni 275.03.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 253.74** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 21.29** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

### 3.1.3 Matumizi

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025, mafungu matatu (3) ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji yamepokea na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 171.47** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 62.35** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichopokelewa, **Shilingi bilioni 10.47** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 155.83** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 5.17** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, matumizi hlisi yalifikia Shilingi **bilioni 169.68** sawa na **asilimia 98.96** ya kiasi kilichopokelewa.

### 3.2. MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2021-2025

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita (2021 – 2025), mafanikio mbalimbali yamepatikana katika maeneo ya mipango ya Taifa ya Maendeleo, uwekezaji wa umma na sekta binafsi na maboresho ya mazingira.

### 3.2.1 Mipango ya Taifa ya Maendeleo

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya mageuzi makubwa katika kuimarisha mipango ya Taifa. Itakumbukwa kuwa tarehe 22 Aprili, 2021 Mheshimiwa Rais alipolihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya kwanza, pamoja na masuala mengine, aliweka wazi dhamira yake ya kusimamia na kuimarisha ukuaji wa uchumi nchini. Ili kufikia azma

hiyo Mheshimiwa Rais ameanzisha Tume ya Taifa ya Mipango inayosimamia na kuratibu masuala ya mipango na Uchumi ya nchi. Tume hiyo, ambayo Mwenyekiti wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeonesha mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka miwili tangu kuanzishwa kwake ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

(i) **Kukamilisha Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050**

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2024/25 Ofisi imeendelea kuratibu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 ambapo Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ilizinduliwa tarehe 11 Desemba, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Maandalizi ya rasimu hiyo yalihusisha hatua jumuishi za ushirikishwaji wa wadau na wananchi, ambapo jumla ya washiriki 1,172,106 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walifikiwa kupitia mikutano, warsha, na majukwaa ya majadiliano. Aidha, uchambuzi wa maoni ya wadau na wananchi, pamoja na maandalizi ya moduli ya uchumi jumla na taarifa ya idadi ya watu (demographic dividend), vimewezesha kubainisha viashiria vya uchumi na maeneo ya kipaumbele yaliyopendekezwa kuzingatiwa katika Dira 2050. Baada ya uzinduzi wa Rasimu ya Dira ya Taifa, Tume iliendelea na mchakato wa kuhakiki rasimu hiyo ambapo jumla ya wadau 1,268 wameshiriki kwenye vikao vya uhakiki. Kukamilika kwa Dira 2050 kutawezesha Taifa kuwa na maendeleo endelevu kupitia kubainisha mwelekeo wa nchi kimkakati kwa kipindi cha muda mfupi; wa kati na muda mrefu; malengo; na mikakati ya utekelezaji. **Aidha, nipende kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imeandaliwa na Watanzania na kwa kutumia fedha zetu za ndani kwa asilimia 100**.

**(ii) Uandaaji wa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu**

**26.** ***Mheshimwa Spika,*** Ofisi imeendelea na uratibu wa zoezi la uandaaji wa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (LTPP) ambao ni Mkakati wa Utekelezaji wa Dira 2050 utakaotumika kama mwongozo wa maandalizi wa Mpango wa Muda wa Kati

na Muda mfupi. Zoezi la uandaaji wa Mpango lilianza Januari 2025 baada ya kukamilika kwa rasimu ya Dira. Aidha, matarajio ni kuwa Mpango Elekezi wa muda mrefu pamoja na Dira zitawasilishwa Serikalini kwa ajili ya udhinishwaji na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo Juni, 2025.

### 3.2.2 Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

**27.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI) unaolenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuondoa changamoto mbalimbali katika taratibu za uwekezaji na ufanyaji biashara. Katika kipindi cha utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mheshimiwa. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maboresho makubwa ya ya Kisera, Kisheria na Kikanuni yamefanyika yaliyochagia kuimarisha mazingira ya Uwekezaji na Biashara. Utekelezaji huo ulijumuisha kurekebisha sheria za kuwezesha uanzishwaji na uendeshaji wa uwekezaji na biashara; kufuta au kupunguza tozo ambazo zilionekana kuwa ni changamoto kwa biashara; kuunganisha taasisi zilizokuwa zinatekeleza majukumu yanayofanana; na kuweka mifumo ya kieletroniki ya utoaji huduma kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwazi kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya mafanikio katika uimarishaji wa mazingira ya biashara ni pamoja na:

a) Serikali imepitia na kurekebisha sheria na kanuni 66 zilizoibuliwa wakati wa kufanya tathmini ya MKUMBI hususan katika sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara, kilimo, ufugaji, afya na maliasili na utalii. Marekebisho ya sheria hizi yamesaidia kupunguza ushuru na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji, kukuza biashara na uchumi kwa ujumla;

b) Serikali imefuta au kupunguza tozo, ada na faini mbalimbali zipatazo 383 zilizobainishwa kuwa kero katika ufanyaji biashara. Kwa mfano, Mamlaka ya Maabara ya

Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ilifuta ada 14 na kupunguza kiasi cha ada 9, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) ilifuta ada 16, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilifuta ada 12, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilifuta ada 6, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ilifuta ada 11 na kupunguza kiasi cha ada 4, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FFR) lilipunguza ada 8. Pamoja na maboresho haya, Serikali imeendelea kufanyia kazi tozo mpya zilizoibuka baada ya zoezi la tathmini kukamilika;

c) Serikali imeondoa au kuunganisha majukumu ya mamlaka za udhibiti ambayo yanafanana. Mathalani majukumu ya kutoa vibali vya kusafirisha kemikali vilivyokuwa vinatolewa na taasisi za Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Wakala ya Barabara Tanzania (TANROAD) na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) hivi sasa vinatolewa na GCLA pekee; mwingiliano kati ya Taasisi ya Udhibiti na Viatilifu katika Ukanda wa Kitropiki (TPRI) na Idara ya Mimea umeondolewa; muingiliano wa mamlaka kati ya TBS na Bodi ya Nyama kuhusu usajili, uuzaji na uhifadhi wa nyama ulitatuliwa kati ya mamlaka hizo mbili; majukumu ya kupanga viwango vya kitaifa vya ubora wa mafuta hivi sasa yanafanywa na Shirika la Viwango Tanzasnia (TBS) pekee badala ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na TBS kwa pamoja.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio mengine ya utekelezaji wa Mpango huu ni pamoja na:

(a) Kuimarishwa kwa mifumo ya kietroniki ili kuboresha utoaji wa huduma. Mfano, mfumo wa kuwezesha Mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa (*Government Enterprise Service Bus - GovESB)* umeimarishwa ambapo mifumo 179 ya Taasisi za Umma 202 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidigitali. Aidha, Serikali imeandaa Kanzidata ya kodi,

ushuru, leseni na vibali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mfumo wa TAUSI ambapo moduli ya vibali na leseni katika mfumo huo zinazoweka wazi sheria ndogo, ada, na tozo kufanya urahisi kwa wawekezaji na wafanyabiashara. Ujenzi wa mifumo hii imeongeza ufanisi wa utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi na kuokoa muda kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati;

(b) Kuanzishwa kwa Idara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote 184 na kuanzisha Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Sekretarieti za mikoa 26. Hatua hii imechochea kasi ya uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, kuhudumia sekta binafsi na kutatua changamoto zao;

(c) Kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji *(Tanzania Electronic Investment Window - TeIW*) kwa awamu ya kwanza ambao ulizinduliwa mwezi Septemba, 2024 na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika awamu hii mfumo umeunganisha huduma 7 kutoka taasisi 6 ambapo wawekezaji wanaweza kuomba na kupatiwa Cheti cha Uwekezaji, vibali vya kazi na ukaazi, Cheti cha Mlipa Kodi (TIN), Vivutio vya Kikodi, Kitambulisho cha Taifa (NIDA), na usajili wa makampuni. Katika awamu ya pili, inatarajiwa Wizara, Taasisi na Wakala nyingine zote 8 zilizobaki chini ya Kituo cha Huduma za Mahala pamoja zitaunganishwa ambazo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Kilimo; TBS; Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), Baraza la Taifa na Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), TMDA, TANESCO, na Tume ya Madini.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na taasisi za Sekta Binafsi za TPSF, CTI, na TCCIA ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

(MKUMBI) kwa lengo la kupata hali halisi ya utekelezaji wa MKUMBI. Tathmini hiyo ilikamilika na kuandaliwa kwa taarifa ambayo ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Septemba, 2024.

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, tathmini hiyo ilionesha matokeo chanya mbalimbali yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Mpango huo yakiwemo:

(i) Muda wa kushughulikia maombi ya vibali umepunguzwa kwa kiasi kikubwa, kutoka wastani wa siku 14 hadi siku 3 tu kwa vibali vingi;

(ii) Muda wa usajili wa hospitali binafsi umepungua kutoka miezi 12 hadi miezi 3;

(iii) Muda wa usafiri kwa malori ya mizigo kutoka Dar es Salaam hadi mpakani mwa Zambia (Tunduma) na mpakani mwa Rwanda (Rusumo), umepungua kutoka siku 4 na 7 hadi siku 2 na 3, mtawalia;

(iv) Muda wa kupata Cheti cha Usajili wa sehemu za kazi (Registration Certificate) umepungua kutoka siku 14 hadi siku 1;

(v) Muda wa kutoa Leseni ya Kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (Compliance License) kutoka siku 28 hadi siku 3;

(vi) Muda wa kushughulikia maombi ya Vibali vya Kazi kutoka siku zaidi 14 zilizoko kisheria hadi wastani wa siku 3 hadi siku 7;

(vii) Kupungua kwa michakato ya ushughulikiaji wa maombi (business processes) mfano taasisi ya OSHA, hatua zimepungua kutoka hatua 33 hadi 7;

(viii) Kupungua au kutokuwa na foleni kabisa katika ofisi nyingi za mamlaka za udhibiti zikiwepo BRELA, GCLA, TCRA na TMDA kutokana na matumizi ya mifumo ya kielekroniki;

(ix) Kwa ujumla sasa mwekezaji Tanzania anaweza kusajili kampuni chini ya masaa 8; kupata leseni ya biashara chini ya saa 1;

(x) Malipo ya huduma yanaweza kufanyika ukiwa popote bila kuonana na mtu; na

(xi) Vigezo vya ukaguzi vimekuwa wazi.


**32.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio niliyoyataja hapo juu, na tathmini hiyo imeonesha umuhimu wa kuandaa Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI II) kwa kuzingatia: maono ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; mahitaji ya sasa ya uwekezaji na ufanyaji biashara; mabadiliko ya teknolojia na kiuchumi; kuendeleza sekta binafsi ambayo ni msingi wa mageuzi ya kiuchumi; kujumuisha sekta nyingi zaidi zikiwemo elimu, miundombinu, na kampuni changa bunifu (startups); pamoja na kutatua changamoto zilizojitokeza ambazo hazikujumuishwa katika mpango unaotekelezwa sasa.

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza hilo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi maandalizi Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II) tarehe 3 Aprili, 2025 jijini Dar es Salaam. Nitumie fursa hii kutoa rai na kuwahimiza wadau wote wa biashara na uwekezaji nchini kushirikiana na Timu ya Kitaifa ya Wataalam ya uandaaji wa mpango huo kwa kutoa maoni yatakayobainisha changamoto na mikakati ya utatuzi wake. Zoezi la uandaaji MKUMBI II kukamilika na kuanza kutekelezwa kwa Mpango huo ifikapo mwezi Desemba, 2025.

### 3.2.3 Mwenendo wa Uwekezaji wa Sekta Binafsi

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2021 - 2024, jumla ya miradi 2,175 imesajiliwa inayotarajiwa kuzalisha ajira 650,674 na kuwekeza jumla ya mtaji wa **dola za Marekani milioni** 25,530.14 (**Kiambatisho Na 3**). Sekta tano (5) zinazoongoza ni viwanda ikiwa na miradi 983, sawa na asilimia 45.20; usafiri na usafirishaji, miradi 373 sawa na asilimia 17.15; majengo ya biashara, miradi 216 sawa na asilimia 9.93; utalii, miradi 203 sawa na asilimia 9.33; na kilimo, miradi 197 sawa na asilimia 9.06 (**Umbo Na 1**).

**Umbo 1: Asilimia ya Miradi Kisekta Iliyosajiliwa (2021-2024)**





***Chanzo: TIC (2024)***

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, tathmini inaonesha kuwa idadi ya miradi na kiwango cha mtaji na ajira zitokanazo na miradi ya uwekezaji nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.


Mathalani, idadi ya miradi iliongezeka kutoka miradi 256 mwaka 2021 hadi miradi 901 mwaka 2024. Kiwango cha mitaji kilipanda kutoka **dola za Marekani milioni** 3,749 mwaka 2021 hadi **dola za Marekani milioni** 9,313 mwaka 2024. Aidha, idadi ya ajira iliongezeka kutoka 53,025 mwaka 2021 hadi 212,293 mwaka 2024 **(Umbo Na. 2 hadi 4).**

**Umbo 2: Miradi Iliyosajiliwa kati ya Mwaka 2021 na 2024**





***Chanzo: TIC 2024***

**Umbo 3:** Mitaji Iliyovutiwa Kutoka Nje (FDI) Kutokana na Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa na TIC kati ya Mwaka 2021 na 2024*l*




***Chanzo: TIC 2024***

**Umbo 4:** Idadi ya Ajira Zilizotarajiwa Kupatikana Kutokana na Miradi ya Uwekezaji kati ya Mwaka 2021 - 2024




***Chanzo: TIC 2024***

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, Awamu ya Sita imekuwa na mafanikio makubwa kuvutia uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) ambapo jumla ya miradi 45 imesajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini kupitia leseni za EPZ na SEZ. Miradi hiyo imeleta mitaji ya jumla ya **dola za Marekani milioni** 1,171.97, na kuongeza ukuaji wa mauzo ya nje yenye thamani ya **dola za Marekani milioni** 397.64 na ajira zipatazo 20,674. Aidha, miradi hiyo imejikita katika sekta zinazozalisha bidhaa zitokanazo na kilimo, bidhaa za viwandani, bidhaa za mifugo, bidhaa za kemikali, bidhaa za madini na bidhaa za mazao ya misitu.

### 3.2.4 Uwekezaji wa Miradi Mikubwa ya Kimkakati

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara zimefanikisha nchi kuvutia

miradi mikubwa na ya kimkakati yenye manufaa ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Miradi hiyo inajumuisha ile inayotekelezwa na sekta binafsi ya Watanzania na wawekezaji kutoka nje ya nchi pamoja na ile ya taasisiza sekta ya umma. Aidha, miradi hii imejumuisha sekta zote za kiuchumi ikiwemo viwanda, kilimo, uchukuzi, ujenzi, mifugo na uvuvi, utalii, afya na madini. Vilevile, miradi hii inapatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mgawanyo wa uwekezaji huo kisekta ni kama ifuatavyo:-

**a. Sekta ya Viwanda**

Miongoni mwa miradi mikubwa kwa upande wa sekta ya uzalishaji viwandani ni pamoja na ifuatayo:

(i) Mradi wa kuzalisha ndege wa kampuni ya AIRPLANES AFRICA LIMITED; uliopo Morogoro uliowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni 3.02** na umeajiri watu 150. Hiki ni kiwanda cha kwanza cha aina yake kwa teknolojia inayotumika;

(ii) Mradi wa kuzalisha vioo vya ujenzi wa kampuni ya KEDA (T) Ceramics Co. Ltd. uliopo Mkuranga, Pwani uliowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni 620** na umeajiri watu 43,000. Mradi huu unazalisha vioo tani 1,100 kwa siku na asilimia 80 huuzwa nje na hivyo kuchangia upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi;

(iii) Mradi wa kuzalisha mabati wa kampuni ya Lodhia Industries uliopo wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milion 52 i na umeajiri watu 2,200. Mradi huu unazalisha jumla ya tani milioni 1.2 kwa mwaka ukilinganmisha na mahitaji ya ndani ambayo ni takribani tani 600,000 kwa mwaka na hivyo kuchangia mauzo nje ya nchi;

(iv) Mradi wa kuzalisha mabati wa kampuni ya Kinglion Steel Mill uliopo Kibaha, Pwani uliowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni 42** kati ya **dola za Marekani milioni 62** na umeajiri watu 2,000. Mradi huu unawezesha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vingine vya mabati na upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na mauzo nje ya nchi;

(v) Mradi wa kongani ya viwanda wa kampuni ya Sino-Tan Industrial Park uliopo Kwala, Pwani, utakaowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni 327** na kutoa ajira za watu 100,000 kutokana na viwanda vikubwa na vya kati 200 na viwanda vidogo 300 vitakavyowekezwa. Hadi sasa mradi umewekeza **dola za Marekani milioni 36** na umetoa ajira 651. Mradi huu wenye eneo la ukubwa wa ekari 2,500 na utakuwa na viwanda vinavyohusiana na usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa vifaa, viwanda vya dawa, vifaa vya ujenzi, usindikaji wa viatu na nguo, na viwanda vya kemikali. Hadi sasa kongani hii ina viwanda 3 ambavyo vinazalisha, viwanda 3 vinakamilisha kufunga mitambo na viwanda 4 vinatarajiwa kuanza ufungaji wa mitambo ifikapo mwisho wa mwezi Aprili 2025;

(vi) Mradi wa kuzalisha saruji wa kampuni ya Maweni Limestone Limited uliopo Kata ya Maweni Halmashauri ya Jiji la Tanga, uliowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni 170**, Aidha, kiasi cha zaidi ya **dola za Marekani milioni 30** zimewekezwa kwa kwa ajili ya upanuzi wa awamu ya pili katika uzalishaji wa saruji na mradi huu umeajiri jumla ya watu 904 ambapo wazawa ni 424, wageni ni 82 na wenye mikataba kutoka kwa mzabuni ni 400. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha bidhaa za Clinker Tani Milioni 1.24 kwa Mwaka pamoja na Saruji Tani Milioni 1.5 kwa Mwaka;

(vii) Maweni Limestone Limited kinamilikiwa na raia kutoka nchi ya China na pia kinajulikana kwa jina la Huaxin Cement Co. Ltd

(viii) Mradi wa kuzalisha vinywaji vya vileo wa kampuni ya Mati Super Brands Ltd. uliopo Manyara uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 2.64 unailikiwa na Mtanzania kwa asilimia 100 na umeajiri watu 269;

(ix) Mradi wa uzalishaji wa vifaa vya ujenzi wa kampuni ya Ziwa Steel and Wire Products limited uliopo jijini Mwanza uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 3.4 na umeajiri watu 508. Kupitia mradi huu wakazi wa Mwanza na mikoa ya jirani sasa wamehakikishiwa upatikanaji wa vifaa vya ujenzi kwa bei nafuu na hivyo kupelekea ujenzi wa nyumba bora na kuboresha hali ya maisha.

(x) Mradi wa uzalishaji wa vinywaji baridi wa kampuni ya A-One Products and Bottlers Limited uliopo jijini Mbeya uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 30 na umeajiri watu 150. Mradi huu umewezesha utunzaji wa mazingira pamoja na utengenezaji wa chupa ambazo hutumika kama malighafi katika viwanda vingine vya vinywaji baridi; na

(xi) Mradi wa kuzalisha vinywaji baria wa kampuni ya Dew Drop Drinks Co. Ltd. uliopo mkoani Rukwa uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 20 na umeajiri watu 150.

**b. Kilimo na Uongezaji Thamani**

(i) Mradi wa kilimo cha parachichi, ufungashaji na uchakataji wa mafuta ya parachichi wa kampuni ya AvoAfrica TZ Limited uliopo mkoani Njombe

uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 4.8 na umeajiri watu 650. Mradi huu umehakikisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima wa parachichi waliopo karibu na eneo la mradi, upatikanaji wa bidhaa ya mafuta na upatikanai wa fedha za kigeni kutokana na mauzo ya parachichi na mafuta nje ya nchi;

(ii) Mradi wa upanuzi wa kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari wa kampuni ya Kagera sugar Limited uliopo mkoani Kagera uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 220 na umeajiri watu 10,094. Mradi huu umeendelea kuchangia upatikanaji wa sukari nchini na kupunguza uagizaji kutoka nje ya nchi;

(iii) Mradi wa kilimo cha alizeti na uchakataji wa mafuta ya kula wa kampuni ya Mainland Group Agroprocess Co. Ltd. uliopo Dodoma uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 28 na umeajiri watu 130. Mradi huu unahakikisha upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima wa zao la alizeti ambayo inatumika kama mali ghafi kiwandani;

(iv) Mradi wa kuzalisha mafuta ya kula wa kampuni ya Wild Flower Grains and Oil Mills uliopo Singida uliowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni** 240 na umeajiri watu 400. Aidha, mradi huu unamilikiwa na Mtanzania kwa asilimia 100 unaokoa fedha za kigeni kwa kupunguza pengo la mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya nchi;

(v) Mradi wa kuzalisha mbolea wa kampuni ya Itracom Fertilizers Limited uliopo jijini Dodoma uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 180 na umeajiri watu 3,000. Mradi huu una uwezo wa kuzalisha mbolea tani 700,000 kwa mwaka na hivyo unachinga katika kukuza kilimo na

upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kuuza mbolea nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa mbolea; na

(vi) Mradi wa kuchakata mpunga wa kampuni ya Wilmar Rice Tanzania ltd uliopo mjini Morogoro uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 71 na umeajiri watu 498. Mradi huu umeleta teknolojia ya kisasa ya kuchakata mpunga na kuzalisha bidhaa mbalimbali za mchele na pumba za mpunga. Vilevile, mradi umewezesha upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima wa zao la mpunga pamoja na upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na uuzaji wa mchele nje ya nchi.

**c. Mifugo na Uvuvi na Uongezaji Thamani**

(i) Mradi wa uzalishaji wa samaki kwa kutumia vizimba wa kampuni ya the Big Best Company Limited uliopo jijini Mwanza uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 12.3 na umeajiri watu 133. Mradi huu unatarajia kuzalisha tani 900 hadi 1200 za samaki aina ya sato kila mwezi ifikapo mwaka 2026. Aidha, mradi huo utahamasisha uhamishaji wa teknolojia ya kisasa ya uzalishaji wa samaki kwa kutumia vizimba, kukuza uchumi wa mkoa wa Mwanza na taifa kwa ujumla;

(ii) Mradi wa kusindika maziwa wa kampuni ya Kahama Fresh Ltd. uliopo mkoani Kagera uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 1 na umeajiri watu 300; na

(iii) Mradi wa kuzalisha chakula cha mifugo wa kampuni ya Rofi Farming Company Limited uliopo jijini Mwanza uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 10.1 na umeajiri watu 60. Mradi huu umewezesha kukuza sekta nyingine za ufugaji kutokana na kuzalisha bidhaa ambayo ni

malighafi katika shughuli za ufugaji. Aidha uwepo wa mradi huu unachochea kubadilisha mfumo wa ufugaji kuwa wa kisasa na kibiashara.

**d. Afya**

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Miradi mikubwa ya sekta ya afya kwa upande wa sekta binafsi inahusisha ujenzi wa hospitali na uzalishaji wa vifaa tiba kama ifuatavyo:-

Mradi wa uzalishaji wa bomba za sindano wa kampuni ya Medical Dawlia Limited uliopo katika wilaya ya Kigamboni Mkoa wa Dar es salaam uliowekeza mtaji wa **dola za Marekani milioni** 3 na umeajiri watu 41. Mradi huu umewezesha upatikanaji wa vifaa tiba ambavyo hapo awali vilikuwa vinaagizwa nje ya nchi na hivyo kuokoa fedha za kigeni.

**e. Nishati**

Mradi wa uhifadhi wa mafuta wa kampuni ya Afroil International Transformers Tanzania (PVT) Ltd. uliopo sehemu ya Vijibweni wilaya ya Kigamboni mkoa wa Dar es salaam uliowekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 90 ambao unamiilikiwa na Mtanzania kwa asilimia 100 na umeajiri wafanyakazi 500. Kufanikiwa kwa mradi huu kunachochea ukuaji wa miradi mingine ya uwekezaji kama vile majengo ya biashara.

**3.2.4 Uwekezaji wa Umma**

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya awamu ya Sita imeendelea na maboresho ya kimuundo na kiutawala ambayo yamechangia ufanisi wa kiutendaji na ongezeko la mapato ya nchi. Sehemu ya Mapato yaliyoongezeka yametokana na kukusanya mapato yasiyo ya kodi kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma yanayojumuisha Gawio (dividends), Michango ya asilimia 15 ya Mapato ghafi na mapato mengineyo. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita mapato yasiyo ya kikodi (Non-Tax Revenue) yameongezeka kutoka shilingi **billioni**

**637.66** mwaka 2021 **hadi shilingi Trilioni 1.00839** mwaka 2023 ambalo ni ongezeko la asilimia 58.14.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, uwekezaji wa ndani wa Serikali kwenye mashirika, taasisi na wakala za Serikali umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka shilingi **trilioni 67.01** mwaka 2020/21 na kufikia shilingi **trilioni 85.4** mwaka 2023/24 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 27.4**. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, uwekezaji wa Serikali nje ya nchi ulifikia shilingi **bilioni 846.22** kutoka shilingi **bilioni 722.94** mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la **asilimia 17**.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika kipindi kinachoishia Februari 2024, Serikali imefanikiwa kuongeza umiliki wa hisa katika Kampuni ya Madini ya SOTA Mining kutoka asilimia 16 hadi asilimia 20, Umiliki wa kampuni ya Inflight Catering imeongezeka kutoka asilimia 10.99 hadi asilimia 31.69. Sambamba na hilo, serikali imesaini mikataba ya ubia iliyoiwezesha nchi kumiliki kwa kuanzia kiwango cha asilimia 16 ya hisa zisizohamishika kwa kampuni saba (7) ambazo ni: Faru Graphite Corporation; Kudu Graphite Corporation, Dumagraphite Company Limited, Mamba mineral Corporation Limited, Nyati Minerals Limited pamoja na Tembo Nickel Refining Limited. Mafanikio hayo ni uthibitisho wa adhma ya Serikali ya Awamu ya Sita, yaliyolenga kuyataka mashirika ya Umma kujiendesha kwa ufanisi na faida.

***42.*** ***Mheshimiwa Spika***, eneo lingine ni la uimarishwaji wa mashirika ya Umma ambapo zaidi ya shillingi Trillioni 5.5 zimeongezwa kama mtaji ili kuziwezesha taasisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Benki ya Biashara Tanzania (TCB) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kujiendesha kibiashara na kupata faida na kuchangia kwenye pato la Taifa. Aidha, shirika la TANESCO iliongezewa shillingi trillioni 2.419, ili kuwezesha ufanisi wa shirika hilo kwa kuboresha njia za usafirishaji wa umeme na miundombinu ya uzalishaji, shirika la TPDC liliongezewa shillingi trillioni 2.752 kuboresha tafiti za mafuta na gesi ili kufanikisha utafiti na uchimbaji na usambazaji wa mafuta na gesi, TADB shillingi bilioni 208 kukopesha wawekezaji walio katika kilimo, na Benki ya

TCB shillingi billioni 131. Kufuatiwa kuongezewa mtaji TCB kwa mara ya kwanza imefanikiwa kupata faida ya takribani Shillingi billioni 31.6 kwa mwaka 2024 kutoka kwenye kundi la Taasisi zilizokuwa zinapata hasara.

### 3.3. MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2024/25

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio ya miaka minne yaliyoelezwa katika sehemu iliyopita, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji imepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa mwaka 2024/25 kama ifuatavyo:-

(i) **Kuandaa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26**

***Mheshimwa Spika,*** Ofisi imeandaa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ambao ni wa tano (5) na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Mapendekezo ya mpango huo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 01 Novemba, 2024 na kupitishwa. Vilevile, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 yanaendelea na unatarajiwa kupitishwa na Bunge lako tukufu mwezi Juni, 2025. Mpango huu ni kiungo kati ya mipango iliyokamilika na mipango inayotarajiwa kutekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambapo mapendekezo yake yamejielekeza katika kuainisha na kutekeleza programu na miradi muhimu ambayo haijakamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo.

(ii) **Kufanya tathmini ya thamani ya uwekezaji na athari ya miradi ya kielelezo na kimkakati katika kuendeleza na kukuza uchumi**

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika miradi na programu za Serikali, Tume ilifanya uchambuzi wa miradi na programu zinazotekelezwa na

Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi thabiti na ufanisi katika programu za maendeleo. Kufuatia uchambuzi huo ilibainika kuwa jumla ya miradi 9,711 inatekelezwa na Serikali katika ngazi mbalimbali, matokeo ya uchambuzi huo ni msingi katika kuwezesha ufuatiliaji na tathmini za programu na miradi ya maendeleo. Aidha, Tume imeendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo (NPMIS) ili kuongeza ufanisi katika uchambuzi wa maandiko ya miradi na programu kupitia teknolojia ya kisasa na akili mnemba. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya maandiko 150 ya miradi na programu mbalimbali yamechambuliwa na kutolewa maoni kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaleta tija.

**(vii) Kuwezesha tafiti za kisayansi, tathmini ya hali ya rasilimali ya taifa na Sera mbalimbali kwa lengo la kuimarisha upangaji na utekelezaji kwa kuzingatia mipango ya maendeleo**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha tafiti za kisayansi, tathmini ya hali ya rasilimali za Taifa na Sera mbalimbali, Ofisi inaendelea kuratibu zoezi la tathmini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Tathmini hiyo inafanyiwa kazi na Mtathmini huru ambaye ni Taasisi ya Tafiti za Kiuchumi na Kijamii (ESRF) ambapo taarifa ya awali (inception report) imewasilishwa na kutolewa maoni. Lengo la tathmni hiyo ni kuutaarifu umma kuhusu kiwango cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) pamoja na kutumika katika maandalizi ya Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

**46.** ***Mheshimwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo unataarifiwa na tafiti mbalimbali Ofisi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango iliweza kufanya tathmini ya tafiti **365** kutoka Taasisi za ndani na nje ya nchi ambazo zimetumika kuibua maeneo ya vipaumbele vilivyotumika kutaarifu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu.

**(viii) Kukamilisha uandaaji wa Sera mpya ya Uwekezaji na Mkakati wa Utekelezaji**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha tunaenda sambamba na maendeleo na mabadiliko yanayotokea duniani katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, Ofisi imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na imeandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 2024 na Mkakati wake. Maandalizi ya Sera na Mkakati umezingatia mazingira ya sasa ya uwekezaji na biashara ikiwa ni pamoja na kujumuisha Mipango ya Maendeleo ya Taifa na Vipaumbele vya nchi. Aidha, Ofisi inakamilisha maboresho ya malengo na mikakati ya Sera hiyo kwa kuzingatia maono ya rasimu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

**(ix) Kukamilisha uunganishaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje (EPZA)**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25 Ofisi ilipanga kukamilisha uunganishaji wa Taasisi za Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje ambapo tarehe 13 Februari, 2025 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliazimia na kupitisha Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Na. 16 ya Mwaka 2024 kuwa Sheria. Sheria hiyo inaanzisha Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Tanzania (Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority – TISEZA) ambayo itatekeleza majukumu ya zilizokuwa TIC na EPZA. Pamoja na mambo mengine, Sheria hii mpya pia imeweka masharti ya uendelezaji wa uwekezaji na mazingira bora kwa wawekezaji Tanzania; kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu, ulinzi, uvutiaji, uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji nchini; na uendelezaji na usimamizi wa maeneo maalumu ya kiuchumi.

**(x) Kukamilisha Mwongozo wa Ujenzi na Uendeshaji wa Kongani za Viwanda nchini**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2024/25, Ofisi imefanya tathmini ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi na kuandaa Mwongozo wa Maendeleo na Usimamizi wa Kanda Maalum za Kiuchumi Tanzania ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Septemba 2024. Mwongozo huo unaweka utaratibu wa usimamizi na uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi nchini kupitia sekta binafsi na sekta yaumma. Mwongozo huo unajumuisha uendelezaji na usimamizi wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ), Kongani za Viwanda (Industrial Parks), Kongani za Utalii (Tourism Parks), Kongani za Kilimo (Agro -Industrial Zones), Kongani za Teknolojia (Technological Parks) na Maeneo huru ya biashara (Free Trade Zones).

**(xi) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mageuzi katika uendeshaji wa Mashirika ya Umma.**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha utekelezaji wa mageuzi ya uendeshaji wa masharika ya umma yanaleta ufanisi, Serikali imeendelea na utekelezaji wa maamuzi ya kuunganisha na kufuta Taasisi za Umma zilizo chini ya Wizara nyingine za Kisekta ili kuimarisha utendaji wa taasisi za Umma na kuongeza tija katika kuchangia maendeleo ya Taifa. utekelezaji wa maamuzi haya upo katika hatua mbalimbali, ambapo masuala ya msingi yamekamilika ikiwemo uandaaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na Rasimu za Muundo wa Taasisi mpya zitakazoundwa. Vilevile, Ofisi itaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa ufutaji na uunganishaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma kama ilivyoelekezwa na Serikali. Ufuatiliaji huo utajumuisha tathmini ya utekelezaji, kubaini changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuzishughulikia katika mamlaka zinazohusika.

**(xii) Kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa Sera na Miongozo ya Uwekezaji wa Sekta Binafsi**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuzijengea Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kutoa huduma zenye viwango bora kwa wafanyabiashara na wawekezaji, Ofisi imefanikiwa kununua vitendea kazi (meza 693 na viti 693) ambavyo vitakabidhiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya Idara mpya ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Hii ni hatua muhimu katika kujenga uwezo wa Idara hii mpya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha zinatoa huduma zinazoridhisha kwa sekta binafsi. Aidha, katika jitiahada za kuchochea ushiriki wa Sekta Binafsi katika mageuzi ya kiuchumi, Maandalizi ya uandaaji wa mwongozo wa mafunzo (Training Manual) katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa yamekamilika ambapo mafunzo yanatarajiwa kufanyika katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2024/25.

**(xiii) Kufanya mapitio ya Sheria zinazohusu masuala ya madini, ardhi, kilimo, utalii na biashara kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ilipanga kupitia sheria zinazohusu masuala ya madini, ardhi, kilimo, utalii na biashara kwa lengo la kuweka mazingira wezesha kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje. Hadi Machi, 2025 jumla ya sheria **12** zilizolenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuleta unafuu mkubwa kwa wawekezaji na sekta binafsi zimefanyiwa maboresho na kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 na Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscelleneous Amendments) za mwaka 2024. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Taifa ya Viwanda (Leseni na Usajili), Sura 124; Sheria ya Leseni za Biashara, Sura 101; Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura 283; Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Sura 427; Sheria ya Madini, Sura 123; Sheria ya Viwango

Sura 130; Sheria ya Ushindani Sura 13; Sheria ya Uhamiaji Sura 54; Sheria ya Uvuvi Sura 279; Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2024 inayohusisha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii Sura ya 123; Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263, na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Utumishi wa Umma Sura 371.

**(xiv) Kukamilisha Sheria ya Uwekezaji wa Umma na Kanuni zake**

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25 Ofisi ilipanga kukamilisha Sheria ya Uwekezaji wa Umma na Kanuni zake kwa lengo la kuhakikisha Mashirika ya Umma yanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali na kuchangia uchumi wa nchi. Hadi Machi, 2025 Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya maboresho ya Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma ya mwaka 2023 ambapo tarehe 21 Agosti, 2024 mapendekezo ya marekebisho ya Muswada yaliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza Bungeni mwezi Novemba, 2023. Aidha, kufuatia wasilisho hilo, Serikali inaendelea na majadiliano ya ndani kuhusu maboresho ya Muswada huo na baada ya kujiridhisha na maboresho hayo, Muswada huo utawasilishwa Bungeni kwa mara ya pili na tatu ili Bunge liweze kujadili na kuupitisha kuwa Sheria.

**(xv) Kuchochea ushindani wa uwekezaji na mazingira bora ya biashara ndani ya nchi**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mazingira wezeshi yanayochochea ushindani kwa wawekezaji na wafanyabiashara nchini, Ofisi iliratibu zoezi la utafiti wa urahisi wa ufanyaji biashara na uwekezaji kwa sasa unatambulika kama ***Business Ready.*** Katika taarifa ya ***Business Ready*** ya mwaka 2024 iliyohusisha nchi 50 duniani, Tanzania imewekwa katika kundi la Tatu (3rd Quantile) kati ya makundi matano kwa alama za wastani za utendaji katika tathmnini.

**55.** **Mheshimiwa Spika**, kati ya nchi zilizofanyiwa tathmini katika Bara la Afrika, utendaji wa Tanzania katika taarifa

ya *Business Ready* ya mwaka 2024; Katika Nguzo I - Tanzania imeshika nafasi ya 7; katika Nguzo II - Tanzania imeshika nafasi ya 4; na katika Nguzo III - Tanzania imeshika nafasi ya 7 kwa mchanganuo ufuatao;

a. **Mifumo ya Kisheria (Nguzo I):** Tanzania ilipata alama ya **65.00**, ikiifanya iwe katika kundi la tatu (3rd Quantile). Alama kubwa katika Nguzo I ni ya Hungary kwa kupata alama 78.23 wakati alama ndogo ni 46.21 ya Timor – Leste;

b. **Huduma za Umma (Nguzo II):** Tanzania ilipata alama ya **51.56,** ikiifanya iwe katika kundi la nne (4th Quantile). Alama kubwa katika Nguzo II ni ya Estonia kwa kupata alama 73.31 wakati alama ndogo ni 18.35 ya Jamhuri ya Afrika ya Kati;

c. **Ufanisi wa Uendeshaji Biashara (Nguzo III):** Tanzania ilifikia alama ya 62.15, ikiifanya iwe katika kundi la tatu (3rd Quantile). Alama kubwa katika Nguzo III ni ya Singapore kwa kupata alama 87.33 wakati alama ndogo ni 40.00 ya Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**(xvi) Ushindanishi katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu kuvutia wawekezaji na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji biashara**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) iliandaa vigezo vya kupima ubora wa mazingira ya biashara ili kukuza uwekezaji na uchumi nchini. Mazingira bora ya biashara hukuza uwekezaji na Uchumi kwa ujumla na huoneshwa kwa asilimia kubwa zaidi kuanzia asilimia 0 hadi 10. Kwa sasa Mkoa au Wilaya hupimwa kwa kuzingatia tathmini ya taarifa (data) zinazokusanywa kwa mujibu wa vigezo husika vya Baraza la Taifa la Biashara. Aidha, taarifa za ziada zinazotumika ni ukuaji wa uchumi na kodi katika eneo husika. Hivyo, kwa mwaka 2024 mikoa

iliyoongoza katika maeneo hayo ni Dodoma, Kilimanjaro na Dar es Salaam.

**(xvii) Uendelezaji wa miradi ya kitaifa ya Kielelezo ikiwemo Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ)**

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi inaendelea kuratibu uendelezaji wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo. Katika kipindi cha Mwaka 2024/25, Serikali imeendelea na uendelezaji wa Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Bagamoyo (BSEZ) kwa kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami (Asphalt Concrete) yenye urefu wa kilomita tatu (3) katika eneo lenye viwanda Zinga – Bagamoyo ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70. Aidha, Ofisi inaendelea kuandaa andiko la mradi 'Prospectus' litakalotumika kupata mtaji wa kuendeleza eneo hilo hususani ujenzi wa majengo ya viwanda (industrial sheds).

**58.** ***Mheshimwa Spika,*** kwa kutambua kuwa ukamilishaji wa miundombinu ya msingi utahitaji uwepo wa miundombinu ya juu kwa uzalishaji wa viwanda. Serikali imeendelea kushirikiana na wadau akiwemo FSD Africa kuandaa taratibu na kubuni bidhaa ya soko la mitaji kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya viwanda na maghala kwa kutumia bidhaa za uwekezaji wa pamoja wa majengo ya viwanda (Industrial REIT). Sambamba na FSD Afrika, wadau wengine tunaoshirikiana nao ni pamoja na ORBIT Securities, Watumishi Housing, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa Dar es salaam (DSE) na Benki ya CRDB.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mamlaka ya EPZA imeendelea na uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Nala Dodoma, Songea Ruvuma na Mara SEZ kwa kuandaa ramani ya Mipango Miji (Town Planning Map), Usanifu wa michoro ya majengo, *Topographical survey* pamoja na Mpango Kabambe na Upembuzi Yakinifu.

**(xviii) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo saba (7) ya viwanda vilivyokabidhiwa kwa Mamlaka ya EPZ**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo saba (7) ya viwanda vilivyokuwa vimebinafsishwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina na vilikabidhiwa kwa Mamlaka ya EPZ. Hadi Machi 2025, viwanda vitatu (3) vimeshapata wawekezaji ambavyo ni Nachingwea Cashew Nuts, Mafuta Ilulu na National Steel kwa njia ya zabuni. Aidha, kiwanda cha Nachingwea na kiwanda cha Mafuta Ilulu vilivyopo Mkoani Lindi vimepata wawekezaji kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo na kiwanda cha National Steel kilichopo Chang'ombe Dar es salaam kimepata mwekezaji kwa ajili ya kutengeneza samani, vinywaji baridi na kutoa huduma ya ugavi na biashara. Vilevile, viwanda vinne (4) ambavyo ni Mwanza Tanneries LTD, Tanganyika Packers Limited (TPL) - Mbeya, Tanganyika packers Limited (TPL) – Shinyanga na Mkata Samills LTD (Tanga) vilivyobaki Ofisi inaendelea kutafuta wawekezaji.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi imeshirikiana na Halmashauri ya Kahama pamoja na Barrick Gold kukamilisha utaratibu wa kulitangaza eneo la BUZWAGI kuwa Eneo Maalum la Kiuchumi ambapo kampuni tatu (3) zinazojihusisha na uchenjuaji wa madini zimewasilisha maombi ya kupewa leseni za kuchakata madini. Eneo hilo lina baadhi ya miundombinu ya msingi kama vile umeme, barabara, maji safi na maji taka.

**(xix) Usajili wa Miradi ya Uwekezaji kupitia TIC na EPZA**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ilifanya maboresho ya mifumo ya usajili kwa ajili ya kuhudumia wawekezaji wa ndani na nje. Hadi kufikia Machi 2025, TIC imesajili jumla ya **miradi mipya 691** yenye thamani ya **dola za Marekani milioni 7,997.06** ambayo inatarajiwa kuzalisha **ajira mpya 298,257.** Usajili wa miradi hiyo ni sawa na ongezeko la **asilimia 35.76** ya miradi iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2023/24 ambapo Kituo kilisajili jumla ya miradi **509** yenye thamani ya **dola za Marekani milioni5,825.00** na

kutarajiwa kuzalisha ajira mpya 130,202. Kati ya miradi hiyo iliyosajiliwa, miradi **222** sawa na **asilimia 32** inamilikiwa na Watanzania, miradi **156** sawa na **asilimia 23** ni ya Ubia na miradi **313** sawa na **asilimia 45** inamilikiwa na wageni.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi kupitia TIC ni uzalishaji viwandani miradi **305** sawa na **asilimia 44**; usafirishaji miradi **110** sawa na **asilimia 16;** kilimo miradi **74** sawa na **asilimia 11**; ujenzi wa majengo ya biashara miradi **72** sawa na **asilimia 10;** na utalii miradi **60** sawa na **asilimia 9**. Sekta nyingine za huduma, rasilimali watu, miundombinu ya kiuchumi, nishati, ujenzi, madini na mafuta, pamoja na mawasiliano ya simu zimesajili jumla ya miradi **70** sawa na takribani **asilimia 10** (**Kiambatisho Na. 1**).

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kufanyika katika Mikoa mbalimbali kama ifuatavyo: Dar es Salaam miradi **269**, Pwani miradi **133**, Arusha miradi **51**, Dodoma miradi **34**, Mwanza miradi **28**, Geita miradi **21**, Morogoro miradi **21**, Mbeya miradi **18**, Tanga miradi **13**, Kilimanjaro miradi **12**, Lindi miradi **11**, na Shinyanga miradi **11**. Miradi mingine **69** ipo katika mikoa mingine kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**. Uwekezaji huo umechangiwa na mazingira bora ya uwekezaji na biashara chini ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Sheria ya Uwekezaji Namba 10 ya 2022.

**65.** ***Mhehimiwa Spika***, vilevile, Kituo kimesajili jumla ya miradi **36** ya upanuzi na ukarabati yenye thamani ya **dola za Marekani milioni 1,257.97** na kutarajiwa kuzalisha ajira **7,139**. Takwimu hizo zinaonesha Sheria Mpya ya Uwekezaji, Na. 10 ya 2022, imeleta athari chanya katika Sekta ya Uwekezaji ambapo wawekezaji walitumia faida zao kuwekezatena. Vilevile, takwimu zinaonesha wawekezaji wa ndani walitumia fursa ya vivutio vinavyotolewa na Sheria mpya kufanya upanuzi na matengenezo ya miradi yao.

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, kiwango cha mtaji na ajira zitokanazo na miradi ya uwekezaji katika Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC) imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mathalani, idadi ya miradi iliongezeka kutoka miradi **256** mwaka 2021 hadi kufikia miradi **901** mwaka 2024. Kiwango cha mitaji inayotokana na miradi ya uwekezaji kilipanda kutoka **dola za Marekani milioni 3,749** mwaka 2021 hadi **dola za Marekani milioni 9,313** mwaka 2024. Aidha, idadi ya ajira itokanayo na miradi ya uwekezaji iliongezeka kutoka **53,025** mwaka 2021 hadi **212,293** mwaka 2024.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2025, Mamlaka ya EPZ imesajili na kutoa leseni mpya za uwekezaji kwenye Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje 29 zikiwemo leseni nane (8) za uendeshaji na leseni 21 za uendelezaji. Miradi hiyo 29 inatarajiwa kuwekeza **dola za Marekani milioni 430.62**, kuchangia mauzo ya nje kwa **dola za Marekani milioni 259.28** na kutoa ajira **27,085**. Usajili wa miradi hiyo ni sawa na ongezeko la **asilimia 21** ya miradi iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24 ambapo Mamlaka ilisajili jumla ya miradi **24** yenye thamani ya **dola za Marekani milioni 355.12** na iliyotarajiwa kuzalisha ajira mpya **19,877**. Kati ya miradi hiyo iliyosajiliwa, miradi **9** sawa na **asilimia 31** inamilikiwa na Watanzania, miradi **2** sawa na **asilimia 7** ni ya Ubia na miradi **18** sawa na **asilimia 62** inamilikiwa na wageni (**Kiambatisho Na. 4**).

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi kupitia Mamlaka ya EPZA ni kilimo miradi **13** sawa na **asilimia 45**; uzalishaji viwandani miradi saba (**7)** sawa na **asilimia 25;** madini miradi mitano (**5)** sawa na **asilimia 17**; miundombinu miradi miwili (**2)** sawa na **asilimia saba (7);** afya mradi mmoja (**1)** sawa na **asilimia tatu (3)** na misitu mradi mmoja (**1)** sawa na **asilimia tatu (3)**. Rejea **Kiambatisho Na. 5**.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi kupitia Mamlaka ni kilimo miradi **13** sawa na **asilimia 45**; uzalishaji viwandani miradi saba (**7)** sawa na **asilimia 25;** madini miradi mitano (**5)** sawa na **asilimia 17**; miundombinu miradi miwili (**2)** sawa na **asilimia saba (7);** afya mradi mmoja (**1)** sawa na **asilimia tatu (3)** na misitu mradi mmoja(**1)** sawa na **asilimia tatu (3)**. Rejea **Kiambatisho Na. 5**.

***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kufanyika katika Mikoa mbalimbali kama ifuatavyo: Dar es Salaam **miradi 11**; Iringa mitatu (**3)**, Tanga **mitatu (3),** Mtwara mitatu (**3)**, Pwani **mmoja (1)**, Lindi **mmoja (1)**, Katavi **mmoja (1)**, Morogoro **mmoja (1)**, Shinyanga **mmoja (1)**, Arusha **mmoja (1)**, Mbeya **mmoja (1)**, Kigoma **mmoja (1)** na Njombe **mradi mmoja** (**1)**, rejea **Kiambatisho Na. 6.**

**(xx) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa**

**70.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, TIC imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi ya kimkakati (strategic investment projects) na kimkakati maalum (special strategic investment projects) ambapo jumla ya miradi Saba **(**7), ilijadiliwa na kuidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (NISC) mwezi Novemba 2024. Miradi hiyo ni kampuni ya Camel Gas kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mafuta; kampuni ya Maweni Limestone kwa ajili ya kiwanda cha uzalishaji wa saruji; kampuni ya Kinglion Investment kwa ajili ya uzalishaji wa mabati; kampuni ya East Africa Commercial and Logistics Co. Ltd (EACLC) kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya biashara; kampuni ya GSM Tanzania kwa ajili ya uzalishaji wa vyakula na vinywaji; kampuni ya Shafa Agro Ltd kwa ajili ya ufugaji na uchakataji wa mazao ya maziwa; na kampuni ya Kilimanjaro Industrial Park kwa ajili ya ujenzi wa kongani za viwanda. Faida tarajiwa za miradi hiyo ni pamoja na uzalishaji wa ajira, ongezeko la mitaji toka nje na ndani ya nchi, na faida nyingine ikiwemo ukuaji wa matumizi ya teknolojia.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa kuratibu uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji Serikali kupitia TIC imetembelea jumla ya miradi **20** ili kubaini changamoto na kuzitatua. Utatuzi wa changamoto hizo umewezesha miradi kuimarika zaidi na kuwa kielelezo cha mazingira bora ya uwekezaji hapa nchini. Miradi hiyo ina thamani ya mitaji halisi ya **dola za Marekani milioni 1,832.24** na imezalisha jumla ya ajira halisi **65,436.**

### (xxi) Kuanzisha masijala ya kielektroniki ya ardhi kwa wawekezaji

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2025, Serikali kupitia TIC imetenga maeneo manne (4) yenye ukubwa wa hekta **84,403.73** kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje. Maeneo hayo yanapatikana katika mikoa ya Kigoma, Morogoro, na Tanga. Kati ya maeneo hayo Serikali imefanikiwa kukodisha jumla ya hekta **73,881.9** katika mashamba matatu. Mashamba hayo ni Mkulazi - Morogoro lenye ukubwa wa hekta **60,103**, Lugufu - Kigoma lenye ukubwa wa hekta **10,529.9** na Basanza- Kigoma lenye ukubwa wa hekta **3,249**. Aidha, eneo lenye ukubwa wa hekta **10,521.83** lililopo Pangani - Tanga linaendelea kutafutiwa wawekezaji. Vilevile, Kituo cha Uwekezaji kinaendelea na maandalizi ya mkakati wa uanzishwaji wa masijala ya kielektroniki ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

### (xxii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya uwekezaji

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, kama ilivyo ainishwa kwenye Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 2022, Ofisi kupitia TIC imeanzisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Uwekezaji. Hadi Machi 2025, Ofisi imefanya ufuatiliaji wa miradi ya kimkakati na kimkakati maalum ambapo jumla ya **miradi 16** ilitembelewa. Vilevile, Kituo kiliendelea na ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya kawaida ya uwekezaji ambapo jumla ya **miradi 6,304** ilitembelewa. Lengo la ufuatiliaji na tathmini hizo ni kujionea maendeleo, kusikia changamoto hasa katika mchakato wa utoaji wa Tangazo la Serikali (GN) na utekelezaji wake na kuona namna ya kutatua changamoto hizo. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini hiyo yamesaidi kutatua changamoto zilizokuwa zinawakumba wawekezaji pamoja na kupata mrejesho wa hali halisi ya maendeleo ya miradi.

### (xxiii) Kuhamasishaji uwekezaji wa Watanzania

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi iliendesha kampeni ya kitaifa katika mikoa yote nchini yenye lengo kuu la

kuhamasisha uwekezaji wa ndani, kampeni iliyobebwa na kauli mbiu ***"2024 Isipite bila Kutekeleza Mradi Wako"***. Kampeni hii imefanyika kwa kushirikisha wadau wa uwekezaji katika mikoa husika ikiwa na malengo yafuatayo: kubadili fikra na mtizamo wa kwamba TIC ni mahsusi kwa wawekezaji wa kutoka nje ya nchi na siyo kwa watanzania; kutoa elimu ya uwekezaji hususan taratibu za kusajili miradi ya uwekezaji; na kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayomilikiwa na Watanzania kwa lengo la kuwashirikisha kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

**(xxiv) Kufanya tathmini ya thamani ya uwekezaji na athari ya miradi ya kielelezo na kimkakati katika kuendeleza na kukuza uchumi**

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika miradi na programu za Serikali, Tume ilifanya uchambuzi wa miradi na programu zinazotekelezwa na Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi thabiti na ufanisi katika programu za maendeleo. Kufuatia uchambuzi huo ilibainika kuwa jumla ya miradi 9,711 inatekelezwa na Serikali katika ngazi mbalimbali, matokeo ya uchambuzi huo ni msingi katika kuwezesha ufuatiliaji na tathmini za programu na miradi ya maendeleo. Aidha, Tume imeendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo (NPMIS) ili kuongeza ufanisi katika uchambuzi wa maandiko ya miradi na programu kupitia teknolojia ya kisasa na akili mnemba. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya maandiko 150 ya miradi na programu mbalimbali yamechambuliwa na kutolewa maoni kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaleta tija.

**(xxv) Kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo**.

**76.** ***Mheshimwa Spika,*** katika kuhakikisha ushiriki wa sekta binafsi katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Ofisi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango imeendelea na maandalizi ya taarifa ya tathmini ya mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Vilevile, imetekeleza

mkakati wa kuwakutanisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi kupitia mdahalo wa pamoja (Public-Private Dialogue – PPD) uliokuwa na lengo la kuimarisha ushirikiano katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

**(xxvi) Kuandaa Mpango Mkakati wa Muda Mrefu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kipindi cha miaka 25.**

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25, Ofisi kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kuandaa Mpango Mkakati wa Muda Mrefu kwa kipindi cha miaka 25. Hadi Machi, 2025 Ofisi imeendelea na maandalizi ya Mpango wa Muda Mrefu wa Ofisi wa mwaka 2025/26 - 2049/50. Lengo la Mpango huu ni kuandaa mikakati ya muda mrefu itayowezesha Taasisi na Mashirika ya Umma kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuchangia pato la Taifa kwa asilimia 10 hadi 15. Aidha, tayari Ofisi imeshampata Mshauri Elekezi atakayeandaa Mpango huo.

**(xxvii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na tathmini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kampuni Tanzu na Kampuni ambazo Serikali ni mbia pamoja na mashirika yaliyobinafsishwa**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imekamilisha tathmini ya utekelezaji wa mikataba ya utendaji kazi ambayo iliingiwa mwaka 2022/23 (kulingana na taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa) ya Taasisi na Mashirika ya Umma. Hadi Machi 2025, tathmini imefanyika kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma **34** kati ya **50** yaliyopangwa kufanyika sawa na ufanisi wa **asilimia 68.** Maandalizi ya kufanya tathmini kwa Taasisi na Mashirika ya Umma **16** yaliyosalia yanaendelea. Aidha, Ofisi imefanya Ukaguzi wa Kimenejimenti katika Taasisi na Mashirika ya Umma **36** sawa na **asilimia 72** ya lengo la kukagua mashirika **50.** Rasimu za taarifa za ukaguzi wa kimenejimenti zipo kwenye hatua ya mapitio kabla ya kuwasilishwa kwenye Mamlaka mbalimbali kwa hatua stahiki. Tathmini hiyo ilijikita katika uzingatiaji wa sheria, kanuni na

miongozo kuhusu masuala ya kiutendaji, utawala na usimamizi wa rasilimali watu.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi imeendelea na ujenzi wa *Dashboard* yenye lengo la kuboresha usimamizi katika uendeshaji wa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma. Mfumo huo utawezesha upatikanaji wa taarifa za Taasisi hizo katika dirisha moja, kurahisisha uchambuzi wa utendaji kazi wa mashirika na usimamizi sahihi wa taarifa za mashirika. Taarifa hizo ni pamoja na uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma, uchangiaji wa mapato yasiyo ya kikodi katika mfuko mkuu wa Serikali, bodi za wakurugenzi pamoja na upimaji wa utendaji wa bodi hizo. Aidha, mchakato wa uandaaji wa mikataba ya utendaji kazi (Performance Contract), utekelezaji wake na tathimini vitafanyika kwa kutumia mfumo huo.

**80.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi iliandaa Taarifa ya Fedha ya Mwaka 2023/24 na kuiwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria. Taarifa hiyo inaonesha uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma **253** yanayomilikiwa na Serikali kama mbia mkuu pamoja na kampuni **56** ambayo Serikali inamiliki hisa chache umeongezeka kwa **asilimia 13.85** kutoka **Shilingi trilioni 75.79** katika mwaka wa fedha 2022/23 hadi **Shilingi trilioni 86.29** katika mwaka 2023/24. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya taasisi na mashirika ya umma pamoja na ongezeko la thamani ya mizania ya kampuni ikiwemo Benki ya NMB PLC, Benki ya NBC Ltd, Kilombero Sugar Ltd, TPC Ltd na Airtel Tanzania PLC.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2025, Ofisi imefanikisha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Taasisi za umma ikiwemo Shirika la Nyumba la Taifa - NHC (**Shilingi bilioni 269.33),** Chuo cha Uhasibu Arusha - IAA (**Shilingi bilioni 8**), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA (**Shilingi bilioni 27.58**), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro - NCAA (**Shilingi bilioni 266.68**), na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara - MTUWASA (**Shilingi bilioni 1.22**).

**(xxviii) Kuandaa Mkakati Fungamanishi wa Kisekta wa Ufuatiliaji na Tathmini**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ilipanga kuandaa Mkakati Fungamanishi wa Kisekta wa Ufuatiliaji na Tathmini kuhusu masuala ya mipango na uwekezaji. Hadi Machi, 2025 Ofisi imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini ambayo ipo katika hatua za mapitio na kukusanya maoni ya wadau. Aidha, kukamilika kwa Mwongozo huo kutawezesha utekelezaji wa mkakati fungamanishi wa Kisekta wa Ufuatiliaji na Tathmini katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

**(xxix) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utendaji kazi, Ofisi imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi. Hadi Machi 2025 Ofisi imetoa miongozo mbalimbali ya huduma za kiutawala, kiutumishi na kisheria. Aidha, watumishi wanaendelea kujengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali ikiwemo takwimu, uchumi, ugavi, TEHAMA, menejimenti ya rasilimali watu na usimamizi wa miradi, ufuatiliaji na tathmini. Pia, Ofisi imefanikiwa kununua vitendea kazi ikiwemo magari kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake, kutoa vitendea kazi kwa watumishi pamoja na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambapo kwa sasa ujenzi umefikia **asilimia 74**.

**3.4. UTEKELEZAJI WA MAENEO MENGINE MUHIMU KWA MWAKA 2024/25**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utekelezaji wa vipaumbele kwa mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imefanikiwa kutekeleza maeneo mengine muhimu kama ifuatavyo:-

(i) **Kuratibu Mkutano wa Mwaka wa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu Mkutano Mkuu wa Pili wa mwaka wa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa lengo la kuwakumbusha wajibu na msingi wa dhamana waliyopewa na Serikali katika kusimamia utendaji wa Taasisi za Umma. Mgeni Rasmi wa Mkutano huo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huo ulikuwa na jumla ya **washiriki 642**. Aidha, mada mbalimbali ziliwasilishwa kutoka kwa Wawasilishaji wa ndani na nje ya nchi zikilenga kuwajengea uwezo na kuwapa uzoefu Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika kuboresha utendaji wa Taasisi wanazosimamia ndani ya nchi na pia kuona na kutumia fursa za kuwekeza nje ya nchi chini ya Kauli Mbiu isemayo "***Mikakati ya Taasisi na Mashirika ya Umma Kuwekeza Nje ya Tanzania***''.

**(ii) Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa wajumbe wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma**

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi ilitoa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi **234** kutoka Taasisi **29** ikilinganishwa na malengo ya kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi **250** kutoka katika Taasisi **30** katika mwaka 2024/25. Wajumbe wa Bodi zilizofanyiwa mafunzo wameteuliwa katika kipindi cha mwaka 2022/23 hadi Februari, 2025. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uelewa wa majukumu yao katika Bodi, matarajio ya Serikali kutoka katika Bodi hizo pamoja na miongozo muhimu wanayopaswa kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu yao.

**(iii) Kuandaa Taarifa za Wasifu wa Miradi kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma nchini kwa ajili ya kuitangaza kwa wawekezaji**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi za Umma ilifanya uchambuzi wa miradi kwa kuzingatia sekta

zitakazochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka kwa maendeleo jumuishi na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/26. Uchambuzi huo ulilenga kuandaa Taarifa ya Wasifu wa Miradi ya kimkakati ya Umma kwa lengo la kuitangaza kwa wawekezaji. Wasifu wa miradi iliyoandaliwa itarahisisha Wawekezaji wa ndani na nje kupata taarifa za miradi husika, mahali ilipo, hatua iliyofikiwa, gharama na vivutio vinavyotolewa na Serikali. Aidha, taarifa hiyo itawezesha Sekta Binafsi na Umma kushirikiana katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

**(iv) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Kimkakati katika Sekta ya Umma**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 12 ya kimkakati inayotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya Umma kwa lengo la kubaini hatua za utekelezaji; kufahamu changamoto katika kukamilisha miradi husika; na kushauri hatua za kuchukua kutokana na changamoto zilizobainika ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa inafikia malengo yaliyokusudiwa. Miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini ni miradi kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Taasisi ya Mifupa (MOI), Kiwanda cha Madawa cha Keko, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN).

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, tathmini hiyo ilibainisha changamoto mbalimbali ikiwemo kutokuanza kutumika kwa baadhi ya miradi kutokana na kutokamilika kwa miradi saidiizi na kukosekana kwa fedha za uendeshaji baada ya miradi kukamilika zinazopelekea kukwamisha utekelezaji wa miradi hiyo kama ilivyopangwa. Kufuatia tathmini hiyo, Ofisi ilitoa mapendekezo kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo inakamilika. Aidha, katika changamoto hizo kuna baadhi zinahitaji kuchukuliwa hatua za haraka ili kuepuka kusuasua kwa miradi

hiyo kwa kuzingatia kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi kwa lengo la kupata tija.

**(v) Kuandaa Mkakati wa Kitaifa kuhusu Uwekezaji**

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha tunaenda sambamba na mabadiliko yanayotokea duniani katika nyanja ya uwekezaji, Ofisi inaendelea na ukamilishaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uwekezaji. Lengo la mkakati huo ni kubainisha fursa za uwekezaji katika sekta za kipaumbele kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa shughuli za uhamasishaji na uwezeshaji uwekezaji nchini na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi

**(vi) Kuratibu Ushiriki wa Nchi Kwenye Majadiliano ya Mikataba ya Kimataifa ya Uwekezaji**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kushiriki katika majadiliano ya Mikataba ya Kimataifa ya Uwekezaji (*International Investment Agreements* – IIAs) ikiwemo Mikataba ya uwili ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji (*Bilateral Investment Treaties* – BITs) baina ya Tanzania na nchi nyingine. Hadi kufikia Machi 2025, Ofisi imefanya majadiliano na nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Canada na Indonesia. Aidha, Ofisi imeratibu majadiliano ya awali ya Mikataba ya Ubia wa Kiuchumi (EPA) baina ya Tanzania na nchi za UAE na kati ya Tanzania na Korea. Mikataba ya Ushirikiano wa Kiuchumi inalenga kukuza biashara, uwekezaji na ushirikiano katika sekta za kipaumbele. Vilevile, Ofisi imeshiriki katika majadiliano ya Mkataba wa Itifaki ya Uwekezaji ya Eneo Huru la Biashara Afrika (*AfCFTA Investment Protocol*) yalihusu Kiambatisho cha Kanuni na Taratibu zinazosimamia Uzuiaji, Usimamizi na Utatuzi wa Migogoro ya wawekezaji wakati wa utekelezaji wa Itifaki hiyo, ili kuimarisha mazingira ya uwekezaji kwa wawekezaji wa Afrika.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Ofisi iliratibu maandalizi ya Mkutano wa Kwanza wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano wa Biashara na Uchumi kati ya Urusi na Tanzania uliofanyika tarehe 28 – 29 Oktoba 2024 jijini Dar es Salaam, Tanzania. Mkutano huo ni utekelezaji wa Hati ya Makubaliano baina ya Serikali za Tanzania

na Urusi iliyosainiwa mwaka 2022. Lengo la makubaliano hayo ni kuanzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano wa Kiserikali kwenye maeneo ya Biashara na Uchumi. Ofisi inaendelea na uratibu wa utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huo kupitia Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na maandalizi ya Mkutano wa Pili utakaofanyika mwezi Mei 2025 nchini Urusi.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini, Ofisi imeandaa na kushiriki katika makongamano na mikutano ya Uwekezaji na biashara ya ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi Machi, 2025, Ofisi imeandaa na kushiriki makongamano **11** ya nje ya nchi. Makongamano hayo ni baina ya Tanzania na nchi za: Korea, China, Saudi Arabia, Oman, Ufaransa, Ubelgiji, Misri, Marekani, India, Italia na Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika makongamano hayo mafanikio mbalimbali yalipatikana ikiwemo kusaini Hati za Makubaliano, kupokea ujumbe wa wafanyabiashara na wawekezaji takribani **200** kutoka nchi za Saudi Arabia, Ubelgiji, China, Japani na Italia kwa lengo la kuwekeza nchini. Aidha, kwa upande wa makongamano ya ndani ya nchi, Ofisi imeratibu na kushiriki katika kuhamasisha uwekezaji wa ndani katika Mikoa **10** ya Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Simiyu, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, na Katavi.

**(vii) Kuandaa Mfumo wa Kanzidata ya Kitaifa ya Uwekezaji**

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kanzidata ya Kitaifa wa Uwekezaji (National Investment Database System) unaolenga kuunganisha mifumo ya usajili wa miradi ya uwekezaji inayosimamiwa na taasisi zinazohusika na masuala ya uwekezaji zikiwemo TIC, EPZA, Tume ya Madini, PURA, TMDA na EWURA. Aidha, Mfumo huo unalenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa taarifa na takwimu za uwekezaji. Hadi Machi 2025, Ofisi imekamilisha uandaaji wa mfumo na kufanya majaribio, kutoa mafunzo ya matumizi kwa Timu ya Watalaam kutoka Wizara, Taasisi na Idara za Serikali. Pia,

inaendelea kukusanya na kuhakiki taarifa za miradi ya uwekezaji kwa ajili ya kuingizwa kwenye mfumo.

### 3.5. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**95. *Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2024/25 Ofisi ilipanga kutekeleza mradi wa uimarishaji wa Taasisi (Institutional Support) unaolenga kuhamasisha na kusimamia Uwekezaji na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Kupitia mradi huo, Ofisi imeanza kuandaa Mkataba wa Kifani wa Kukuza na Kulinda Uwekezaji, Kuwezesha kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma, uchambuzi wa Sera za kisekta kuhusiana na masuala ya uwekezaji, Kufanya ufuatiliaji wa miradi ya uwekezaji, kujengewa uwezo watumishi nane (8) kuhusu usimamizi na uchambuzi wa uwekezaji katika sekta ya umma na kufanya stadi kizio kuhusu Sera ya Uwekezaji wa Umma. Utekelezaji wa kazi hizo unaendelea.

**96. *Mheshimiwa Spika*,** pia, Ofisi imeratibu utekelezaji wa programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP). Katika kipindi husika, Ofisi imetekeleza yafuatayo: kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; kuandaa mahitaji na kuanza kujenga kanzidata ya takwimu za Ofisi; kuwajengea uwezo maafisa viungo wa ufuatiliaji na tathmini 30 katika hatua za ufuatiliaji na Tathmini kwa kuzingatia matokeo na mbinu za uandishi wa taarifa; kuandaa mahitaji ya mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji na tathmini wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na kuwajengea uwezo watumishi 11 katika ufuatiliaji na Tathmini wa viashiria vya kitaifa vya uwekezaji.

**97. *Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara (Implementation of BEST Programme) ambapo shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

a. Kufanya marekebisho ya Sheria 12 kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*Miscellaneous Amendments*) ya mwaka 2024 zilizolenga kuweka unafuu katika mazingira ya biashara na uwekezaji;

b. Kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini (Government e - Payment Gateway – GePG) ambao umerahisisha taratibu za ulipaji wa ada na tozo mbalimbali za Serikali. Kwa mwaka 2024 vituo vya kutolea huduma na Taasisi mpya **24** vimeunganishwa kwenye mfumo huo na kufanya jumla ya Taasisi na vituo vya kutolea huduma vilivyounganishwa kufikia **1,007** kutoka watoa huduma **983** waliounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la **asilimia 2.4**;

c. Kuimarishwa kwa Mfumo wa Kuwezesha Mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidigitali (*Government Enterprise Service Bus - GovESB*) ambapo mifumo **179** ya Taasisi za Umma imeunganishwa ikilinganishwa na mifumo **130** iliyounganishwa awali. Hatua hii inajumuisha taasisi za Umma **202** kutoka Taasisi za Umma **119** zilizojumuishwa awali;

d. Kuimarishwa kwa Mfumo wa Kuwezesha Mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidigitali (*Government Enterprise Service Bus - GovESB*) ambapo mifumo **179** ya Taasisi za Umma imeunganishwa ikilinganishwa na mifumo **130** iliyounganishwa awali. Hatua hii inajumuisha taasisi za Umma **202** kutoka Taasisi za Umma **119** zilizojumuishwa awali;

e. Kukamilika kwa ujenzi wa awamu zote tatu (3) za Mfumo wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (*Tanzania electronic Single Window System - TeSWS*) kwa kushirikiana na sekta binafsi. Ukamilishaji wa mfumo huo umewezesha kubadilishana taarifa na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - TANCIS, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania – (TPA) - TOS, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na

Vifaa Tiba (TMDA), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Bodi ya Nyama (TMB), Bodi ya Maziwa (TDB), Wizara ya Mifugo na Wizara ya Uvuvi; na

f. Serikali imekamilisha ujenzi wa mifumo mbalimbali: Mfumo wa Uchakataji Maombi ya Leseni za Utalii Kidigitali unaoungalisha mifumo ya BRELA, Bodi ya Utalii na OR-TAMISEMI; Mfumo wa kidigitali unaounganisha taasisi za COSOTA, BASATA, na Bodi ya Filamu Tanzania (TFB); na Kanzidata ya kodi, ushuru, leseni na vibali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mfumo wa TAUSI ambapo *module* ya vibali na leseni (*database for levies, fees and charges*) katika mfumo huo zinazoweka wazi sheria ndogo, ada, na tozo kwa wawekezaji na wafanyabiashara. Mifumo hii inarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wakati.

**98.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi kupitia mradi wa Tanzania Mini Tiger Plan 2020 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita tatu (3) kwa kiwango cha lami kwenye eneo la viwanda Zinga Bagamoyo; kuteua Kamati ya Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi wanaohusika na utekelezaji wa mradi ili kuimarisha uratibu; kukamilika kwa kumpata Mtaalam Mshauri atakayeandaa ramani ya mipango miji - Town Planning (TP) Map, Usanifu wa michoro ya majengo, *Topographical survey* na kuandaa gharama za ujenzi katika eneo la Bagamoyo; na kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya ndani katika eneo la uwekezaji la Benjamin William Mkapa.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mradi wa Uendelezaji wa Maeneo Maalum kwa Uzalishaji wa Bidhaa kwa Mauzo ya Nje - Export Processing Zone Development shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ukamilishaji wa Upembuzi Yakinifu,

Mpango Kabambe (Feasibility Study and Master Plan) wa Ukanda Maalum wa Kiuchumi wa Manyara; kukamilika kwa kuwapata Wataalam Washauri Elekezi wanaofanya kazi ya kuandaa Mpango Kabambe, Upembuzi Yakinifu, *Topographical & Cadastral Surveys* pamoja na usanifu wa miundombinu ya msingi katika maeneo ya Nala, Ruvuma, Mara na Kwala SEZ.

**Sura ya Nne**

## 4. MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2025/26

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Ofisi pamoja na taasisi kwa mwaka 2024/25, sasa napenda kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2025/26.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2025/26 umezingatia miongozo mbalimbali ya Kisera, Sheria, Kanuni na Mikakati ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja na Mpango Mkakati wa Mpito wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji wa 2024/25 - 2025/26; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake; Mikakati na makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; Mkakati wa Sita wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa miaka mitano (2021/22-2025/26); Agenda ya Umoja wa Afrika 2063: Afrika Tuitakayo; Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs); Mikakati ya kisekta na masuala mtambuka ikiwemo

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV) 2023-2030 na UKIMWI.

### 4.1. VIPAUMBELE KWA MWAKA 2025/26 NA MAOMBI YA FEDHA KWA KILA FUNGU

#### 4.1.1. Fungu 011: Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, Maeneo ya vipaumbele ambayo yamepangwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (Fungu 011) kwa Mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo :

(i) Kuratibu maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kuzingatia Dira Mpya ya Maendeleo ya Mwaka 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka kwa mujibu wa Mwongozo wa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050;

(ii) Kuratibu ushiriki wa nchi na kusimamia majadiliano ya mikataba ya kimataifa ya uwekezaji baina ya nchi, katika ngazi ya kikanda na kimataifa;

(iii) Kuratibu na kusimamia uwekezaji katika Kanda Maalum za Kiuchumi na kongani za viwanda;

(iv) Kuratibu na kusimamia uwekezaji wa umma;

(v) Kuratibu uhamasishaji na uwezeshaji wa uwekezaji wa sekta binafsi;

(vi) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;

(vii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; na

(viii) Kuandaa Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II) ili kujumuisha maeneo mapya yaliyojitokeza na yanayoendelea kujitokeza kutokana na mabadiliko ya uchumi wa dunia na teknolojia.

#### 4.1.2. Fungu 066: Tume ya Taifa ya Mipango

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa na Tume ya Taifa ya Mipango ni kama vifuatavyo: -

(i) Kufanya tathmini ya matokeo ya miradi ya kielelezo na kimkakati katika kuendeleza na kukuza uchumi;

(ii) Kuwezesha tafiti ili kukuza ubunifu katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo;

(iii) Kufanya utambuzi wa maeneo muhimu ya vipaumbele vya kitaifa yenye matokeo makubwa ili kuwianisha na matumizi yenye tija ya rasilimali za nchi;

(iv) Kuandaa nyenzo za utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na kutoa elimu kwa umma;

(v) Kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi na kutoa miongozo ya mashirikiano kwa ajili ya kufanikisha upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo; na

(vi) Kuendelea kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi kupitia mifumo ya TEHAMA na kuwajengea uwezo watumishi katika kusimamia uchumi, upangaji na utekelezaji wa mipango.

### 4.1.3. Fungu 007: Ofisi ya Msajili wa Hazina

**104.** **Mheshimiwa *Spika,*** vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ni kama vifuatavyo:-

(i) Kukamilisha na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Muda Mrefu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina wa Mwaka 2025/26 – 2049/50;

(ii) Kuendelea kufanya ufatiliaji na tathmini ya mali za Serikali zilizo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na zilizobinafsishwa ikiwemo mashamba; viwanda na viwanja;

(iii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kikodi;

(iv) Kuimarisha usimamizi na tathmini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kampuni Tanzu na Kampuni ambazo Serikali ni Mbia; na

(v) Kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuimarisha utendaji kazi.

### 4.1.4. Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa mwaka 2025/25 zimepanga kutekeleza vipaumbele kama vifuatavyo: -

(i) Kuendeleza miradi ya kitaifa ya Kielelezo (National Flagship Projects) ikiwa ni pamoja na kuanza hatua za awali za uendelezaji katika maeneo ya Ruvuma, Mara, Tanga, Shinyanga;

(ii) Kuzindua na kutangaza mradi wa Bagamoyo SEZ kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa nia ya kuendeleza mradi kwa njia mbalimbali ikiwemo ubia na sekta binafsi kwa kufuata mpango uliorejewa;

(iii) Kubaini bidhaa na kutumia huduma za Soko la Mitaji (Capital Markets) kupata fedha za kuendeleza miradi ya SEZ;

(iv) Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwenye Maeneo Maalum ya Kiuchumi kupitia dirisha la huduma za mahala pamoja kwa kutumia mfumo wa kidigitali;

(v) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo ya viwanda vilivyokabidhiwa kwa Mamlaka na Msajili wa Hazina;

(vi) Kuendeleza Maeneo Maalum ya Kiuchumi kwa kushirikiana na TAMISEMI, Sekta binafsi na Wadau wa maendeleo;

(vii) Kutoa elimu kwa Umma, kufanya tafiti, ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyopewa leseni na Mamlaka;

(viii) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa;

(ix) Kuboresha mifumo ya kusajili na kuhudumia wawekezaji;

(x) Kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kutoa majawabu kuwezesha kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuibua fursa mpya za uwekezaji nchini;

(xi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya uwekezaji; na

(xii) Kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuboresha mashirikiano kati ya TISEZA na wadau wa umma na binafsi ili kurahisisha jukumu la uratibu wa uhamasishaji na huduma kwa wawekezaji nchini.

**Sura ya Tano**

## 5. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, OFISI YA MSAJILI WA HAZINA NA TUME YA TAIFA YA MIPANGO KWA MWAKA 2025/2026

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kueleza utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2024/25 na vipaumbele vya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2025/26, ninaomba sasa kuwasilisha rasmi Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/26 kwa muhtasari kama ifuatavyo:

**(a) Mapato**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Ofisi ya Msajili wa Hazina - Fungu 007 imepangiwa kukusanya na kuchangia kwenye mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya **Shilingi trilioni 1.56** kutoka kwenye vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi kupitia gawio, michango ya **asilimia 15** ya mapato ghafi,mapato yatokanayo na Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS); rejesho la riba na mikopo, ziada na mapato mengineyo.

**(b) Matumizi**

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha jumla ya **Shilingi 148,629,961,000** ikiwa **Shilingi 122,122,685,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 26,507,276,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2025/26.

Uchambuzi wa kina wa matumizi wa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Namba 1 hapo chini.**

**Jedwali 1:** Matumizi kwa Fungu 11; 007; na 066

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a.** | **Fungu 011: Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji** | | |
| i) | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 22,392,185,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 15,475,308,000 |
| | **Jumla Ndogo A** | **Sh.** | **37,867,493,000** |
| ii) | **Fungu 066: Tume ya Taifa ya Mipango** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 39,145,369,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 9,361,277,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **48,506,646,000** |
| iii) | **Fungu 007: Ofisi ya Msajili wa Hazina** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 60,585,131,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 1,670,691,000 |
| | **Jumla Ndogo** | Sh. | **62,255,822,000** |
| | Jumla Kuu - Matumizi ya Kawaida | Sh. | 122,122,685,000 |
| | Jumla Kuu - Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 26,507,276,000 |
| | **Jumla Kuu kwa Mafungu Yote** | **Sh.** | **148,629,961,000** |

## 6. HITIMISHO

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyotangulia kusema awali, Mkutano huu wa Bunge ni wa mwisho katika muhula huu wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Sita. Ninapenda kutumia fursa hii kukiri kuwa, katika kipindi chote cha muhula huu, Ofisi imenufaika sana na maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao umesaidia kuchochea uwekezaji na kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa maono yake na maelekezo yaliyochochea uandaaji na usimamizi wa mipango na kuinua sekta ya uwekezaji kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, akiwa kwenye ziara ya kikazi Jijini Tanga mnamo tarehe 01 Machi, 2025 aliendelea kuwahakikishia wawekezaji kuwa "***Tanzania imefunguka kwa uwekezaji, Tanzania ni salama kwa uwekezaji, na sera za uwekezaji za Tanzania ni rafiki na endelevu.”*** Kauli hiyo imekuwa chachu kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na imeendelea kuhamasisha idadi kubwa ya wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania. **Hatuna shaka kwamba kwa mambo haya makubwa ya kimaendeleo aliyolifanyia Taifa letu, Watanzania kwa ujumla wataendelea kumuamini na kumpa kura nyingi katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, 2025.**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa kiti cha Urais pamoja na mgombea mwenza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025. Timu hii ni ya ushindi na hakuna shaka kuwa itashinda kwa kishindo. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya urais na Mwenyekiti wa Serikali na Baraza la Mapinduzi Zanzibar kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). **HAKIKA KAZI NA UTU – TUNASONGA MBELE**

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo**, Mbunge makini wa Jimbo la Maswa Mashariki na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi. Nampongeza sana kwa uchapakazi na kujitoa kwake na ninapenda niwaombe Wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki wamrejeshe kwa kishindo katika Bunge lijalo. Aidha, namshukuru **Dkt. Tausi Mbaga Kida**, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wa Taasisi kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya Ofisi na Taasisi. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Idara, Vitengo na

Wafanyakazi wote wa Ofisi na Taasisi zake, kwa ushirikiano na utekelezaji mzuri wa majukumu yao ya kila siku.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru wadau wote waliochangia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, pamoja na taasisi zilizo chini yake. Wadau hao ni pamoja na Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), TradeMark Afrika, Taasisi ya Gatsby Africa, Umoja wa Ulaya, Serikali ya Uingereza na Taasisi zake ikiwemo Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Uingereza (ODI), Benki ya Dunia, Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Shirikisho la wenye viwanda Tanzania (CTI), Taasisi ya Kilimo Afrika (AGRA), Shirika la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD), Benki ya Azania na Growth Teams.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyotanguliwa hapo awali kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ubungo kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita na kunipa ushirikiano na imani wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha, naomba niwaahidi kuwa tukiwa tunaelekea katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025 na wakati utakapofika na kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, mimi Kitila Alexander Mkumbo nipo tayari kuendelea kuwatumika kwa ari, moyo na nguvu zote.

***115.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, ninapenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, nawashukuru wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii na kuhakikisha inakamilika kwa wakati. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ambayo ni *www.planninginvestment.go.tz*

***116.*** ***Mheshimiwa Spika,*** sasa ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 148,629,961,000** ikiwa **Shilingi 122,122,685,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 26,507,276,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2025/26.

***117.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nimejulishwa kwamba Katibu Mkuu ameshaingia hapa Bungeni. Dkt. Kida, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu na sasa ataingia Mwenyekiti kunipokea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wetu mahiri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hiyo kwa huu Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba taarifa hii yote kwa pamoja iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti yanayokusudiwa na Kanuni ya 118(9) ya Kamati ya Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla kuonesha misingi na muundo wa taarifa ya pamoja kwa namna ya kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya Pili, inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti na utekelezaji wa miradi na mwendelezo wa uzingatiaji ushauri wa maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu, inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya Nne, inayohusu majumuisho na maoni ya ushauri wa Kamati; na

(e) Sehemu ya Tano, ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati hii kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na uratibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge za Februari, 2023 Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha nyongeza ya (8) ya Kanuni za Bunge zinazotambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, kanuni ya 114(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji ya makadirio ya ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa katika hili Bunge Tukufu. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huu Kamati ilipitia Mafungu matatu ambayo ni Fungu Na.7, Fungu 11 na Fungu 60. Fungu Na.7 linahusu Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 11 linahusu Ofisi ya Rais, Mipano na Uwekezaji na Fungu 66 ni Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji za bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi yanayoweka misingi ya ushauri kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, ninaomba kubainisha mambo makuu ambayo yaliyochambuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Makusanyo ya Maduhuli;

(b) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo;

(c) Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji;

(d) Uzingatiaji wa maazimio ya Bunge; na

(e) Ulinganisho wa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na makadiro ya matumizi ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilikadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi kiasi cha shilingi trilioni moja bilioni mia moja kumi na tatu nukta tisa kupitia Fungu Na.7, Ofisi ya Msajili wa Hazina. Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonyesha kuwa, ofisi hii kupitia Fungu Na.7 hadi kufikia Februari 2025 ofisi imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 562.5, sawa na 51% ya lengo la mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuweza kuongeza ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2023/2024 ambao hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikusanya maduhuli kwa 37% ya makadirio. Aidha, mchanganuo wa maduhuli ya Fungu Na.7 unaonyeshwa katika Jedwali Naamba Moja lililopo katika taarifa yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba, bado ukusanyaji wa maduhuli unaendelea na kwamba, hadi

itakapofika robo ya tatu na ya nne ya mwaka huu wa fedha unaoisha, Wizara kupitia Msajili wa Hazina watakuwa wameweza kufikisha lengo kwa kuwa gawio na michango kutoka mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa, ambapo kwa utaratibu uliopo gawio hutolewa kipindi hicho kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilielezwa kwamba, sehemu kubwa ya ukusanyaji wa maduhuli hadi kufikia Februari, 2025 unatokana na kodi za upangishaji, michango ya 15% ya mapato ghafi, gawio, marejesho ya *TTMS*, rejesho la riba na mikopo, ziada na malipo mengineyo ya ukusanyaji wa madeni, *XMDC* na ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi na matumizi ya bajeti Fungu Na.7 – Msajili wa Hazina. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa shilingi bilioni 167.8, baada ya uhamisho wa shilingi bilioni 115.5 ambayo ilitoka Wizara ya Fedha, ambayo iliwasilishwa Mamlaka ya Ngorongoro kwa ajili ya kutekeleza zoezi la uhamisho wa wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa, shilingi bilioni 7.3 zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 159.3 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya fedha za maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 132.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na 83% ya bajeti iliyoidhinishwa; ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 4.0 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 128.0 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kati ya fedha hizo za matumizi mengineyo, shilingi bilioni 117.7 ni kwa ajili ya matumizi maalumu na shilingi bilioni 10.3 ni kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi. Aidha, shilingi milioni 970.1 sawa na 75% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Naamba 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 30.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6.7 ni mishahara na shilingi bilioni 11.8 ni kwa ajili ya

matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 11.5 ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 15.2 sawa na 51%, ambapo shilingi bilioni 11.8 sawa na 63% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 4.4 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 7.3 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 3.4 ambayo ni sawa na 30%, zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 66 – Tume ya Mipango. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 46.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 37.8 sawa na 82% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 3.8 ni mishahara na shilingi bilioni 34 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 8.4 sawa na 18% ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 23.1, sawa na 50%. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 22.3 sawa na 44.4% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.9 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 20.4 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi milioni 715 sawa na asilimia 8.8 ilitolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonyesha kwamba, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni wa kuridhisha ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/2024, ambapo hadi kufikia Februari 2024 hakuna Fungu ambalo liliweza kupata fedha kwa uwiano wa 66.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kupeleka fedha kwa wakati kwenye Wizara hii muhimu, kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu la Tanzania. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza kikamilifu majukumu yaliyoweka kisheria ili kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa na vyanzo imara vya mapato ambavyo

vitatuondosha na kuwa tegemezi kwa fedha za nje. Mchanganuo wa fedha hizo kwa mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali namba mbili na Jedwali namba tatu, lililopo katika taarifa yetu hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu Namba 66 – Tume ya Mipango, Mradi 2229 ambao ulitengewa shilingi bilioni nane ambapo hadi kufikia Februari 2025 mradi huu ulipokea shilingi milioni 300.0 tu, sawa na asilimia 3.75 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mpango na majukumu ya Ofisi ya Rais. Bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishiwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara na taasisi zilizo chini ya ofisi hii ziliidhinishiwa shilingi bilioni 21.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha unaonekana katika jedwali namba nne lililopo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea mradi mmoja kati ya miradi saba inayotekelezwa na ofisi hii kwa kupitia bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, na kuchambua utekelezaji wa mradi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Namba 4933, Ujenzi wa Ofisi ya Kanda Maalumu ya Kiuchumi ya *Benjamin Mpaka Special Economic Zone* – Dar es Salaam. Mradi huu unahusu ujenzi wa

uzio ambao unatenganisha eneo la viwanda na eneo la kupooza umeme na ukarabati wa mifereji ya maji ya mvua katika Ukanda Maalum wa kiuchumi wa B*enjamin William Mkapa Special Economic Zone*. Mradi huu ulipokea fedha kiasi cha shilingi 149,900,530 mnamo Disemba, 2023 na ulianza kutekelezwa tarehe 19 Februari na ukakamilika Agosti, 2024 na kukabidhiwa kwa Serikali tarehe 20 Novemba, 2024. Aidha, Kamati ilielezwa kwamba mradi huu ulitekelezwa kwa kutumia utaratibu wa *force account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea baadhi ya wawekezaji ambao wanasimamiwa na Mamlaka ya Uwekezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi waliopo katika eneo hilo la *Benjamin Mkapa Special Economic Zone*, ambapo walionyesha kufurahishwa na usimamizi wa Wizara kwao kama wawekezaji. Aidha, walikuwa na maombi kwa Serikali kushirikiana na taasisi za kifedha kuwa na dirisha la kutoa mikopo kwa wamiliki wa viwanda na kuongeza thamani za bidhaa zao ili kuweza kushindana na bei ya Soko la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kufungua milango kwa wawekezaji nchini na kutafuta fursa kwa wawekezaji wazawa. Hali hii inadhihirisha namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kukuza sekta ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya ofisi hiyo. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi na makadirio ya matumizi ya Mwaka wa Fedha 2025/2026. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa kukusanya shilingi trilioni moja, milioni mia tano sitini na sita nukta mbili ikilinganishwa na shilingi trilioni moja, bilioni mia

moja sitini na nane nukta tano katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ambavyo imeidhinishwa katika jedwali namba tano lililopo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa kwamba, ongezeko hilo la makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 linatokana na uimarishaji wa mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ya Msajili wa Hazina, ambayo inaongeza usahihi wa takwimu, upatikanaji wa mapato kutoka kwenye mashirika ambayo Serikali ina hisa au kutegemea kupata gawio na kurahisisha utoaji taarifa na ufuatiliaji wa mapato na matumizi ya mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya kawaida, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizo chini yake, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 122.1 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 22.5 ni mishahara na shilingi bilioni 99.5 ni matumizi mengineyo ambayo yamechanganuliwa katika jedwali namba sita lililopo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2025/2026 imepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 59.5, sawa na 33%, ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoishia, ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wa bajeti wa shilingi bilioni 181.7, ikiwa ni baada ya ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 115.5 ambayo ilitoka Wizara ya Fedha na iliwasilishwa kwa Mamlaka ya Ngorongoro kwa ajili ya kutekeleza zoezi la uhamisho wa wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais,

Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 26.5 kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 14.5 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 11.9 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 5.2 sawa na 19.6%, ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Sababu ya kuongezeka kwa bajeti imechangiwa na mipango ya Serikali iliyowekwa kuhakikisha kwamba kuna maendeleo endelevu kwa Watanzania wote, kwa kuhimiza mipango madhubuti ya uwekezaji nchini, kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali namba saba lililopo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inazipongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Aidha, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kwamba fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinapatikana kwa wakati, zinatekeleza miradi iliyopangwa ili kuweza kuleta tija na ustawi kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne; Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa ofisi kujiwekea malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na.7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina:-

(i) Kwa kuwa uwekezaji wa kimkakati katika masoko ya hisa, taasisi binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa, Serikali inakosa gawio ambalo linaweza kutumika kwa maendeleo ya nchi;

(ii) Mali zilizorejeshwa Serikalini zisipofanyiwa tathmini zinaisababishia Serikali upotevu wa fedha kwa kushindwa kujua thamani halisi ya mali hizo;

(iii) Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokuwa na usimamizi madhubuti wa mashirika ya umma huchangia kukosekana kwa gawio na kupunguza mapato ambayo yameingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(iv) Kutokuwepo kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake, hupelekea kuonekana kuwa hakuna tathmini ya kutosha juu ya vyanzo hivyo vya ukusanyaji wa maduhuli;

(v) Madeni yanayotokana na ubinafsishaji wa mali ya Serikali ili kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato hayatakuwa na tija kwa Taifa, kama Msajili wa Hazina hatoboresha njia bora za kusimamia ukusanyaji wa mapato hayo kupitia vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; kutokuwepo kwa usimamizi Madhubuti, thabiti, wa Kanda Maalum ya Kiuchumi kunapelekea uanzishwaji wa kanda hizo kutokuwa na tija zilizokusudiwa na Taifa. Changamoto ya elimu ya kutosha ya uwekezaji na fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi, inapelekea wadau hao kuwekeza katika maeneo na miradi ambayo si ya kimkakati kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mahsusi, Fungu 66 – Tume ya Mipango;

(i) Serikali ihakikishe inaandaa nyenzo bora za utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020 – 2050 ili kuweza kuleta tija kwa wananchi;

(ii) Serikali ihakikishe ushiriki wa Sekta Binafsi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo nchini;

(iii) Serikali ifanye tathmini kuhusu miradi ya kimkakati inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo ineleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na.7 – Msajili wa Hazina:-

(i) Serikali kupitia Ofisi ya Msajhili wa Hazina ihakikishe kwamba inaendelea na uwekezaji katika Masoko ya Hisa, na taasisi binafsi zenye manufaa na tija kwa Taifa;

(ii) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inafanya tathmini ya mali zilizorejeshwa Serikalini, kuziendeleza ili ziweze kuongeza mapato kwa Serikali;

(iii) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia uwekezaji wa umma ili kuongeza mchango wa taasisi na mashirika hayo katika kuchangia, katika Mfuko Mkuu wa Serikali ili kukuza Pato la Serikali na Taifa kwa ujumla;

(iv) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaweka makadirio na makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo na ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake; na

(v) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaboresha vyanzo vingine vya mapato ikiwemo madeni yanayotokana na ubinafsishaji wa mali za Serikali ili kuboresha kuongeza makusanyo, ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 11 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji:-

(i) Serikali kusimamia uwekezaji wa kanda maalumu za kiuchumi ili kuleta tija kwa Taifa; na

(ii) Serikali iendelee kutoa elimu ya uwekezaji na fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kanda maalumu za kiuchumi na miradi ya kimkakati ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu wa kutupatia nafasi za kuwasilisha taarifa hii. Ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu hatimaye kukamilisha taarifa hii. Ninaomba majina yao yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni mwenyekiti wa Tume ya Mipango. Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Kwa ushirikiano ambao wameendelea kutoa kwa Kamati wakati wote wa kujadili mjadala wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati iliyoongozwa na Katibu Mkuu, ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida; Ndugu Fred Matola Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; na Ndugu Nehemiah Kyando Mchechu, Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka I. Leonard kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii. Aidha, kiupekee ninawashukuru Sekretarieti ya Kamati yetu kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii ambayo ninaiwakilisha mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, ambaye umekalia kiti hiki leo, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

***1.1. Maelezo ya Awali***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

### 1.2. *Msingi wa Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### *1.3. Mawanda ya Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matatu (3) ambayo ni: -

a) **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina;

b) **Fungu 11** - Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; na

c) **Fungu 66** – Tume ya Mipango

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 *Ufafanuzi wa Jumla*

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji;

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(e) Ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

### 2.2 *Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/25, ilikadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi kiasi cha **Shilingi 1,113,949,673,000.00** kupitia Fungu Na. 07 Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa Ofisi hii kupitia Fungu Na. 07 hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Ofisi imekusanya kiasi cha **Shilingi 562,585,408,207.53** sawa na **asilimia 51** ya lengo la mwaka.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuweza kuongeza Ukusanyaji wa Mapato ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo hadi kufikia Februari 2024 Wizara ilikusanya Maduhuli kwa **asilimia 37** ya makadirio.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa Fungu Na. 07 unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili Wa Hazina | 1,113,949,673,000 | 562,585,408,207.53 | **51** |
| **JUMLA KUU** | 1,113,949,673,000 | 562,585,408,207.53 | **51** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba bado ukusanyaji wa maduhuli unaendelea na hadi itakapofika robo tatu na nne ya mwaka huu wa fedha unaoisha Wizara kupitia Msajili wa Hazina watakuwa wameweza kufikisha lengo kwakuwa gawio na michango kutoka kwenye mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa ambao kwa utaratibu uliopo gawio hutolewa kipindi hiko kwa kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati ilielezwa kwamba Sehemu kubwa ya Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia Februari, 2025 unatokana na Kodi za Upangishaji, Michango ya asilimia 15 ya Mapato Ghafi, Gawio, Marejesho ya TTMS, Rejesho la Riba na Mikopo, Ziada na Malipo mengineyo na Ukusanyaji wa Madeni ya EX-NBC na Ubinafsishaji.

## 2.3 *Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti*

### *2.3.1* Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa Fedha 2024/25, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 167,895,468,325.00** baada ya uhamisho wa **Shilingi 115,513,345,325.00** ambayo ilitoka Wizara ya fedha ambayo iliwasilishwa Mamlaka ya Ngorongoro kwa ajili ya kutekeleza zoezi la uhamisho wa wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika** kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa, **Shilingi 7,305,056,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 159,300,754,325** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 1,289,658,000.00** kwa ajili ya Fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 132,106,065,459.31** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 83** ya bajeti iliyoidhinishwa, ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 4,069,756,537.04** ni kwa ajili ya Mishara **na Sh. 128,036,308,922.27** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo ambapo kati ya fedha hizo za matumizi Mengineyo **Sh. 117,702,209,549.57** ni kwa ajili ya matumizi maalum na **Sh. 10,334,099,372.70** ni kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi. Aidha **Sh. 970,188,000.00** sawa na **asilimia 75** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### 2.3.1 Fungu Na. 11- Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 30,216,547,238.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 18,632,828,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 6,774,092,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 11,858,736,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 11,583,719,238.00** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 15,290,692,815.34** sawa na asilimia **51** ambapo **sh. 11,804,354,730.34** sawa na **asilimia 63.3** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 4,436,098,062.00** ni

kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.7,368,256,668.34** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 3,486,338,085.00** sawa na **asilimia 30** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**2.3.2 Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 46,221,630,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 37,806,250,000.00,** sawa na **asilimia 82** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 3,806,250,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 34,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 8,415,380,000.00** sawa na **asilimia 18.2** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 23,100,442,792.08** sawa na asilimia **50** kati ya fedha hizo **sh. 22,384,992,792.08** sawa na **asiliimia 48.4** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 1,962,782,480.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.20,422,210,312.08** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 715,450,000.00** sawa na **asilimia 8.5** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba Upatikanaji wa Fedha kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa Fedha 2024/25 ni wa kuridhisha ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/24 ambapo hadi kufikia februari 2024 hakuna Fungu ambalo liliweza kupata fedha kwa Uwiano wa Asilimia 66.6.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kupeleka fedha kwa wakati kwenye Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yaliyowekwa kisheria kikamilifu ili kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa na vyanzo imara vya mapato ambavyo vitatuondosha na kuwa tegemezi kwa fedha nje.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Jedwali Na. 3**.

**JEDWALI NA. 2: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 159,300,754,325 | 132,106,065,459.31 | 84 |
| **Fungu 11** – Ofisi ya Rais,Mipango na Uwekezaji | **18,632,828,000.00** | **11,804,354,730.34** | 63.5 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **37,806,250,000.00** | **22,384,992,792.08** | 59.21 |
| **JUMLA KUU** | **181,714,207,325** | **166,295,412,981.73** | **91.5** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **1,289,658,000.00** | **970,188,000.00** | 75 |
| **Fungu 11**– Ofisi Rais Mipango na Uwekezaji | **11,583,719,238.00** | **3,486,338,085.00** | 48.58 |
| **Fungu 66** – Tume Mipango | **8,415,380,000.00** | **715,450,000.00** | 8.5 |
| **JUMLA KUU** | **21,288,757,238.00** | **5,171,976,085.00** | **24** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi ifuatayo;

a) **Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango**

**Mradi Na. 2229: Enhancement of Institutional Capacity and Research** ambao ulitengewa **Sh. 8,000,000,000.00,** ambapo hadi Kufikia Februari 2025 Miradi huu ulipokea Jumla ya **Sh. 300,070,000.00** sawa na **asilimia 3.75** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

**2.4 *Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais*,**

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2024/25.

**2.5 *Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara na taasisi zilizo chini ya ofisi hii ziliidhinishiwa jumla ya **Sh 21,288,757,238.00**kwa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 4**

**JEDWALI NA. 4: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 |
|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **NA. 6251** Programu ya maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma | 1,289,658,000.00 |
| **Fungu 11** – Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji | **NA. 4429** Institutional Support<br>**NA 4933** Export Processing Zone Development<br>**NA 4920** Tanzania Mini Tiger Plan 2020<br>**NA. 4901** Implementation of BEST Programme | 1,896,549,000.00<br>5,410,226,000.00<br>1,314,506,000.00<br>3,406,726,000.00 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity and Research<br>**NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity and Research | 8,000,000,000<br>415,380,000 |
| **JUMLA KUU** | | **21,288,757,238.00** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilitembelea mradi mmoja kati ya Miradi saba (7) inayotekelezwa na Ofisi hii kwa kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na kuchambua utekelezaji wa mradi huo kama ifuatavyo:-

**Mradi Na. 4933:** Ujenzi wa Ofisi ya Kanda maalumu ya Kiuchumi ya Benjamini Mkapa-Benjamin Mkapa Special Economic Zone, Dar Es salaam.

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu unahusu ujenzi wa Uzio ambao unatenganisha eneo la viwanda na eneo la kupooza umeme na ukarabati wa mifereji ya maji ya Mvua katika ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa **Benjamin William Mkapa (BWM Special Economic Zone).**

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu ulipokea pesa kiasi cha **Shilingi 149,900,530** mnamo mwezi **Disemba 2023** na ulianza kutekelezwa kuanzia **19 Februari 2024** na ulikamilika **Agosti 2024** na kukabidhwa kwa Serikali tarehe **20 Novemba 2024.**Aidha Kamati ilielezwa

kwamba mradi huu ulitekelzwa kwa kutumia utaratibu wa **FORCE ACCOUNT.**

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile Kamatii ilitembelea baadhi ya wawekezaji ambao wanasimamiwa na Mamlaka ya Uwekezaji wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi waliopo katika eno hilo la **Benjamin Mkapa Special Ecomnomic zone** ambao walionesha kufurahishwa na usimamizi wa Wizara kwao kama wawekezaji. Aidha walikua na maombi kwa Serikali kushirikiana na Taasisi za kifedha kuwa na dirisha la kutoa mikopo kwa wamiliki wa viwanda ya kuongeza thamani ya bidhaa zao ilikuweza kushindana na bei ya soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha Kamati inampongeza **Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa namna ambavyo anaendelea kufungua milango kwa wawekezaji nchini na kutafuta fursa kwa wawekezaji wazawa, hali hii inadhihirisha namna ambavyo Serikali ya awamu ya Sita imedhamiria kukuza Sekta ya uwekezaji nchini.

### 2.6 *Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### *3.1* ***Maduhuli***

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 1,566,260,545,635.00** ikilinganishwa na **Sh. 1,168,543,413,000.00** katika Mwaka wa Fedha **2024/2025** kama

ambavyo imeainishwa katika **Jedwali Na. 5**. Hii ni na sawa na ongezeko la **asilimia 25.4** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha unaoisha.

**JEDWALI NA. 5: Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 |
|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,168,543,413,000.00 | **1,566,260,545,635.0** |
| **JUMLA KUU** | **1,168,543,413,000.00** | **1,566,260,545,635.00** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hilo la makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha **2024/2025** litatokana na uimarishaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya Msajili wa Hazina ambayo itaongeza usahihi wa takwimu za upatikanaji wa mapato na mashirika ambayo serikali ina hisa au kutegemea kupata gawio na kurahisisha utoaji taarifa na ufatiliaji wa mapato na matumizi ya Mashirika.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 122,122,585,000** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 22,525,101,000**ni mishahara, na **Sh. 99,597,584,000**ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6.**

**JEDWALI NA. 6: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026**
***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 8,662,948,000.00 | 51,922,183,000.00 | 60,585,131,000.00 |
| **Fungu 11**– Ofisi Rais Mipango na Uwekezaji | 8,716,784,000.00 | 13,675,401,000.00 | 22,392,185,000.00 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | 5,145,369,000.00 | 34,000,000,000.00 | 39,145,369,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **22,525,101,000** | **99,597,584,000** | **122,122,585,000** |

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepungua kwa kiasi cha **Sh. 59,591,622,325** sawa na **asilimia 33** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 181,714,207,325 ikiwa na baada ya ongezeko la kiasi** cha Shilingi **115,513,345,325.00** ambayo ilitoka Wizara ya fedha na iliwasilishwa kwa Mamlaka ya Ngorongoro kwa jili ya kutekeleza zoezi la uhamisho wa wananchi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### *3.3* **Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 26,507,276,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 14,553,437,000.00** ni fedha za ndani, na **Sh. 11,953,839,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Sh. 5,218,518,762.00** sawa na **asilimia 19.6** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya kuongezeka kwa bajeti kumechangiwa na mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba kuna maendeleo endelevu kwa watanzania wote kwa kuhimiza mipango madhubuti na Uwekezaji nchini. Kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 7.**

**JEDWALI NA. 7: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2025/2026**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **NA. 6251** Programu ya maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma | 370,691,000 | 1,300,000,000 |
| **Fungu 11**– Ofisi ya Rais,Mipango na Uwekezaji | **NA 4901** Implementation of BEST Programme<br>**NA. 4904** Financial Access for sustainable and Transformationa;(FAST) Growth Project<br>**NA 4920** Tanzania Mini Tiger Plan 2020<br>**NA 4933** Export Processing Zone Development<br>**NA.**6251 Public Finance Management Reform Programme (PERMP)<br>**NA.**6260 Institutional Support | 2,747,906,800<br>788,703,600<br>6,582,881,000 | 5,372,130,823<br>2,420,431,177<br>1,062,102,000 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity | 7,566,093,328<br>433,906,672 | 0<br>779,074,600 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | and Research<br>**NA 6251** PFMRP VI<br>**NA 6526** National Population Project | | 582,202,400 |
| **Jumla Ndogo** | | **14,553,437,000** | **11,953,839,00** |
| **JUMLA KUU** | | **26,507,276,000.00** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza Miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani, Aidha Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha kwamba Fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya Utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinapatikana kwa wakati, zinatekeleza miradi iliyopangwa kutekelezwa ili kuweza kuleta tija na ustawi wa wananchi kwa ujumla.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### *4.1* ***Maoni ya Jumla***

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa ofisi kujiwekekea malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

### ***4.2 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina***

(i) Kukokuwa na Uwekezaji wa kimkakati katika masoko ya Hisa na Taasisi Binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa, Serikali itakosa gawio ambalo linaweza kutumika kwa maendeleo ya Nchi;

(ii) Mali zilizorejeshwa serikalini zisipofanyiwa tathimini zinasabishia Serikali upotevu wa fedha kwa kushindwa kujua thamani halisi ya mali hizo;

(iii) Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokuwa na usimamizi Madhubuti wa mashirika ya Umma kunachangia kukosekana kwa gawio kwa serikali na kupunguza mapato ambayo yangeingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(iv) Kutokuwepo kwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake hupelekea kuonekana kuwa hakuna tathmini ya kutosha juu ya vyanzo hivyo vya ukusanyaji wa maduhuli; na

(v) Madeni yanayotokana na ubinafsishaji wa mali za Serikali ili kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato hayatakuwa na tija kwa Taifa kama Msajili wa Hazina hatoboresha njia bora ya kusimamia ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo hivyo.

### *4.3 Fungu 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji*

(i) Kutokuwepo kwa usimamizi thabiti wa Kanda Maalumu za Kiuchumi kunapelekea uanzishwaji wa kanda hizo kutokuwa na tija iliyokusudiwa kwa Taifa; na

(ii) Changamoto ya elimu ya kutosha ya uwekezaji na fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi, inapelekea wadau hao kuwekeza katika maeneo na Miradi ambayo si ya kimkakati kwa Taifa.

### *4.4 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu*

#### 4.4.1 Fungu 66 – Tume ya Mipango

(i) Serikali ihakikishe inaandaa nyenzo bora za Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050 ili kuweza kulata Tija kwa wananchi;

(ii) Serikali ihakikishe ushiriki wa Sekta binafsi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo nchini; na

(iii) Serikali ifanye tathmini na kuhusu miradi ya Kimkakati inayotekelezwa na inayotarajiwa kutekelezwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inaleta Tija kwa wananchi na Taifa.

### 4.4.2 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

i. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaendelea na Uwekezaji katika masoko ya Hisa na Taasisi Binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa;

ii. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe inafanya tathmini ya mali zilizorejeshwa serikalini, kuziendeleza ili ziweze kuongeza mapato kwa Serikali.

iii. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia uwekezaji wa umma ili kuongeza mchango wa Taasisi na Mashirika hayo katika kuchangia katika Mfuko Mkuubwa Serikali ili kukuza pato la serikali na Taifa kwa ujumla.

iv. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake; na

v. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaboresha vyanzo vingine vya mapato ikiwemo madeni yanayotokana na ubinafsishaji wa mali za Serikali ili kuboresha na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

### 4.4.3 FUNGU NA 011- *Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji*

i. Serikali kusimamia uwekezaji wa kanda maalumu za kiuchumi ili kuleta tija kwa Taifa; na

ii. Serikali iendelee kutoa elimu ya Uwekezaji na fursa za Uwekezaji kwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika Kanda maalumu ya kiuchumi na miradi ya Kimkakati ya Taifa.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb.
22. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb

**24 APRILI, 2025**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambae pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, (Mb) –Waziri Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Mhe. Stanslaus Haroun Nyongo, (Mb)- Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Uwekezaji kwa ushirikiano ambao wameendelela kutoa kwa Kamati kwa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida, Ndg. Fred Matola Msemwa – Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na Ndg. Nehemiah Kyando Mchechu - Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
24 Aprili, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare, Mjumbe Mwandamizi wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kusoma taarifa yako kwa ufasaha mkubwa sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Yahaya Massare. Aidha, ninamshukuru pia Mheshimiwa Waziri, ambaye amehitimisha hotuba yake kabla ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge tutakuwa na uchangiaji kama ilivyo kawaida yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatia Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursaa hii ya kutoa mchango wangu. Mwaka 1967 marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema: "Taifa letu linatumia zaidi ya 20% ya Bajeti ya Taifa katika Sekta ya Elimu." Kwa muktadha huo basi sisi kama Taifa tunapaswa kutathmini ubora wa elimu na kama elimu hiyo tunayoitoa kwa vijana wetu inakidhi mahitaji ya Taifa letu. Kwa mawazo yangu, tathmini hiyo ya mwaka 1967 pengine leo baada ya miaka 58 ina uzito mkubwa zaidi kwetu kama ilivyokuwa huko nyuma. Ninalisema hili kwa sababu tunatumia takribani shilingi milioni 800 kwa mikopo ya elimu ya juu, tunapaswa kutathmini je, elimu inakidhi mahitaji ya soko la ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja mwenye busara aliwahi kusema, mataifa ambayo yanategemea rasilimali zilizopo juu ya ardhi, uchumi wake utazidi kuimarika kadiri siku zinavyokwenda. Kwa nini alisema hivyo? Alisema hivyo kwa sababu akili, ujuzi na maarifa ya watu yanaongezeka kila kukicha tofauti na rasilimali zilizopo chini ya ardhi siku moja zitamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hayo niliyoyasema ili kuonesha ni kwa kiasi gani elimu hasa elimu iliyobora inaweza kulisaidia Taifa kujenga maendeleo endelevu na ustawi kwa ujumla wake. Bila ya kuwekeza kwenye sekta ya elimu na bila ya kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata elimu inayokuza weledi, ujuzi na umahiri wao, hasa vijana wanaohitimu vyuo vikuu, bila shaka tutaendelea kuwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mzazi na kama Mtanzania, ninapotathmini elimu ya vyuo vikuu ninabaini kama kuna kasoro mahali fulani na nitazisema. Vyuo vikuu ni mahali ambapo tunategemea kutakuwa na mijadala ya kisomi inayojadili masuala ya uchumi na utafiti wa kisayansi, wale ambao tunakumbuka vizuri ukumbi wa Nkrumah Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnaweza kukubaliana na mimi kwamba utamaduni wa kujadili hoja nzito na ajenda za kitaifa unazidi kupungua kadri siku zinavyokwenda. Sababu ya kuanguka kwa kiwango cha elimu kwangu ninaiona ni moja tu, mbinu zinazotumika katika kuwasomesha vijana wa chuo kikuu zimepitwa na wakati. Hivi sasa mkazo mkubwa zaidi unawekwa katika kufaulu mitihani na kukariri badala ya kutoa maarifa na ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu tunatakiwa kufanya mambo manne ili tuimarishe umahiri wa vijana wetu na haya hayahitaji fedha. La kwanza, badala ya kuwapa wanafunzi wa vyuo vikuu mitihani ya kuchagua majibu, tungewapa wanafunzi wa chuo kikuu wajibu mitihani kwa kutumia vitabu *(open book exams)* na jambo hili siyo jipya, wanasheria na mahakimu wanatumia wanapoamua kesi wanakusanya vitabu vya aina mbalimbali. Madaktari wanapoamua kesi za utabibu ngumu, wanakusanya majarida ya kitaaluma ambayo, kwa nini wanafunzi tuwalazimishe kukariri badala ya kutumia vitabu? Mimi sioni mantiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tuwape kazi maalum, *project* nyingi kadri inavyowezekana, wanafunzi wa chuo kikuu wanatakiwa kutengeneza mawazo na fikra. La tatu, tuwape kazi za kufanya uchambuzi na mapitio ya vitabu mbalimbali wanavyosoma; na nne, tuwape kazi maalum za mawasilisho darasani. Nina uhakika tukiyafanya hayo tutatoka hapa tulipo. Karne ya 21 haihitaji watu wenye shahada nyingi za vyuo vikuu, tunahitaji ujuzi na maarifa ya watu. Watu wenye ujuzi na maarifa ya kufanya kazi, ndiyo maana miaka minne iliyopita Serikali ya China ilibadilisha vyuo vikuu 600 kuwa vyuo vya ufundi na ufundi stadi kwa ajili ya muktadha huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Marekani, Rais mpya Trump mwaka jana alisema anataka kuanzisha chuo kikuu cha ujuzi na mafunzo ya kazi badala ya *degree* za jumlajumla. Mjasiriamali maarufu duniani Elon Musk mwaka jana alisema anataka kuanzisha Chuo Kikuu cha Teknolojia na Sayansi badala ya kuwa na vyuo vikuu vya jumlajumla. Sasa Waingereza wana msemo maarufu wanasema hivi: "*if gold rusts, what will iron do*?" Kama dhahabu inaota kutu, bati na chuma vitakuwaje? Ninataka kusema nini, ninachotaka kusema hapa kama China na Marekani wameiona kasoro, kwa nini Watanzania hatutaki kuiona kasoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pale tunapolazimika kutoa shahada za chuo kikuu, kwa nini hatuangalii *courses* ambazo zina uwezo wa kuwaajiri vijana na kutengeneza ajira na kushindana na wengine duniani? Nitatoa mfano, hivi katika karne hii tunafundisha kweli historia ya dunia, badala ya kufundisha *political science* ambayo inajumuisha falsafa, historia na saikolojia. Tunafundisha historia kweli? Tunaandaa watu wa Taifa la namna gani? Tunasomesha manunuzi badala ya kufundisha ujasiriamali na *agribusiness*, tunaandaa Taifa la namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafundisha vijana sosholojia badala ya kufundisha *practical psychology* au saikolojia ambayo inatumika katika kila nyanja, tunafundisha sosholojia kweli? Tunafundisha Sarufi ya Kingereza na Kiswahili badala ya kufundisha matumizi ya lugha katika muktadha maalum *(applied linguistics and languages)* tunafundisha kweli sarufi katika karne hii? Tunafundisha fasihi badala ya kufundisha vijana wetu uandishi wa ubunifu *(creative writing)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano hii bila shaka Waheshimiwa ipo mingi sana na sitaimaliza, lakini nimeona niseme mifano michache, tuangalie tu kwamba hali yetu ya elimu ya chuo kikuu haipo vizuri sana. Mwaka jana tulifanya mageuzi hapa ya Sera ya Elimu na Mitaala, lakini sisi viongozi tupo kimya juu ya elimu ya chuo kikuu kana kwamba shwari, mambo si shwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilikuwa naangalia kwenye *YouTube* na kuangalia mijadala ya wanafunzi wa chuo

kikuu juu ya kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba wanafunzi wa vyuo vikuu waende elimu ya *VETA*. Wakawa wanajadili, inaonekana kwamba 95% hawakuridhika na kauli hiyo kama. Sasa ushauri wangu, ninasema kuna jambo la kufanya, elimu yetu haiwezi kuwafanya vijana wakashindana na vijana, hata ukichukua mfano tu wa nchi zinazotuzunguka Afrika Mashariki, ukimchukua kijana ambaye amesoma Shahada ya Kiswahili sisemi Kiingereza waweke kwenye mjadala wa dakika 10 ni mahusiano ya ardhi na mbingu. Hii inadhihirisha kwamba elimu yetu mahali fulani ina kasoro na sisi kama viongozi tusikae kimya, tuseme na kama nilivyosema, lakini tuseme na tutoe mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tu ya msingi, nimetoa mapendekezo ya mambo manne, hayahitaji fedha, hayahitaji teknolojia, yanahitaji tu maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu udahili wa wanafunzi wa vyuo vikuu. Vyuo vikuu vinavyofanya udahili wa wanafunzi ninashangaa sana hawaangalii umahiri, weledi, ujuzi na vipaji vya wanafunzi badala yake wanaangalia ufaulu wa kidato cha sita. Nitatoa mifano miwili ili mnielewe; mwanafunzi aliyehitimu kidato cha nne, akaamua kwenda kujiendeleza katika kiwango cha diploma, akafaulu diploma ya miaka mitatu ya Sayansi ya Tiba na Utibabu ya miaka mitatu na amefanya kazi ya uganga msaidizi kwa muda wa miaka minne, anapotaka kwenda chuo kikuu anaulizwa cheti cha kidato cha sita kipo wapi? Tena cheti chanyewe cha ufaulu wa masomo matatu ambayo ni ya kukariri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninauliza tu hii ni elimu gani? Tunatafuta nini? Nilidhani kazi ya elimu ni kukuza vipaji na umahiri wa watu, ndiyo nilidhani kazi ya elimu hiyo. Kumbe kazi ya elimu tunayoifanya ni kukusanya watu wenye ufaulu. Ninadhani si sawa, sisi kama viongozi si sawa. Mfano wa pili, kijana amemaliza kidato cha nne amekwenda kusoma diploma ya miaka mitatu ya sheria ya miaka mitatu na amefanya kazi ya miaka mitano kwenye jamii ya huduma za sheria, anapoomba nafasi ya chuo kikuu anaambiwa cheti cha kidato cha sita kipo wapi? Halafu anachukuliwa kijana ambaye ana ufaulu wa masomo matatu

katika daraja la C. Haya mimi nauliza tu hii elimu ni elimu inataka kutibu nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kama tuna wasiwasi na watu wenye elimu ya kujiendeleza wenyewe, vyuo vikuu maarufu duniani vinatumia njia tatu tu: ya kwanza, Wamarekani wana mtihani unaitwa *standard aptitude test*, unapima weledi wa mwanafunzi. Jambo la pili, kuna vyuo vinatumia mtihani maalum wa kukuza weledi ambao wanaita *foundation program* na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatumia utaratibu huo, kwa nini *conventional university* hazitumii? Mimi sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, vyuo vikuu maarufu duniani vinatumia *pre university program*, kwa nini vyuo vikuu vya Tanzania havitaki kutumia *pre university program*? Sasa tunataka kutengeneza watu kwa ajili ya kazi gani? Nilidhani kazi ya elimu ni kukuza vipawa vya watu, umahiri wa watu, ujuzi wa watu badala ya kuwakusanya watu waliofaulu kidato cha sita. Kwanza, faida yake ukimchukua kijana mwenye diploma, anapokwenda chuo kikuu anajua anatakiwa kusoma nini, kwa nini asome hiyo *course*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi wa *form six!* Ati mimi ninashangaa, *form six* tunamfundisha Kiswahili, Kiingereza na Historia, asome sheria. Sasa mimi ninajiuliza tu uhusiano wa Kiswahili na Kiingereza kwenye sheria uko wapi? *I don't see the connection;* mimi ninataka kuwa daktari, unanifunidisha *physics, chemistry* na *biology,* uhusiano wa *physics, chemistry, biology* na utabibu uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma Diploma ya *Clinical Medicine* uhusiano ninauona moja kwa moja. Ninapokwenda chuo kikuu ninasoma kwa umahiri, kwa uweledi na ninajua ninachokwenda kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wamemaliza Shahada ya Udaktari, baadaye baada ya kumaliza miaka mitano anakwenda kufuga kuku. Sasa ninajiuliza, kwa nini hakwenda Chuo Kikuu cha Sokoine akasome ufugaji? Wapo watu wanasoma uhandisi baada ya miaka mitano wanafanya boda

boda, sasa mimi ninasema kwa nini hakwenda kusoma *VETA* ufundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaonesha tu viongozi wenzangu tusikae kimya tukadhani kwamba, mambo ni mazuri kiasi hiki tuna kazi ya kufanya. Tumefanya kazi nzuri sana kwa sera ya elimu, kwa ajili ya elimu ya sekondari na *primary,* mbona hatuna sera maalum, kwa ajili ya elimu ya vyuo vikuu? Ninadhani wakati umefika wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa mchango wako unaofikirisha sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na uchangiaji. Ninamuita sasa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza. Mheshimiwa *Eng*. Stella Martin Manyanya, ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Nimpongeze mchangiaji aliyemaliza, Mheshimiwa Nahodha, kwa *contribution* yake kubwa sana wakati anazungumza kwamba, *Lawyers* wanatumia *open book exam* na sitaki kuingilia *field* nyingine, lakini ninataka ku-*share* naye tu, kama kum-*support* kwamba, *Lawyers* wanatumia *open book exam* kwa sababu, kwanza ina-*stimulate professional practice* na ina-*assess high order skills,* ina-*encourage Lawyers* wa-*apply* zile *principles*. Kwa hiyo, siyo *necessarily* ku-*recall fact,* lakini ni ku-*test mind in a more practical way.* Sasa sijui kama inaweza ika-*apply* maeneo mengine, *but I think is the good contribution. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha Tume hii ya Mipango. Tume ya Mipango, hapa katikati, ni kama ili ilisimama hivi, lakini kutokana na umuhimu wa uwekezaji na hakuna Taifa linaweza kukaa kuzungumza habari ya mipango bila kuwa na Tume ambayo ndio *think tank* wetu, ambao wanatuambia mambo ya kiuchumi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo,

Katibu Mkuu na timu yenu nzima, wamepata heshima nyingine mpya kwa nchi yetu ya kuja na mipango ya nchi yetu, mipango ya miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tume hii ilivyoanzishwa, Tume ya Mipango mpya, ukiangalia Sheria mpya ya Tume ya Mipango imeongeza kazi nyingi sana ukilinganisha na sheria zilizopita, imeweka nguvu zaidi kuliko sheria iliyopita na imeongeza majukumu zaidi, kusisitiza tu umuhimu wa Tume ya Mipango ya Taifa kwa Taifa letu. Tunachotarajia kutoka kwenu, kwa sababu, uchumi sasa duniani ni kitu ambacho kinayumba, tunaona sera za wenzetu, sasa kuwa na Tume hii ambayo kazi yake mojawapo, ni kubuni na kuboresha vyanzo vipya vya mapato na kusimamia uwekezaji wa mitaji ya umma iweze kuongeza pato la Taifa, lakini iweze kuwa na tija kwa nchi yetu. Siyo kazi ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana, ninajua hii *thinking* ni *controversial* kwa Tanzania siku hizi, lakini *I am a strong believer* kwamba, Mwalimu Nyerere Mwaka 1995 alisema hivi, ninanukuu, "*there is no way in which we can begin to deal with the problems of Africa without leadership and without commitment. If you go to Asia one thing that strikes you is the commitment of state, the development. You see it in Japan that commitment of the Government of Japan to development. Even now they are developed country but there is tremendous commitment by the state to development*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ndiyo *controversial* ambayo *I support it, by the way, don't listen to that non sense that the state should give up the direction of the economy, it is non sensical.* Nani ameacha? *Who has done it?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Japanese have not done it, the British have done it and the Germans have not done it*. Tunasisitiza habari ya uwekezaji wa mitaji ya umma, kuna watu wanafikiri Serikali isijihusishe na biashara, kazi yake ni ku-*regulate,* lakini mimi ninakubaliana na Mwalimu Nyerere, *we should not leave the direction of the economy*. Haiwezekani, *of course* ku-*regulate* ni kazi mojawapo na ni *function* ya tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotakiwa kufanya kwa mabadiliko ya sasa ni lazima tuendane na *economy* mpya sasa. Miaka ya 1995, 1970, miaka ya huko nyuma zaidi, mambo yamebadilika, tunapoamua kufanya biashara ni lazima tuendane na *principle* za biashara. *Handoff,* lazima mashirika haya yaongozwe kibiashara na lazima ziwe *autonomous.* Lazima zi-*appreciate* ku-*promote skills* na kuwaruhusu hawa waweze kuajiri watu ambao ni *sharp.* Isifuate ile *traditional way* ya ajira kwa sababu, tunafanya biashara tunawekeza mitaji ya nchi na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima timu ambayo itafanya kazi kwenye mashirika haya ya umma tukiamua kufanya biashara wawe ni *very exceptional.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Kitila, tunachotarajia kwa tume mpya Msajili wa Hazina mnapofanya kazi na mashirika haya ya umma siyo tu kushauri, wawekeze mitaji kwenye maeneo maalum na lazima wawe na *autonomous* fulani, ili waweze kufanya biashara. Msiwaingilie, mkiwaingilia ni *contradiction* tukiamua kufanya biashara. Mkiwaingilia mnavuruga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma kitabu cha marehemu Shirima, aliyeanzisha *Precision Air,* akielezea *frustration* zake alivyokuwa kwenye *industry* ya *airline*. *Initially* alifanya *East Africa* baadaye ilivyo-*collapse* akaja kwetu, akaambiwa aanzishe shirika la ndege, lakini *frustration* za mwingiliano zilimfanya a-*quite* na akaanzisha *airline* yake; ame-*share* kila kitu kwenye kitabu, *Frustration. In fact,* hata Bunge, Kamati za Bunge anasema zinakuja, ninatoa tu *order* fulani, ndege imejaa, halafu wanamwambia eti washushe abiria wakawachukue Mawaziri sijui wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tukubaliane biashara inahitaji nidhamu. Tuamue kufanya biashara tufanye biashara, mambo mengine wafanye kwa namna nyingine, lakini waki-*contradict* hatutaweza kufanya biashara ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa kazi nyingine ya Tume hii kwa mujibu wa sheria ni kushirikisha *private sector,* siyo tu kwenye mipango, kwenye mikakati yote kwa sababu,

tunakubaliana hapa *capacity* ya Serikali kuajiri ni ndogo sana. *Hardly, we are talking about one million* hawezi, lakini wanaoajiri ni hawa. Kwa hiyo, tukiweka mazingira yawe mazuri, tuka-*regulate* na tukaweka mazingira mazuri wafanyabiashara hawa ndiyo wanaleta kodi, ndiyo wanaleta ajira, wanaleta ubunifu, wanaleta mitaji na wanaleta fedha za kigeni. Kwa hiyo, *private sector* ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Kitila, wakati wapo kwenye kukusanya maoni ya dira uli-*witness* sana *contribution* ya *private sector,* wakati wanakusanya maoni, *very brilliant,* ni watu ambao wapo *filed,* siyo tu wana *knowledge,* lakini wako na *practice* hiyo. Kwa hiyo, kuendeleza *private sector in that sense* na kukaribisha mijadala ya pamoja ninadhani tutajenga Taifa ambalo ni zuri kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza, aah. Kwa hiyo, kazi nyingine ya tume hii kwa mujibu wa sheria…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kisau, ni kengele ya pili, lakini ninakuongezea dakika mbili.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, Mwenyekiti wangu wa Kamati. Kazi nyingine kwa mujibu wa sheria, Mheshimiwa Profesa Kitila, ni Tume kutoa mwongozo wa nchi yetu tushirikiane na nani kiuchumi kati ya nchi yetu na nchi nyingine na mashirika mengine ya kitaifa. Hii kazi siyo rahisi sana kwa sababu, *policy* za dunia sasa zinapindukapinduka kila wakati. Kwa hiyo, *you need a team* ambayo ni *sharp,* ambayo inaweza kutushauri. Kwa hiyo, kazi ya Tume hii ni muhimu mno na mzigo sasa upo kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria *this time* imewapa mamlaka makubwa sana kwamba, ninyi leo ile tume ni kama *quasi-judicial body,* wanaweza waka-*summon* sera za Wizara nyingine wakaweka *online* na nyingine wakakataa. Kwa sababu, dira tunayotengeneza ya miaka mitano ni lazima tuwe na *discipline* ya

kumaliza vizuri bila *interruption* na kutengeneza *coordination,* ambayo ni *well-coordinated. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashukuru sana kwa dakika hizi, tunawatakia kila la heri. Hii timu ina kazi kubwa sana, lakini mradi ule wa ku-*promote* mashamba na wafanyabiashara wadogo na kuwa-*link* na watu, wawekezaji, ni mradi ambao ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mkurugenzi wa *TIC,* alituma watu Kiteto. Tunataka Watanzania wenye mashamba yao, lakini hawana mitaji wapate fursa hizi za kukutana na wawekezaji kufanya *partnership,* ili waweze kuajiri wenzao. Baada ya kusema hayo tuwapitishie bajeti hawa wakafanye hiyo kazi muhimu sana kwa Taifa. Ahsanteni sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita kwa mchango wako. Tunaye Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng*. Stella Martin Manyanya na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, ajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi nami niweke mchango wangu kwenye bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Kitila, Naibu Waziri na Viongozi wote wa Wizara na Watumishi wa Wizara na vituo mbalimbali chini ya Wizara ambavyo vinafanya kazi nzuri sana ya mipango ya maendeleo katika nchi yetu kutuletea uchumi bora, hongereni sana. Wanafanya kazi kubwa ya kukuza uchumi, wanapanga mipango mizuri na hivyo, nchi yetu inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ingawa tunakwenda vizuri, lakini ninataka nizungumzie viwanda kwa sababu, ndiyo jukwaa la maendeleo. Ukitaka maendeleo lazima upanue viwanda, viwe vingi na vizalishe vizuri. Nchi ambazo zimeendelea, Ulaya yote, Amerika yote na hasa Kaskazini, Japan, wamesema hapa na nchi nyingine za Asia zinakuja vizuri ni viwanda vinakuwa imara.

Viwanda vinakuwa vingi, vinaongeza ajira, vinaongeza mapato na kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa kwetu kwenye viwanda bado tupo nyuma sana na ndio maana hatujaweza kwenda mbali sana, hata kama tunakwenda vizuri. Sasa Mheshimiwa Waziri ameeleza miradi mingi hapa, hasa ya viwanda maeneo mbalimbali ya nchi, lakini ninafikiri tuna nafasi kubwa sana ya kufanya vizuri zaidi miradi hiyo iwe mingi mara dufu, hata mara kumi, hata mara mia, ili tuongeze ufanisi wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna uwezekano mkubwa wa kufanya hivyo. Viwanda ambavyo vipo Tanzania, amevisema Waziri hapa, karibu 100% ni vya kutoka nje, ni vya wawekezaji kutoka nje, *foreign direct investment*. Tunaona viwanda pale Mkuranga, vingi vidogo pale, upande huu wa Pwani, Kibaha na mpaka Chalinze huku, tunaviona viwanda. Karibu vyote ni vya wageni kutoka China, kutoka wapi, ndio wanaowekeza hapa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikri kwamba, hii ni nzuri kidogo siyo nzuri sana. Tunahitaji uwekezaji wa wazawa, Watanzania wazawa ndio wawekeze kwenye viwanda hivi na tuweze kupiga hatua kubwa, uwezekano huo upo ninarudia kusema. Leo Watanzania wenzetu wanazo hela nyingi kidogo, wanazo. Ndiyo maana ukiangalia kwenye *income per capita,* ile *PPP (Purchasing Power Parity)* tupo kwenye shilingi 10,000,000 *per person*. Shilingi 10,000,000 kwa mtu na zaidi kidogo ile nyingine *ya income per se*, *per capital per se,* ni kwenye shilingi 3,000,000 au shilingi 2,000,000 ila ile kwenye *PPP* tupo kwenye shilingi milioni 10. Hiyo ina maana kwamba, kuna watu ambao wana hela nyingi sana ndani ya nchi hii, wafanyabiashara wakubwa na wengine ambao wana hela nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna mifano ipo mizuri, angalia watu wanajenga majumba ya kifahari ya kuishi. Jumba la shilingi 2,000,000,000, shilingi 3,000,000,000 jumba moja au watu wanajenga hoteli kubwa nzuri za kifahari za nyota tano, wanatumia shilingi 1,000,000,000, shilingi 2,000,000,000 kujenga hoteli au mtu anajenga kituo cha mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa kuna siku nilihesabu kutoka Chalinze hadi Kibaha vituo vya mafuta 86, mwaka juzi ninafikiri, kilometa kama 70 au 60 hivi vituo 86. Angalia pikipiki na bodaboda za kubeba abiria mjini humu, Dar es Salaam na miji mingine yote hii zilivyo nyingi. Sasa ni kwa sababu, watu hawana pa kuwekeza kwenye maeneo mengine, anaamua awekeze kwenye huduma hizi za hoteli, bodaboda, nyumba za kuishi, shule na baa. Hawana pa kuwekeza, hawajui wawekeze wapi kwenye maeneo mengine, anawekeza kwenye huduma za usafiri, za kulala, za nini? Ni huduma si mbaya, lakini hazizalishi kwa maana ya kuleta viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajaji moja nimeuliza hapa, nikaambiwa sasahivi ni kwenye shilingi milioni 10 kuinunua. Kujenga sheli moja, kituo cha mafuta kimoja, kwa wastani labda ni shilingi 2,000,000,000 tuseme, kwa chini sana shilingi 1,000,000,000. Kujenga hoteli nzuri ni shilingi 2,000,000,000, shilingi 3,000,000,000, kwa chini sana shilingi 1,000,000,000 na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukichukua watu 50 waliowekeza kwenye sheli hizo, ina maana ni shilingi bilioni 50. Ukichukua watu 60 waliowekeza kwenye hoteli ni shilingi bilioni 60 kwa uchache kwa chini. Shilingi bilioni 60 ni kiwanda cha kutengeneza *TV,* cha kutengeneza pikipiki, ni kiwanda kikubwa. Shilingi bilioni 50 za wale watu wa sheli ni kiwanda cha kutengeneza matairi ya pikipiki, matairi ya magari na vitu vingine vikubwa vikubwa. Wenye bajaji 100 ni kiwanda cha kutengeneza *furniture,* samani kama hizi za ndani humu, meza nzuri, makabati, kwa kiwango cha hali ya juu sana, lakini tunawekeza kwenye hiyo huduma ya usafiri wa bajaji na pikipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo nchi yetu hii tuna soko kubwa sana la Kimataifa la nje ya nchi yetu. Pale Kariakoo ni Soko la Kimataifa, tuna wanunuaji kutoka nchi jirani; Malawi, Zambia, Zimbabwe, Kongo *DRC*, Burundi, Rwanda, Uganda, Msumbiji ambayo ina Bahari, lakini wanakuja kununua Kariakoo, Kenya na wengine, soko kubwa sana la bidhaa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa hizi zinazouzwa pale Kariakoo ni zile ambazo na sisi tumenunua nje huko Dubai, Japan na kwingineko ambazo ni nguo na vipodozi, ndiyo tunanunua pale ambavyo siyo vya kwetu, tumenunua nje, tumekuja kuuza hapa. Kwa hiyo, kimsingi sisi ni wachuuzi tu, tunanunua nje, tunauza, hatuna uzalishaji wowote. Tungekuwa na viwanda vya ndani vya kwetu, tungeuza bidhaa za kwetu, tungepata fedha na tungepata mtaji na tija kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mfano nichukulie bajaji 100 ambazo ukifanya hesabu ni shilingi bilioni moja kuzinunua. Hiyo shilingi bilioni moja ni mtaji wa kiwanda cha kutengeneza kama nilivyosema *furniture* nzuri au wangeamua kuiweka kwenye kuongeza thamani ya mazao tuseme mahindi, ni kiwanda kikubwa cha kuzalisha unga mzuri *grade one*, safi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kiwanda kama hicho kinaweza kuajiri watu zaidi ya 1,000. Wakulima wa mahindi wana soko la uhakika pale kiwandani, na wasafirishaji wa kupeleka mahindi kwenye kiwanda watapeleka kwa uhakika na kuuza hapo. Wafanyakazi pale kiwandani wa kwenda kuchuuza kwenye kuuza maduka huko ndani na nje, hawapungui 1,000 kwa kiwanda cha shilingi bilioni moja ambacho badala yake, kama ni bajaji ni wale watu mia tu wanaoziendesha, lakini kama ingekuwa ni kiwanda cha kuongeza thamani kwenye unga, tungepata zaidi ya wafanyakazi 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kiwanda hiki cha kuzalisha unga bora kitalipa kodi nyingi sana. Kwanza mahindi yale yakiuzwa pale kiwandani watalipa kodi *direct* au *indirect way;* watalipa kodi kwenye kuuza mahindi pale. Katika kusafirisha, wale wanaopeleka mahindi na kuyatoa pale na kuyapeleka dukani (unga) watalipa kodi. Wafanyakazi walioajiriwa pale watalipa kodi ya mapato *(Pay As You Earn)* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, badala ya kutumia shilingi bilioni moja kununua bajaji 100, ukiongeza kwenye kiwanda cha unga utapata tija kubwa sana ya wafanyakazi 1,000 na kodi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hizo bajaji zinalipa kodi shilingi ngapi ukilinganisha na hicho kiwanda cha kuboresha unga? Hii yote ninayoisema, ninaisema kwa sababu hii Wizara ndiyo ya kutuokoa ili iweze kuwa katika vitendo na kuwa na viwanda vingi. Wana kituo cha uwekezaji, kinaratibu wawekezaji wa nje, zaidi ni wa nje tu. Kwa nini kisianzishe idara, ama kituo chenyewe, au chini Wizara huku kwenye Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuwe na idara ya kuratibu hawa ambao wana hela za ndani za kununua bajaji, kujenga hoteli, badala ya kufanya hivyo, wawaratibu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia moja ambayo mimi napendekeza chini ya Wizara hii, au Ofisi hii, wafanye viwanda kwenye makaratasi, wafanye upembuzi yakinifu *(feasibility study)*. Kwa mfano, kiwanda cha mahindi, cha unga kwamba hapa kuna *raw material* ya mahindi, kuna wafanyakazi *(staff)* na watu wengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nimalizie. Sasa wakitengeneza kwenye makaratasi kwamba hiki kinafaa kiwepo hapa, mtaji wake shilingi fulani, wakitengenezee kampuni halafu watangaze sasa tununue *share* kama tunavyonunua za *Tanzania Breweries*, au *Tanzania Oxygen*. Hatujui wanafanya nini kule. Tunanunua *share*, tununue *share* kwenye viwanda hivi ambavyo tunataka vianzishwe kwa mpango huo chini ya Wizara hii na nchi ipate tija ya viwanda kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, na pia kutoka Kambi ya Walio Wachache, naomba nipewe jina la mchangiaji mmoja kwa dakika 10.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uhai na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi ambavyo ameendelea kusimama na Taifa lake la Tanzania katika kuhakikisha amani inapatikana na maendeleo yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Mpango kwa jinsi ambavyo amelisaidia Taifa hili, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu; na kwa kweli na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ujumla wao. Pia, nawashukuru na wengine wote katika idara mbalimbali kwa namna walivyotusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Spika wetu na ninyi mnaomsaidia kwa kazi nzuri inayoendelea. Ninaamini Mbeya watatutendea haki kuturudishia Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninayo heshima kuungana na Wakatoliki, Wakristo wenzangu kufuatia kifo cha Baba Mtakatifu, Papa Francis. Mwenyezi Mungu ampumzishe kwa amani. Pia, tunawapa pole sana *TANESCO* kwa kifo cha Mkurugenzi wetu ambaye ameshapumzishwa, Mwenyezi Mungu pia ampumzishe kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Chama cha Mapinduzi, napenda kukishukuru chama changu kwa siku zote, kwa uteuzi sahihi waliofanya kwa sisi Waheshimiwa Wabunge wote; na hivi mara ya mwisho kututeulia Dkt. Emmanuel Nchimbi awe mgombea mwenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi natoka Wilaya ya Nyasa anakotoka Dkt. Nchimbi alikozaliwa kwa ndugu zake, ninapenda niseme wazi, mimi ninamfahamu vizuri Dkt. Nchimbi kwamba ni mtu mwema, mwenye hekima, mwaminifu, mwenye upendo wa dhati, atamsaidia vizuri Mheshimiwa Rais na Taifa

lake. Pia, ni mtu wa mikakati na ni mtu wa maneno kidogo, kazi zaidi. Kwa hiyo, tumepata mtu wa kumsaidia Mheshimiwa Rais, wote tumuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Prof. Kitila na msaidizi wake Mheshimiwa Nyongo na wote kwa ujumla, ninayo machache ya kuzungumza, na ya kwangu yataenda moja kwa moja kwenye uhalisia wa maisha ya kawaida. Sitatumia *formula au equation*, hakuna; ni moja kwa moja kwa maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi wetu wa Taifa hili, tumeona kuna mambo ambayo yanatoa matokeo ya haraka moja kwa moja, hayahitaji hata kufikiria, hayahitaji eti watu wajifungie watafakari, yapo moja kwa moja, yana mifano siku zote. Niliwahi kuzungumza hapa kwamba, tatizo la lishe yawezekana siyo tu kwa kukosa kula hivyo vinavyotajwa, ni kwa sababu vinachangiwa na mazingira mengine magumu watu kuweza kupata mahitaji yao ya muhimu. Mtu maskini hata ukimwambia ale mayai, atayatoa wapi? Ale kuku kila siku, atatoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mambo yanayowezesha kufungua milango ya maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi kwa wananchi. Kwa hiyo, nikiwa miongoni mwa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma, ambayo ni sehemu muhimu sana Tanzania kwa upande wa Kusini, ambayo imehusika katika historia kubwa ya nchi hii, sehemu ambayo imehifadhi hata wenzetu kutoka nchi jirani walipokuwa wanapigania uhuru; iliwahi kutamkwa na Mheshimiwa Rais katika awamu zetu, nadhani awamu ya tano, kwamba sisi Wanaruvuma pamoja na mikoa mingine ya Kusini tulichelewa kupata maendeleo kwa sababu tulikuwa tupo kwenye changamoto ya kuwa jirani na maeneo yale ambayo yalikuwa yanapigana. Kwa hiyo, tukaahidiwa kuangaliwa jicho la kipekee katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli muda ufike sasa, tuiangalie kwa jicho la kipekee mikoa hii iliyosimama kwa muda mrefu. Mkoa wa Ruvuma ulikuwa unaonekana kama vile hauna sifa za kuweza kuwekezwa, lakini kwa bahati tukapata ile barabara moja. Sasa

hivi tuna madini ya chuma, ipo Ruvuma na Njombe pale, tuna madini haya ya makaa ya mawe, na tuna mpaka Uranium. Tuna madini mengi ya kimkakati, hata *Nickel* ipo pia katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mkoa wa Ruvuma haujawekezwa vizuri katika barabara. Tunaomba, sasa hadithi hizi ziwe na mwisho wake. Tunaomba hadithi zetu za leo, kesho, keshokutwa, hebu tuziangalie kwa jicho la kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Njombe mpaka Songea ifikie mahali tuiangalie. Hebu siku moja Mheshimiwa Waziri atembelee barabara hiyo aone. Malori yanayobeba makaa ya mawe, mzigo mkubwa na sasa hivi kwenye pato la Taifa tumeongeza kiwango kikubwa kutokana na hayo makaa ya mawe. Hebu hiyo barabara sasa itengenezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa sababu ya chuma cha Liganga na Mchuchuma, hebu reli kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay*, kutoka Songea mpaka kule Mchuchuma na Liganga itengenezwe.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Haya, kwa *seniority* tutaanza na Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, anazungumza vizuri sana na ndiyo maana kiongozi wa awamu ya tatu Mheshimiwa Marehemu Mkapa alikuja na *Mtwara Corridor*. Sasa ni vizuri hiyo kwenye sera yetu tuihuishe. *Mtwara Corridor* ilikuwa imelenga kuhuisha maendeleo upande wa Kusini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella unapokea taarifa?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naipokea taarifa kwa mikono miwili.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba nikusitishe kidogo, Mheshimiwa Sanga tafadhali.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa *Eng.* Manyanya kwa anachokizungumza. Barabara ya Makambako – Njombe - Ruvuma, ina zaidi ya miaka 30, na kwa takwimu za *TANROADS* wanapitisha magari au malori sasa hivi yanayobeba makaa ya mawe zaidi ya 1,500 kwa siku. Kwa hiyo, anachokizungumza kinaleta tija sana kwa ajili ya nyanda za juu Kusini kuhakikisha kwamba barabara hii inakwenda vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga. Mheshimiwa *Engineer* Stella unaipokea taarifa?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kabisa, na hii ni kuonesha kwamba watu wa maeneo hayo, ukanda huo, hayo ndiyo matamanio na changamoto wanazozifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hii barabara ambayo tumeizungumzia sana kutoka Kilombero kuja mpaka Namtumbo, na yenyewe ni barabara ambayo itawezesha uchumi mkubwa, basi iangaliwe kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo ipo mpakani. Nchi hii ili iweze kuwa na amani, lazima iwe na usalama wa mipaka yake yote, kuanzia kule Litui mpaka Chiwindi; na pia ukitoka Nyoni mpaka Mitomoni, hizo zote ni barabara muhimu sana kimkakati na kiulinzi. Naomba sana, zilikuwemo barabara hizo katika Ilani ya Uchaguzi iliyopita, bahati mbaya kwa sababu ya mikakati mingine hatukuweza kuzifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zisitoke mle kwenye Ilani mpya itakayokuja. Hayo maeneo niliyoyazungumzia tuhakikishe

yanarudishwa tena ili wananchi waendelee kujua kwamba Serikali yao ikipanga jambo linatekelezwa. Nashukuru sana kwa Daraja la Mitomoni na Daraja la Mkili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nirudi sasa kwenye masuala ya umeme. Umeme ni jambo muhimu. Umeme ukikatika maeneo fulani, tunasikia kelele nchi nzima. Sasa hivi tumefanikiwa kupata huu umeme wa kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere mpaka Chalinze na maeneo mengine unakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mpaka sasa tunaweza kusafirisha megawati zisizozidi 1,000 *maximum*, 800 au 900. Siyo kwamba hatuna uwezo wa kuzisafirisha zote megawati 2,115 zilizotayarishwa pale; mashine zote tisa zipo tayari, line mpaka Chalinze ipo tayari, lakini Kituo chetu cha Chalinze hakina uwezo wa kubeba megawati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kutoka pale kusambaza kwenda maeneo mengine, bado njia hizo za kusafirishia huo umeme hazijawa tayari. Nawaomba sana, tumefanya kazi kubwa sana kama nchi kuhakikisha Bwawa lile tunalimaliza, na kwa kweli Mheshimiwa Rais anastahili pongezi ya hali ya juu kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusianze hapa kupanga mikakati mingine mingine tukaacha kumalizia hili suala ambalo tumeshalianza. Ndiyo maana watu wanauliza, kwa nini tunataka kununua umeme sehemu nyingine? Ndugu zangu msiogope. Hicho ni kiasi kidogo kitakacholetwa, lakini hasa umeme wa uhakika tulioupata ni huo ambao tumeshautengeneza eneo la Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania, tusiwe tena ni watu wa kuondoka tukaacha hili, tukaenda hili. Hii *project* tuliyoianza tuikamilishe vizuri. Nchi ikishakuwa na umeme wa kutosha, hata wawekezaji wataweza kwenda kuwekeza popote pale. Hayo tumeona

matokeo yake, baada ya kuwa na umeme angalau unaoaminika, hali ya uwekezaji imeendelea kuwa ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, niseme kwamba tunaenda kwenye uchaguzi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako uliisha muda mrefu, naomba uhitimishe.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunaenda kwenye uchaguzi, nategemea bajeti ya kutosha itawekwa ili vyombo vyetu viweze kusimamia vizuri uchaguzi uwe wa haki na wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba wakati tunaendelea, tutambue wageni ambao tunao sasa.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambao ni kama ifuatavyo: Ndugu Vicent Minja, Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo *(TCCIA)*. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Kitila ni Wakurugenzi na Maafisa kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji; tunao wadau wa maendeleo, wawekezaji na wapigakura wake 30 kutoka Jimbo la Ubungo Jijini Dar es Salaam. Karibuni wote kwa pamoja. Mtatusamehe tumewasimamisha kwa ujumla, ahsanteni sana, karibuni sana. Profesa tunaye humu ndani, tunawashukuru kwa kumpigania wakati wote. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni watangazaji wa kipindi cha Kilinge cha Familia kutoka Azam TV Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. (Makofi)

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge na Naibu Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Maswa Mkoani Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni 65 wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge ambao ni wanafunzi na walimu wa *St. Therese of Lisieux* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana waalimu na wanafunzi wetu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Namkaribisha Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya na kama muda utaruhusu nitawakaribisha wachangiaji kutoka kambi ya walio wachache, watachangia wawili kwa dakika tano tano, na kama muda hautaruhusu wachangiaji wetu wataendelea mchana.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kujadili Fungu Na. 66, Tume ya Taifa ya Mipango ambayo katika bajeti hii tunayoijadili hapa, Mheshimiwa Rais ameitengea shilingi bilioni 48.5, ukilinganisha na mwaka 2024 ambayo ilikuwa shilingi bilioni 46.2, kuna ongezeko la zaidi ya shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ile ukiisoma imeainisha changamoto kubwa tatu. Changamoto ya kwanza ni matumizi hafifu ya mifumo katika uchambuzi wa miradi. Changamoto ya pili ni ugumu wa upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya uchambuzi wa masuala ya kimkakati ya uandaaji wa mipango na utekelezaji wake na changamoto ya tatu ambayo imeainishwa ni uelewa mdogo wa wadau kuhusu shughuli za Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wenzetu wa Serikali wenye hoja hii mezani, kwenye mapendekezo yao ya nini wanakwenda kufanya kuhusu changamoto hizo, pendekezo la kwanza wamesema watakwenda kuwekeza kwenye TEHAMA (teknolojia), nawapongeza sana; pendekezo la pili, vivyo hivyo ni

kuwekeza kwenye TEHAMA, kwenye teknolijia, nawapongeza sana; na pendekezo la tatu ni kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mara nyingi imezoeleka kwamba, ukichangia unaorodhesha namna ya utatuzi, lakini mimi nataka niorodheshe changamoto kama mbili hivi ambazo inapaswa zingaliwe ukiacha hizi tatu ambazo zimewekwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ninayoiona ambayo Tume yetu ya Mipango inakabiliwa nayo ni mfumo wa sasa ulivyo. Mheshimiwa Waziri, Profesa hapa, akileta mpango tukaupitisha, tunaanza kuutekeleza, na utekelezaji wake unategemea bajeti ambayo kimsingi inasimamiwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati wa *disbursement,* mpango tumeshaupanga na tumeshaanza kuutekeleza halafu Waziri mwenye dhamana ya Mipango hana nafasi. Nafasi yake huioni kwenye *disbursement* ya fedha za kwenda kutekeleza huo mpango alionao. Kwa maana kwamba *disbursement* inakuwa *initiated* na *PST*. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anaomba kibali kwa *CAG* halafu *CAG* akishatoa kibali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anapeleka kwa Maafisa Masuuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwenye huu mchakato nilioueleza hapo, nafasi ya Tume ya Mipango ionekane, la sivyo, mwishoni utakuwa unashindwa kufanya tathmini yenye uhalisia kwa sababu utakuwa una mpango mzuri halafu ukija kutathmini unagundua kuna baadhi ya maeneo muhimu sana ambayo fedha hazikwenda. Kwa hiyo, ni muhimu sana pawe na hiyo *intervention,* tuione hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tume za mipango duniani kote ndiyo chombo kikubwa na Wizara kubwa kwenye nchi na hata kwetu ndivyo ambavyo Mheshimiwa Rais ameleta hapa sheria tukaiandika hivyo, kwamba, Tume hii ya Mipango kwa maana ya Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji, kwenye eneo la mipango ndiyo chombo kikubwa ndani ya nchi yetu kwenye kusimamia masuala ya mipango na hatma ya Taifa letu kwa miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, tusichoke kuipitia upya ile *structure* yetu kwa ukubwa huo huo. Kila mara najaribu kuangalia ile sheria tuliyoitunga kwamba tuna *structure* yenye Idara Saba na Vitengo Nane. Siku zinazokuja nafikiri tuanze kufikiria na kuangalia, kwenye zile idara saba zipi tuzi-*convert* tuzi-*upgrade* ziwe kurugenzi na ni kwa kuzingatia tu ukubwa wa majukumu yenyewe yaliyopo mbele yenu. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuangalie hiyo *structure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara hii, bajeti pamoja na mipango ni *instrument* ya Mheshimiwa Rais duniani kote. Bajeti na mipango ni *instrument* ya Rais na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miaka minne ambayo amekuwepo madarakani amefanya vizuri sana kwa kutumia mipango na bajeti tunazopitisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni kwa vile tu haiandikwi, nami wakati mwingine nawashangaa wasomi wetu, waandishi wetu na maprofesa wetu wanaotunza kumbukumbu za maeneo mbalimbali duniani. Ni vile tu haiandikwi, ila ingekuwa inaandikwa, kuna maandiko mengi sana ambayo ingelazimika yabadilike kwa namna ambavyo Tanzania imefanya mageuzi na kufika hapa tulipo kwa miaka hii minne ukilinganisha na zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaeleza *reforms* na hii nataka iwe elimu ya matumizi mazuri ya neno "*reforms*." Kuna watu wanalitumia hili neno "*reforms*" vibaya. Nitaeleza *reforms* ambazo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia mipango ambayo tunaifanya hapa ameitekeleza ndani ya miaka hii minne na kuifanya Tanzania kuwa na ramani tofauti kwenye ulimwengu na dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano michache sana. Ukiangalia, kwa mfano kwenye barabara zetu zinazosimamiwa na *TARURA,* tumefanikiwa kufikisha mtandao wa kilometa 144,429 wenye thamani ya trilioni 2.7. Zunguka kwenye nchi nyingi za Afrika; siyo vizuri kuingiza humu kwenye *Hansadi* kwa kuzitaja nchi hizo. Zunguka nchi nyingi za Afrika, utagundua tumewaacha kwa mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye barabara zinazosimamiwa na *TANROADS,* Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia mipango hii na Wizara hii toka ikiwa Wizara ya Fedha mpaka sasa, ametuwezesha kufikia kilometa 37,373 za kiwango cha lami, barabara ambazo zina thamani ya trilioni 32.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizunguka nchi nyingi za Afrika, ukaenda kwenye nchi nyingi za Asia, ukaenda kwenye nchi nyingi za Amerika ya Kusini, utagundua kwamba tumewaacha watu kwa mbali sana, kwa mbali sana. Tumefanya *reforms,* na hizo ndiyo *reforms* ambazo Watanzania wanataka kuona. Ukiinga kwenye sekta ya elimu kwa miaka hii minne peke yake, tumejenga shule 2,441 ambazo ni mpya na katika hizo shule, shule 1,042 ni za sekondari na shule 1,399 ni shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni *reforms* kubwa ambazo tumezifanya ndani ya miaka minne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Zunguka Afrika nzima utagundua kwamba tumewaacha kwa mbali sana kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ipo *SGR* ambayo kama Watanzania kila tukisimama hapa tunajivunia kuwa na jambo kubwa kama lile. Jambo ambalo hata nchi za Ulaya zinalimulika kwa tochi, nchi za Ulaya kwa *SGR* tuliyonayo pale. Haya ni mapinduzi makubwa, mageuzi makubwa, na *reforms* ambazo zinatokana na mipango thabiti hii ambayo tunajadili hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niongelee eneo lingine na nilieleze kwa urefu kidogo huku nikitoa mifano ya jimboni kwangu. Eneo lingine ambalo Mheshimiwa Rais ameifanya Tanzania ikawa kwenye ramani tofauti kabisa duniani ni eneo la afya. Ndani ya miaka hii minne ambayo amekuwepo madarakani, ameweka shilingi trilioni 1.3 ambazo zimefanya kazi zifuatazo kwa nchi nzima, Majimbo yote Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimejengwa hospitali 129 kwenye Halmashauri mbalimbali, zimekarabariwa hospitali kongwe 48

ikiwemo Hospitali ya Handeni Mjini ambayo sasa hivi iko pale. Pia, vimejengwa vituo vya afya 367 nchi nzima, kikiwemo Kituo cha Afya Kwedinguzu kule Malezi chenye hadhi sawa na Hospitali ya Wilaya, mambo haya hayakuwahi kuwepo na haya ni mapinduzi makubwa na ndiyo *reforms* zinazotakiwa kuzungumziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, zimejengwa zahanati 980 na katika hizi 980 hapa Handeni Mjini ukienda kwa wananchi wa Mankinda wameziona hizi *reforms*. Iko zahanati pale, ukienda Kwedizando, Bangu, Kwaluwala, zipo zahanati pale. Ukienda Hedi, Kwediseni pale Msasa, ukaenda Kwabaya na Kwasindi, kote huko Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya *reforms* za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo ndiyo *reforms* inayotakiwa kuzungumzwa. Ukijiona unazungumza *reform* isiyohusu haya mambo, wewe unapoteza muda na kwa kweli watu wakajitathmini. Pale Handeni Mjini hatukuwahi kuwa na *X-Ray* kwa miaka hiyo mitano iliyopita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta X-*Ray* ya kisasa ambayo hata ukisema unatoka hapa unaenda kutibiwa India, utaikuta hiyo hiyo na *specifications* hizo hizo, iko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuna jengo jipya la *ICU, EMD*, maabara ya kisasa ambayo hivi leo Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi ataizindua pale. Sasa haya mambo mengine, hata sisi miaka ile zamani tulivyokuwa wadogo, mkienda kucheza mpira na timu pinzani unaangalia, mkiona ile timu wachezaji wake wote wamevaa viatu, mnakataa kuingia uwanjani. Ni lazima mkatae kuingia uwanjani! Yaani wote wamevaa viatu halafu nyie mko peku! Mnakataa kuingia uwanjani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata mimi sishangai kabisa kwa mambo haya ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya. Hata mimi ningekuwa wao, ningegomea uchaguzi. Ukiingia, ni lazima upigwe tu kwa sababu kazi zimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda huu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Reuben. Nashukuru sana kwa kuzingatia muda pia. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo ni Mheshimiwa ProfesaShukrani Elisha Manya. Karibu.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na hasa kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa mwisho katika *session* ya asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, yako wazi sana na yanaonekana katika huduma bora za usafirishaji, miundombinu, afya, elimu pamoja na nyingi ambazo tunaweza tukaziorodhesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza Dira yetu ya Taifa ya Miaka 25 ijayo ambapo lengo lake kubwa ni kuwa na uchumi jumuishi, kupunguza umaskini na uzalishaji wa ajira nyingi kupitia uwekezaji. Hii dhana ni njema iwapo Watanzania wote wataona uchumi ukikua katika maeneo yao na hata kwa watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirejee mafanikio yaliyopatikana na hatua ambayo tunapaswa Kwenda nayo. Katika eneo la nishati, ni kweli kwamba kukamilika kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere kumeongeza umeme mwingi sana katika *Grid* ya Taifa na hivyo kufanya huduma ya utoaji umeme kwa wananchi, viwandani na kila mahali kuwa imara na bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kujivunia, lakini natamani Serikali ichukulie kwamba ni hatua ambayo inapaswa kuendelezwa ili kukamilisha kile ambacho tunakitaka kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukadhani kwamba umeme huu umetosha, lakini viwanda vitakapokuwa vingi na wananchi watakapokuwa *connected* wote, tunaweza kuanza kuona umeme unapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafanya nini? Serikali inapaswa kuchukulia mafanikio hayo kuwa chachu ya kuendeleza vyanzo vingine vya umeme ili tupate umeme mwingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *potential* ya Tanzania katika eneo hili ni kubwa sana, na kwa sababu vyanzo hivi vipo, Waingereza wanatumia neno la *hanging fruits*, yaani ni tunda ambalo liko chini na ambalo unaweza ukalivuna kwa ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *potential* ya kupata umeme mwingi kupitia nishati ya joto ardhi ni kubwa na utafiti umeshafanyika na sasa chanzo hicho cha *geothermal* ni lazima tukifanyie kazi haraka ili tuweze kuongeza umeme mwingi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumeendelea kuwa na mahali ambapo kuna upepo wa kutosha kwa ajili ya kutoa umeme, lakini tumekuwa bado tukipaacha, lakini nishati ya upepo ni eneo lingine ambalo ni *hanging fruit* ambalo tunaweza tukalivuna na tukapata umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari gani juu ya makaa ya mawe na habari gani juu ya nishati ya jua au *solar energy?* Tukifanya hivyo tukaongeza umeme ukawa mwingi, hata bei ya umeme inapaswa kushuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme utakaposhuka, viwanda vitazalisha bidhaa kwa gharama nafuu, na kwa hiyo tunapata tija watu wote na hata Watanzania wengine wote. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunapokuwa tunapanga mipango yetu tuyazingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mafanikio ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini tuyajazie na vyanzo vingine ambavyo

tayari vinajulikana vipo, na tafiti zimefanyika, ili tuweze kuwa na nishati nyingi nchini Tanzania, tuwe kigezo cha Taifa linalokuwa na nishati inayopatikana kwa gharama nafuu na inayotosheleza mahitaji yote ya viwanda pamoja na ya wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo mipango yetu inapaswa kujielekeza vizuri na kwa mujibu pia wa taarifa ambayo imetolewa hapa, ni eneo la uwekezaji. Katika hili napenda tutambue kwamba tutakapowekeza zaidi ndipo tutakapotengeneza ajira zinazotokana na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imeendelea kuwa ndiyo mwajiri mkubwa na ndiyo maana hapa Bungeni utakuta wote tunagombea zile ajira zinazotokana na Serikali, lakini Serikali itakapoweka mazingira wezeshi na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi, basi tutaona mabadiliko na hivi ndivyo ambavyo napendekeza. Kwamba, mara nyingi sana Serikali imekuwa ikisimiamia na kutoa miongozo, inapokuja kwenye kuwezesha, utagundua kwamba siyo kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika miradi mikubwa, kama kuna kampuni za Kitanzania za wazawa ambazo zina uwezo sawa na kampuni za nje, Serikali ina sababu ya kutoa kipaumbele ili tuweze kukuza uchumi wa wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika miradi hii mikubwa ni lazima Serikali iwaandae Watanzania. Siyo habari ya kutangaza fursa, ni kuwaandaa Watanzania kwamba fursa iko hapa na ninyi mnaweza mkaona mnashirikije katika hii fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unawaanda, wanakuwa tayari, halafu unawapa kipaumbele na kwa jinsi hiyo uchumi utaendelea kukua ndani ya nchi badala ya miradi mikubwa kuwa zinapewa kampuni za nje. Hapo maana yake ni kwamba, Tanzania inachukua hizo fedha zake, inazozalisha, halafu zinakwenda kufaidisha kampuni nyingi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali pengine ambapo nilitamani kuchangia ni kwamba, sisi kama Taifa, nimetamani sana kupata

Lugha ya Kiswahili inayostahili hili neno '*niche'*, lakini sikupata. Tanzania kama Taifa, nini ni kitu ambacho tunasema kwamba tunakifanya kwa ubora kupita Mataifa mengine yote ili tujulikane kwamba, ukifika Tanzania hao wanafanya hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya nchi yetu ni lazima itufikishe mahali ambapo tutasema kwamba hili ndiyo eneo ambalo sisi kama Watanzania tunalifanya vizuri kuliko watu wengine wote. Unaweza kulifanya hilo kwa kuangalia rasilimali ulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la ardhi na kilimo. Tanzania tumejaliwa ardhi inayoweza kulimwa vizuri ukilinganisha na Mataifa yanayotuzunguka. Je, hatuna sababu ya kupanga tukajulikana kwamba, Tanzania kama nchi ndiyo inayolisha watu wengine wote wanaowazunguka kwa sababu, hilo ndiyo eneo ambalo rasilimali yetu ya ardhi inatufanya tuweze kuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani tulipange hilo vizuri, kama tunatamani kuwa nchi itakayolisha watu wengi, maana yake ni *agrarian economy*. Basi, tufanye vizuri katika hilo eneo na tuwe na zao ambalo tunajulikana kwalo kwamba hilo linatoka Tanzania na Watanzania, unapoongea habari ya hilo, hao wanafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina imani kwamba, kwenye kilimo iwapo kitafanywa kuwa cha kuvutia sana, vijana wengi wataingia hapo na litakuwa ni eneo ambalo ajira zinaweza kupatikana. Pia, tuwe na ile dhana ya kwamba tulime mazao yetu, yatoke shambani, yaingie viwandani, halafu ndipo yaende kwa walaji. Kwa hiyo, huo ni mpango ambao ni lazima tuendelee kuusukuma ili hatimaye tuweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, eneo lingine la viwanda, kuongeza thamani ya rasilimali tulizonazo. Katika eneo hili natamani kwamba sisi kama nchi tuweze kujifunza kwa wale waliofanya vizuri zaidi. Hili linakuja tunapoanza mchepuo wa shule zetu za amali, tusianze kwa udhaifu. Kama kuna watu duniani huko wamefanya vizuri zaidi katika kufundisha mchepuo wa

amali, sisi tujifunze kwao ili tunapoanza, tuanze tukiwa na ubora wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano michache. Ninaamini utaniruhusu kwa dakika zilizobaki. Kwa mfano, uchongaji wa vito, nchi kama India ni wazuri sana katika kuchonga vito, madini aina ya vito, duniani kote wanajulikana hivyo. Sisi tunavyo vya kutosha, tunachopaswa kufanya ni kuwaruhusu, tuwaingize waje, tushirikiane nao, watufundishe ili nasi tuanze kuwa ni wachongaji wazuri kama wao. Kwa hiyo, turuhusu ushirikiano huu ili tuweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine wa kujaribu kuonesha hali ambayo tunaweza tukaiendea, Tanzania tuna mazao mengi sana na mazuri ya misitu, mbao laini, na mbao ngumu, lakini kwa nini bado tunapenda *furniture* zinazotoka nje? Ni sababu hatukuchukua za kwetu, tukaziboresha kwa kiwango ambacho ni kikubwa, hatimaye nasi tukawa ni *niche area* ya kwamba mbao au *furniture* kutoka Tanzania zinapendwa hadi nje ya nchi. Hii ni kwa sababu hatujaziboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hili lazima tujifunze kwa waliofanya vizuri zaidi, tushirikiane tupate teknolojia sahihi na ujuzi sahihi ili rasilimali tulizonazo zitusaidie kupata maeneo ambayo tutafanya vizuri. Kwa kufanya hivyo, tutaongeza ajira na tutatambulika hivyo duniani, pia tunaweza hata ku-*export* kwa sababu tumeyachagua kuwa ni maeneo yetu ya ubora ambayo yanazidi watu wengine kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, napenda kuunga mkono hoja na ninaomba tuwapitishie bajeti hii ili waweze kufanya kazi hii, na Tanzania iendelee kuwa ni mahali bora, na iendelee kuwa na watu ambao tunasifika kwa mambo makubwa ambayo tumeyapanga wenyewe, na ni lazima tuwe na vitu ambavyo tunayazidi Mataifa mengine kwa kuzingatia rasilimali tulizonazo kwa kuziboresha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Shukurani Elisha Manya kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru wote ambao mmepata nafasi ya kuchangia asubuhi hii. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuendelea kuzingatia hoja kwanza za Kamati na pili za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunayo matangazo; kwanza ni Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao jioni, ambao ni Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga.

Waheshimiwa Wabunge, pia tunalo tangazo ambalo linatoka kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake *(TWPG)* kuwa tarehe 24 Aprili leo, mara baada ya kuahirisha kikao hiki cha Bunge saa saba mchana huu, kutakuwa na kikao na Mheshimiwa Spika ambacho kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa muda wa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega pia kwa dakika tano na Mheshimiwa Charles Stephen Kimei ajiandae kwa dakika 10.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, na kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii. Kwa kuwa dakika ni chache, nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, na wasaidizi wake: Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri wote, na Serikali kwa ujumla, kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Hongereni sana na tunawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwenye eneo moja kubwa. Kwa kuwa Wizara hii inahusika na mipango mbalimbali na ndiyo ambayo kwa jinsi ambavyo imeundwa na muundo wake, utasimamia programu mbalimbali za kimaendeleo na mipango ya jumla ya nchi ili tuweze kupata Tanzania yenye maendeleo makubwa kwa kushirikiana na Wizara nyingine zote ambazo kwa namna moja ama nyingine zinaingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mikubwa ya kimkakati. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, alichukua nchi hii na miradi hii ya kimkakati yote, hakuna iliyokwama, inaendelea kwa kasi na kwa ubora ule ule ambao ulitakiwa uwepo. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii miradi mikubwa ushauri wangu, mtaiangalia kwenye mipango yenu, miradi hii mikubwa;

*SGR,* Bwawa la Nyerere, ujenzi wa Viwanja vya Ndege, ununuzi wa ndege, na hata ujenzi wa haya majengo makubwa ya Serikali. Ukiacha Mji wa Kiserikali pale Mtumba, lakini pia, kuna taasisi nazo zinafikiria kujenga majengo makubwa ya *billions of money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri kwa sababu inachukua fedha nyingi, miradi hii ikishakamilika kulingana na mipango yake mfano: *SGR* ifike mwisho kama ni Kigoma; Bwawa la Nyerere likamilike kwa ukamilifu wake kulingana na andiko la mradi; na miradi mingine yote. Ushauri wangu ni kwamba, ni lazima tufikirie mbele ya safari kwamba, hii miradi mikubwa ya kimkakati ikishakamilika basi tujipe pumziko kidogo; watu wanasema, "tuvute pumzi kidogo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini? Kwa sababu hii miradi mikubwa inachukua fedha nyingi sana, na wakati mwingine fedha nyingine ni za mikopo. Ikishakamilika tuishie hapo, tuone huu uwekezaji uliofanyika kwenye hii miradi ianze kutengeneza faida, zile ambazo zimekopewa fedha, zianze kulipa madeni yake au mikopo yake. Fedha zitakazopatikana, nyingine zitakazobaki ambazo zitatokana na makusanyo ya Serikali, sasa tuzielekeze kwenye maendeleo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba kwenye maendeleo ya watu imesahaulika, hapana. Hii mikakati mikubwa wakati mwingine wananchi kwa namna moja ama nyingine hawai-*feel,* yaani hawaioni moja kwa moja, wanaweza wakaona kwa upande mchache.

Mheshiiwa Mwenyekiti, tukielekeza nguvu kubwa kwenye yale ambayo kwa namna moja ama nyingine yanagusa watu moja kwa moja, mfano ujenzi wa barabara za lami; upo, siyo kama umesimama, unafanyika, lakini sasa tuelekeze nguvu kubwa kuhakikisha barabara nyingi na kwa kadiri inavyowezekana, ziendelee kufunguliwa, kwa sababu ukifungua barabara, umefungua uchumi wa wananchi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nzuri za viwango zinazopitika mwaka mzima bila changamoto, miradi ya umeme,

miradi ya maji, shule zetu tuendelee kuziboresha na kuziimarisha, pamoja na miradi ya afya kwenye zahanati zetu. Leo tuna zahanati ambazo hazina hata umeme, au umeme upo lakini hata ule utaratibu tu wa halmashauri kufanya mfumo wa umeme, mapato hayatoshi; na zahanati ziko nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufikirie huko mbele ya safari miradi ya kimkakati ikishakamilika kwa ukamilifu wake, sasa turudi kule chini kwenye miradi ambayo itagusa wananchi moja kwa moja, tuwekeze nguvu kubwa, wananchi waweze kuona matokeo ambayo wanatamani kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala zima la ajira na mambo mengine yote ambayo wananchi kwa namna moja ama nyingine wanatamani kuyaona na kuyafikiria, yaani wai-*feel* kwamba kuna kitu ambacho Serikali imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivi, haimaanishi kwamba hakuna kinachoendelea, kuna kazi kubwa imefanyika sana; shule nyingi na nzuri, lakini kwa sababu kuna idadi kubwa ya ongezeko la watu ambao wana hayo mahitaji, kwa mfano huduma bora za afya zenye ukamilifu, watumishi wawepo, madawa yawepo, vifaatiba vyote viwepo kwa ukamilifu wake. Sasa tufikirie mbele ya safari jambo hili liweze kufanyiwa kazi na wananchi waweze kupata huduma muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu ni ushauri wangu na ndiyo mchango wangu katika eneo hili kwa Wizara hii. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, atafuatiwa na Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami nichangie katika Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wizara nzima. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais,

pamoja na Makamu wa Rais; Waziri Mkuu; na Mawaziri kwa kazi wanayoifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahusika na Mipango na Uwekezaji, na kitu kikubwa ambacho tunakiangalia hapa, Wizara karibia zote zina-*fit in* katika Wizara hii. Sasa nina mambo machache tu ya kushauri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia sana kuhusu kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Ameyazungumzia sana katika uboreshaji wa kisera, uboreshaji wa kisheria, na uboreshaji wa kikanuni. Pia amezungumzia mambo mbalimbali na wametoa na kupunguza tozo ambazo zinatokana na changamoto mbalimbali za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa hiki, lakini bado Watanzania wengi wana changamoto mbalimbali. Najua hizo zitaenda kuboreshwa jinsi tunavyokwenda. Nampongeza kwa sababu amepita maeneo mbalimbali kusikiliza wananchi na kujua nini changamoto kubwa zinawapata wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pendekezo langu lilikuwa, katika kufanya kazi zote hizi, katika hii Wizara kuwe na *thinktank* ambayo itajumuisha *Scholars* mbalimbali wa sekta mbalimbali. Kuna nchi nyingine tunakuta wana *thinktank* ambao wapo wa *Government* ambao wanafanya kazi ya kubuni changamoto zilizopo, utatuzi wake na utekelezaji wake ili kwenda haraka katika kupata uchumi mzuri. Kwa hiyo, pakiwa na hicho itasaidia sana kwenda haraka katika utatuzi wa mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na *Centre of Excellency* ambao wanabobea katika masuala hayo, watu waweze kujengwa na kuwa katika maeneo mbalimbali ya mambo hayo. Kwa hiyo, tukiwa na hiyo mikakati, na tukawa na utatuzi mzuri, tutafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nashauri Serikali iwekeze katika mazingira wezeshi ya Sekta ya Kilimo. Tuna changamoto sana ya ajira, lakini tunajua kwamba kilimo

kinaweza kikaajiri watu wengi sana. Sasa kukiwa na mazingira wezeshi ya kilimo na tukawekeza kwa Sekta Binafsi, yaani kuwe na mazingira mazuri ya Sekta binafsi ili waweze kuajiri watu wengi, na nchi yetu itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye Sekta ya Kilimo, Jeshi la Magereza na JKT wana maeneo makubwa sana. Tukifanya uwekezaji katika Jeshi la Magereza na tukawekeza katika Jeshi la Kujenga Taifa, tutafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nchi ya Misri wana hekta 5,000 tu lakini wanalisha nchi 15 za Ulaya. Jeshi la JKT wana hekta 12,000, hiyo ni Chita tu. Sasa je, kama tutawekeza vizuri katika Jeshi letu la Magereza na JKT, tukawawekea mtaji mkubwa, wakaweza kulima kilimo kizuri, bora na cha kisasa hawa watakwenda kukomboa hili janga la watu kukosa ajira, na kweli tutakuwa tumefikisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia nchi nyingine za Afrika, na nyingine duniani, wanawekeza katika hizi sekta vizuri kabisa. Yaani tukitoa fedha kiasi tukawapa, kweli tunaweza tukajikuta tunavuna, tunawekeza vizuri na tunawapa wananchi ajira bila kuwa na changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kweli, miradi mingi imefanyika, na mmefanya kazi kubwa sana katika hiyo miradi mbalimbali katika kufanyia kazi. Kwa hiyo, changamoto iliyopo sasa hivi ni wananchi kuwa na uchumi mmoja, mmoja. Kuwa na uchumi wa mtu mmoja, mmoja ni kitu ambacho mkitazame sana katika hii Wizara ya Uwekezaji, kuangalia ni wapi wananchi wetu watapata hivyo; na je, tunazalisha matajiri wangapi kila mwaka? Tuna matajiri wangapi kila mwaka tunaowazalisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Uwekezaji ndiyo inapaswa iangalie ni wapi tutawekeza ili tuweze kupata watu ambao wanaweza kusaidia kulipa kodi katika hii nchi na tukaweza kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, ahsante sana kwa kujali muda.

Waheshimiwa Wabunge, hawa Wabunge wetu wawili wameanza vizuri sana, wamehakikisha kwamba ndani ya muda waliopangiwa wanakamilisha hotuba zao. Itakuwa vyema kama kila mmoja ataiga mfano mzuri ambao Waheshimiwa Wabunge wameuonesha.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa *reforms* zile ambazo zimeelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, ambazo ninaamini kwamba na zenyewe zimechochea na kuwezesha hii Wizara kuandikisha miradi mingi kwenye kile Kituo cha *TIC* na kwenye maeneo mengine hata kwenye *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake Naibu wake, Katibu Mkuu, wale Viongozi wa zile Taasisi zake Tume ya Mipango (Mkurugenzi Mtendaji), pamoja na watu *TIC* na *EPZA,* na wengine wote pamoja na Katibu Mkuu ambaye nimesahau kumtaja mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa itifaki nitambue na kusema kweli kwamba kazi wameifanya vizuri. Kujenga taasisi ni jambo gumu sana, uanzishe Wizara ambayo inaunganisha taasisi mbalimbali ambazo unaweza kuzifanya zikaweza kufungamanishana, ni jambo ambalo siyo rahisi sana. Niliwahi kuifanya na ninajua kazi ilivyo ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza kwamba, sasa hivi Wizara hii imesimama vizuri na ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuiatamia vizuri na ikaonesha kweli inaweza ikafanya kazi. Nami niliposikia tu kwamba tumeweza kuorodhesha

miradi 901 kwenye *TIC* ambayo ina thamani ya dola bilioni tisa na, nimefurahi na nikasema kumbe tunakwenda pazuri. Niseme kwamba zile *reforms* zilizotajwa ambazo zimetengenezwa na Mheshimiwa Rais zenyewe zimechochea sana hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hizi *reforms* niseme kwamba, kama alivyosema mwenzangu zimefika kila mahali hata kule kwetu kwenye Jimbo letu la Vunjo hizi *reforms* zipo. Kwa mfano, tulikuwa na zahanati 13 na sasa 25; vituo vya afya tulikuwa navyo viwili, na sasa tuna vinne na pengine cha tano kitapatikana. Barabara zimetengenezwa kwa kiwango chake pamoja na *TARURA* na *TANROADS* wanaendelea kutengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara mojawapo ambayo ninaililia sana ya Mandaka – Kilema, ambayo inaenda pole pole, lakini ninaamini kwamba tunaendelea vizuri. Pia tumepata barabara ya lami; *TARURA* wametujengea barabara ya lami kutoka Himo Sokoni – Lotima na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiye aliyetoa hayo maagizo kwamba, hiyo kazi ifanyike mapema na hiyo kazi imefanyika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutoa hizi pongezi, najua kwamba jukumu kubwa la hii Wizara ni kubuni dira, mipango, mikakati, na sera za kukuza uchumi wetu kwa haraka zaidi ili tuweze kufikia angalau zaidi ya asilimia nane ya ukuaji wa kila mwaka wa pato letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kubuni sera za kukuza uchumi, lakini sera ambazo pia zinaleta ushirikishi wa wananchi wetu kwenye shughuli za kiuchumi na hivyo kupata kipato ambapo ni *redistribution,* kwamba ni *growth with redistribution*. Ni jambo ambalo ni gumu, na ninaamini kwamba Serikali imekwenda vizuri, ime-*identify* sekta ambazo zinaweza kuleta tija hapo, kwa mfano kilimo imeweka fedha pale. Niseme kwamba hilo ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme hivi, mwenzangu alisema kuhusu *think tank*, lakini nasema kuna taasisi zinazofanya

utafiti wa sera na utendaji wa uchumi wetu. Kwa mfano, *REPOA* na *ESRF* ni taasisi ambazo zinatakiwa zisaidie hii Wizara katika kuchambua sera zile zinazotekelezwa, na pia kutoa mawazo yao kuhusiana na kitu gani kifanyike ili mambo yawe sawa na *impact* ya hizi, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bahati mbaya hizi taasisi mbili nilizozitaja na pengine kiongozi, hii sijui, wengine wanapata fedha kidogo, lakini taasisi hizi hazina fedha yoyote wanayoipata kwenye Serikali zinategemea Wahisani. Sasa Wahisani wakienda pale wana ajenda zao. Wale jamaa hawawezi kufanya *core research* ambayo itaweza kusaidia Wizara nyingi katika kutatua matatizo hapa na pale na kuonesha ni kitu gani kifanyike huko mbeleni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri wa Mipango kama *thinktank* ahakikishe kwamba anapohitimisha anasema kwamba, hizi taasisi zitapata pesa kutoka Serikalini ili waweze kufanya *research* ambayo itawasaidia wao wenyewe wakati wanapounda hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pamoja na mengine, tumeona kwamba hii Wizara ambayo tulitegemea ndiyo ifanye sasa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Serikali. Imeweka jukumu la ufuatiliaji na tathmini kwenye idara. Sasa hii idara ina Mkurugenzi, huyu Mkurugenzi anatakiwa aweze kufuatilia miradi inayofanyika kwenye Wizara zote na aweze kukosoa, aweze kusimama nao kidete na hata kuwaambia ninyi nitawapeleka mahali fulani muadhibiwe. Lakini sasa huyu Mkurugenzi kweli ataweza kwenda kwa Afisa Masuuli, Katibu Mkuu na kuanza kum-*criticize?* Inakuwa vigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hiyo idara ya tathmini na ufuatiliaji igeuzwe, ifanywe tu kama mamlaka. Mheshimiwa Rais Kikwete wakati wa Awamu yake ali-*create* kitu kinachoitwa *Presidential Delivery Bureau,* ambayo mtu ilikuwa ukiitwa pale hata kama ni kutoka Sekta Binafsi unatetemeka; kwa sababu inakuhoji, inakulazimisha kujibu masuala fulani fulani na kama ni mradi umeshindwa kutekeleza, wanakwambia tutakufukuza, tutafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ile *Presidential Delivery Bureau* ilikuja kufa kimya kimya bila kufanyiwa tathmini ya kutosha. Nafikiri falsafa nzima ya kufanya tathmini na ufuatialiaji wa miradi na ahadi za Serikali, ahadi za viongozi zinatakiwa zifanyike kwenye *Presidential Delivery Bureau*, ambayo inaweza ku-*buy it*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiweka kwenye nanii, maana yake tume-*dilute* hata maana ya hii Wizara ambayo ndiyo inatakiwa itengeneze mpango mkakati, halafu ifuatilie kwenye Wizara zote, ndiyo sababu ninafikiri nilikuwa humo Wizara mama kabisa imekaa katikati. Uzuri mmoja imekaa kwenye Ofisi ya Rais, kwa hiyo, nafikiri kwamba tuangalie ni namna gani ya kuinua hadhi ya Wizara hii ili tuweze kutengeneza chombo ambacho kitafuatilia hii miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi niliwaambia zimekuja *ambulance,* zimepelekwa kwenye kila jimbo, majimbo yanapata *ambulance* tano ilhali tayari wanazo nyingine tano huku jimbo langu linapata *ambulance* moja tu. Sasa, nikienda kule nitasema nini? Ni lazima hii *delivery* iweze kusema mbona kule kuna nne tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala mengine kama ya ajira, kwa mfano 40% ya waajiriwa hawana kazi, wanazubaa zubaa tu huko mtaani. Hii *presidential delivery* ndiyo ingetakiwa ifuatilie kwa sababu wale watu wengine ambao wanahodhi hawa wafanyakazi wana-*conflict of interest,* hawawezi kuwafukuza. Kwa hiyo, nafikiri hiyo ifanyike ili tuweze kuendelea mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mambo ya takwimu ukimsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo au Waziri wa Mifugo anavyoelezea jinsi walivyotekeleza mambo mengi, bajeti yake, imekuwa mara tatu. Anatupa takwimu hapa, mimi nasisimka, nikasema sasa uchumi huu utakua kwa asilimia nane, lakini ukirudi kule kwenye Mtakwimu Mkuu wa Serikali *(NBS)* anakwambia bado kilimo kinakua kwa asilimia nne. *It is impossible,* haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti imeongezeka mara tatu *and then* unasema; au mifugo imeongezewa bajeti halafu wakati huo huo eti uchumi huu unaendelea kwa asilimia nne au tano badala ya kukua kwa asilimia nane, badala ya kukua kwa asilimia nane. Fedha inakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba kuna kitu fulani *corroboration* ya takwimu za Waziri na zile zinatoka kwenye *NBS* inatakiwa isimamiwe na Wizara hii ya mipango, yenyewe ndiyo iweze kujua ni kitu gani kipo kwa uhalisia, na ndiyo maana ya ufuatiliaji na tathmini. Nafikiri kwamba taswira ya Serikali kujiondoa kwenye miradi ya biashara imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani watu tulikuwa tuna-*argue* kwamba Serikali iende, baadaye tukasema isiende; lakini mimi nafikiri kwamba bado Serikali inawajibika kuingia kwenye miradi fulani fulani ya kibiashara ikienda sambamba na sheria yetu ya *PPP*. Maana yake ni kwamba *private sector* ishirikishwe. Mradi kama wa Liganga na Mchuchuma, Serikali ni lazima iweke fedha au itoe *guarantee,* na vitu kama hivyo, na sheria inaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, turudie falsafa hiyo ili tuone namna ya kufanya ili Serikali iweze kuchochea uchumi kwenye sekta hii ya biashara kidogo na watu binafsi waweze kwenda kwa urahisi. Ninaamini kwamba hiyo ndiyo njia pekee ya kuanza kuona miradi mikubwa mikubwa na ile ya kimkakati inachukuliwa hata kwenye sekta binafsi, Serikali iweke fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwuliza Mheshimiwa Waziri aseme, kwamba katika bajeti hii ni kiasi gani cha fedha tutaiona inaelekezwa kwenye miradi ya Serikali ya biashara ambayo inaendeshwa kwa mkakati wa *PPP* ambayo tumeona kwamba kule Serikali imeweka? Kwa mfano, kule kwenye mabenki kule imeweka 25%, lakini wanapata fedha nyingi sana. Vilevile uendeshaji wa mradi ufanyike *efficiently* na watu ambao wanajua na wanajali fedha yao waliyoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwamba, kusema kweli mimi naunga mkono bajeti hii, na ninaamini kwamba Wizara hii

itafanya mabadiliko makubwa kwenye utekelezaji wa miradi ya Serikali na kwenye kubuni dira zetu na mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles. Tunaendelea na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga na Mheshimiwa Dkt. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara hii ambayo kwa kweli imefanya kazi kubwa kwenye kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutafakari, kuona na kuamua kwamba hii ni Wizara muhimu; na kwamba, badala ya kuwa ni idara, iwe Wizara muhimu ambayo ndiyo kiini na ndiyo nguzo yetu kama Taifa na kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hili. Haya ni maono makubwa sana. Pamoja na kwamba nyuma ilikuwepo, lakini kuanzisha kwake tena maana yake ni kuona umuhimu wa Wizara hii. Siyo hilo tu, na kuona ni wataalamu gani wanaweza wakatusaidia ili kutuondoa tulipo na kutufikisha mbali zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake; kwa kweli wameanza vizuri, nami kama miongoni mwa Wabunge, napenda niwapongeze sana kwenye hili. Siyo hilo tu, ni pamoja na kuteuliwa na kuanza kufanya kazi, kwa sababu wanasema unaanguka halafu unakwenda mbio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hii ni kazi kubwa. Amesema Daktari pale kwamba anatua halafu anakwenda mbio. Nao wamekuja na kukamata mipango, mipango hii ambayo kwa

kweli inaonekana kabisa ni mipango ambayo imeamua kulisaidia Taifa, kazi yao ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda kwenye mpango wao wa maendeleo, pale unakuta kwamba kuna miradi 9,711. Kati ya miradi hii, miradi 17 ni miradi ya kielelezo yenye kulenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sababu hii siyo miradi midogo, ni miradi 9,711. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba Taifa sasa limeamua kukimbia kwa kasi, nao wataalam wetu wamekubali kabisa kuifanya kazi hii. Siyo hiyo tu, maana yake wamekubali sasa kutekeleza ilani ya chama chetu, lakini vile vile kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2021 hadi 2025/2026. Hii ni kazi kubwa sana, tumeona matokeo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unikubalie kidogo ninukuu ili iweze kwenda kwenye vichwa vya watu vizuri. Katika mwaka 2019/2020 kwenye uzalishaji wa umeme tulikuwa na *megawatt* 1602, lakini leo tuna 3077 ambalo ni ongezeko la 63%. Hii ni kazi kubwa sana, wamekwenda kwenye mradi wa umeme vijijini, tumetoka 8,587 mpaka 12,318, ambayo ni ongezeko la 100%. Hii ni kazi kubwa sana. Upatikanaji wa huduma za maji vijijini, tumekwenda kuongeza 94% kutoka 70% mpaka 85%. Hili ni ongezeko kubwa ambalo Serikali hatuna haja ya kujificha, lazima tuipongeze kwa kazi kubwa sana. Uwekezaji kwenye *TIC* kutoka miradi 207 mpaka 600, ongezeko la 150% kwenye hili ni lazima tuipe pongezi Serikali, na tuombe iendelee kwa sababu sisi tunahitaji kutoka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiyo naomba niipongeze Wizara kwa usikivu. Mwaka 2024 tuliwaomba wataalamu wetu waanze kujiandaa ili tuondoke kwenye mfumo wa madeni makubwa. Leo wamekuja na mpango mzuri ambao mimi nafarijika, kwamba wamesema katika bajeti ya mwaka 2025/2026 wanakubali kutenga shilingi bilioni 19,471.41, sawa na ongezeko la 34%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hiyo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 13,320.51 na fedha za nje ni 6,150. Ukipanga kwa hesabu za haraka haraka maana yake ni kwamba kwa nyongeza hii Serikali inakwenda kuondokana na utegemezi kwa 68%. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini sana kwa jinsi ambavyo wamejipanga, watakubali kuendeleza jitihada hizi ili tufikie mahali tuondoke kwenye hii 32 ya utegemezi ya mikopo, turudi sasa angalau ile ya kawaida kati ya tano mpaka 10; lengo tuweze kujitegemea kama Taifa kwa sababu uwezo huo tunao, rasilimali tunazo na watalaamu wetu tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba kwa jitihada zao na kwa kuelewa kwamba jukumu lao ni kuliondoa Taifa hili kwenye mikopo chechefu, kulifanya Taifa hili liweze kujitegemea, mimi ninaamini kwamba tutafika vizuri. Ninaamini pia kwamba siyo kipindi kirefu kijacho watatuambia kwamba Taifa letu ni baada ya muda gani tutaondokana na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya msingi, dunia imeanza kuondoka kwenye hoja ya kukopa na kukopesha. Sasa duniani kila mtu anajipa yeye kama yeye atajitegemea vipi, kwa sababu wameanza kujitoa kwenye miradi mbalimbali na sasa wanakuja kwenye Taifa moja moja. Sisi tujiandae kwa sababu nina hakika hawa watu watatuacha mkono siyo siku nyingi zijazo, kwamba hatuna uwezo wa kusaidia mjitegemee wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naamini Mheshimiwa Waziri analiona, analielewa, na ninaamini atafanya jitihada na wataalamu wake ili kutuondoa kwenye utegemezi wa miradi yetu, kwa maana ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiyo, naomba sana kwamba ipo *phenomena* ya kufikiri kwamba Serikali inatakiwa ikae mbali ili kuacha biashara au wafanyabiashara wafanye biashara sisi tukiwa tunasimamia sera tu. Naomba kwenye hili pia Serikali iangalie kwamba tukiendelea na hili nasi tukiamua kukaa mbali, ipo siku wafanyabiashara hawa watatuongoza na watafanya wanachokitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wenzetu wataalamu wa mipango walione hili. Zipo sekta ambazo Serikali haziwezi kukaa mbali. Kwa mfano, sekta ya mafuta, kwa maana ya biashara ya mafuta, katika suala la kuingiza na kuuza, Serikali tusikae mbali. Kama ambavyo hatukukaa mbali kwenye chakula, tunayo akiba ya chakula, naomba kwenye hili Serikali iliangalie na tusikae mbali kwa sababu ipo, wata-*detect terms,* na sisi tutakuwa hatuna nafasi, kwamba itakuwa ni lazima tukubaliane nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa maana hiyo hiyo, naomba sana, mipango yetu ni mizuri, tunafanya kazi. Hata hivyo, ukiangalia kwenye taarifa ya *CAG* utagundua kwamba zipo fedha nyingi ambazo zinakusanywa, lakini haziji kwenye mfumo wa Serikali. Kwa hiyo, kwenye mipango yetu sisi kama Wizara ya Mipango, maana yake tunapanga, lakini hatuendi kuona mwisho matokeo yake yakoje kwenye kila tulichokipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kwenye suala la kupanga, tutakusanya nini? Nani akusanye nini? Naomba kwenye hili, mkono wao uwe mrefu ili kujua kila tunachokipanga kinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, wala hakiingii kwenye mifuko ya wajanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia kwenye Taarifa ya *CAG* fedha nyingi sana haikuingia kwenye mifuko ya Serikali, kwa hiyo, inatuondoa kwenye mipango yetu kama Serikali kuhakikisha kwamba tulichokipanga ndicho tunachokikusanya na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyuma kule tulizungumza hoja ya mifumo. Mwanzoni tulisema mifumo isomane. Sasa tuondoke kwenye mifumo kusomana, tuondoke kwenye usimamizi wa mifumo na kuhakikisha kwamba mwanzo mpaka mwisho hakuna mtu katikati hapa anayeweza ku-*temper* ili akachezee fedha ya Serikali kwa anavyotaka yeye, kwa sababu hili linatuweka vibaya na linaifanya Serikali isiweze kutimiza malengo yake kwa sababu wapo wajanja hapo katikati ambao wao wanadhani kwamba mifumo ni yao na hivyo wanaichezea wanavyotaka na hatuna namna ya kuwashika. Naomba sana kwenye hili tujipange na

tuhakikishe kwamba wanachokipanga hakuna mtu anaye-*temper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa siyo kwa umuhimu wake, Wizara ya Mipango ya Mheshimiwa Waziri inapanga kila kitu. Siyo mapato na matumizi tu, hata amani yetu, Wizara yake inatakiwa ipange na iweze kuhakikisha kwamba kinachopangwa kinatekelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumesikia hapa kwamba kuna kelelekelele kidogo juu ya mambo ya uchaguzi. Sasa mimi naomba sana kwenye hili, na mkono wao uwepo ili twende sambamba kwenye mipango ya uchumi na mipango ya amani ya Taifa letu ili kila mmoja akae kwenye mstari, ili kuhakikisha kwamba hii siasa pia ni sehemu ya mipango yao wasiiachie, kwamba ni lazima apange fulani, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hii ni mipango ya Taifa letu, kwa sababu Taifa ambalo halina amani haliwezi kuishi wala ku-*survive* kwa muda mrefu. Ni lazima wapange kwenye uchumi na kwenye utaratibu wa kuhakikisha kwamba Taifa letu linaishi kwa usalama na amani, na vyama vyote vishiriki na kuhakikisha kwamba vinaongozwa kwenye taratibu, kanuni, na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Zahor na kwa kujali muda. Sasa namwita Mheshimiwa Janeth atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Ng’wasi Damas Kamani ajiandae.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami niungane na wachangiaji wenzangu waliotangulia kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameimarisha mahusiano ya kidiplomasia kwa nchi mbalimbali na amehamasisha uwekezaji kwenye Taifa letu. Kama tulivyosikia

ripoti ya Mheshimiwa Waziri asubuhi hapa, tumeona miradi ya kisekta iliyosajiliwa toka mwaka 2021/2024 imefikia miradi 901.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ajira zilizotarajiwa kutokana miradi hii ya uwekezaji kutoka mwaka 2021/2024 imefikia ajira 20,674. Pia wameweza kukamalisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Mheshimiwa Rais ameweza kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Mheshimiwa Waziri huyu ni miongoni mwa Waheshimiwa Mawaziri ambao wanafikika na amekuwa msaada mkubwa sana kwa wajasiliamali hususan wanawake wa Dar es Salaam. Tumemwona, tunamwona na tunamtumia kila siku, amekuwa akishiriki makongamano mengi sana ya wanawake, anatoa mchango wenye tija, na hachagui; liwe kongamano dogo, kubwa ngazi ya kata, ngazi ya kimkoa popote anafika, ilimradi ratiba yake iwe inaruhusu, nampongeza sana. Amechangia kwa kiasi kikubwa sana wanawake wajasiliamali wa Dar es Salaam kuweza kushiriki kwenye maonyesho ya Saba Saba, na matunda yale ni mchango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, nimshukuru pia na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa Nyongo na Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Tausi Mbaga. Vilevile nimpongeze Mkurugenzi wa Kituo cha *TIC* na timu yake, wanatutendea haki sana wanawake wajasiliamali wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIC* sasa hivi imekuwa ni mahali panapofikika na mtu yeyote; wajasiliamali wadogo, wakubwa wote wanaona kituo kile ni sehemu yao ambayo wanaweza kupata ushauri na wakaelekezwa namna ya kuwekeza. Kila mtu anaona kwamba, kumbe Mtanzania yeyote ana haki ya kufika *TIC* na akapata huduma stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Dar es Salaam shughuli yao kubwa na ya msingi ni ujasiliamali; 80% ya wanawake wa Dar es Salaam ni wajasiliamali; 20% ndio wanawake ambao

wameajiriwa. Katika hii 80%, 10% ni wale wajasiliamali wakubwa, 20% wajasiliamali wa kati, na 50% ni wale wadogo kabisa wanaojitafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu utajikita zaidi kwenye Kituo cha Uwekezaji cha *TIC* na Wanawake wa Dar es Salaam. Tumeona *TIC* sasa hivi wana huduma ya dirisha moja. *TRA* utawapata pale, usajili wa makampuni *BRELA* utawapata pale, vibali vya ardhi utavipata pale. Hili ni jambo kubwa na zuri sana kwani linapunguza urasimu na linaokoa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na *TIC,* wamewezesha kupatikana kwa kituo cha biashara na usafirishaji cha Afrika Mashariki ambacho kinajengwa kwenye Stendi ya Ubungo ya zamani. Kituo hiki kinasimamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa kushirikiana na Kampuni ya *Linghang Group* kutoka China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mradi wa usafirishaji kwa ajili ya bidhaa kutoka China na kwenda nchi mbalimbali za Afrika Mashariki. Mradi ule utakuwa na maduka zaidi ya 2000 na utakuwa na mchango mkubwa hususan kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwani utaongeza mapato kwenye halmashauri zetu, utatengeneza ajira kwa wananchi, utapunguza msongamano wa wajasiliamali wadogo, wa kati na wakubwa katika Jiji la Dar es Salaam, hususan maeneo ya Kariakoo na pia utasaidia kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mradi huu utakapoanza, maduka haya 2000 *plus* tukawaone wajasiliamali wadogo, wa kati na wakubwa wote wawe pale. Kuna wanawake wengi sana pale Dar es Salaam ambao wamenufaika na mikopo ya halmashauri; wana biashara zao, lakini wengi wanakosa maeneo ya kufanyia biashara. Basi tuwaone hata hawa wadogo na vijana wakapate biashara katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba mradi huu utakapoanza mjasiliamali yeyote mwenye mtaji, hata wa shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni 10 atakuwa ana uwezo wa kupata bidhaa kama mtu aliyesafiri kwenda China. Kwa hiyo,

tumwombe Mheshimiwa Waziri, mradi huu utakapoanza asichaguliwe watu wakubwa tu wawe wafanyabiashara wa aina fulani, tunaomba wajasiliamali wote wapate nafasi pale, hususan kundi la wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ombi langu katika Kituo hiki cha Uwekezaji cha Ubungo, natamani kuona kinakuwa na tija kwa wanawake wa Dar es Salaam, lakini pia, kuwe na ushirikishwaji wa wanawake katika mipango ya maendeleo kwa ngazi zote kuanzia Kata mpaka Taifa. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kupata michango mbalimbali, maoni ya akina mama lakini kujua sehemu gani wanatakiwa wawekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nilikuwa na ushauri kwa hawa ndugu zetu wa *TIC,* kwamba tumeona kliniki mbalimbali ambazo zinaanzishwa namna zinavyoleta matunda mazuri kwenye Taifa letu. Tumeona Kliniki ya Ardhi, tumeona hii Kliniki ya Mambo ya Kisheria*, Samia Legal Aids,* inafanya vizuri sana kwa kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *TIC* waje na kliniki kwa ajili ya uwekezaji, na kliniki hii, tunaomba ianzie Mkoa wa Dar es Salaam, kwa sababu ndiyo una wanawake wengi wathubutu, wajasiriamali na wapambanaji. Ninaamini Dar es Salaam itakapoanza, itakapofanya vizuri mikoa mingine itafuatia, lakini mkoa ambao ni *pilot* wa mfano tuanze na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kliniki hii tui-*categorize* katika vikundi. Dar es Salaam kuna vikundi vya chini, vya kati na kuna vikundi vikubwa. Vikundi vikubwa vya Dar es Salaam wanawake wanaweza kukopeshana wenyewe shilingi milioni tano mpaka shilingi milioni 50. Wanawake hawa tayari wana mtaji, waongezewe jicho la kuangalia sasa ni wapi wanawekeza? Tunatamani kuona kampuni na wawekezaji ndani ya Taifa letu wanaotokea kwenye makundi ya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia hii kliniki, najua kutakuwa na *programme* za *mentorship* ambazo zitasaidia kuwasimamia wanawake hawa wajasiriamali waliokwishathubutu,

waliyooneshwa fursa na walikwishaanza na kuwapima kuona wanatoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makundi haya ya wanawake, kuna wengine tayari ndani ya vikundi vyao wana vikampuni vidogo vidogo. Dar es Salaam kuna kampuni na viwanda vingi sana. Tunatamani sasa kupitia kliniki hizi watu wa *TIC* wawasaidie akina mama hao wenye vikundi ambao wana viwanda vidogo vidogo, kampuni za usafi na mambo mbalimbali, wasaidiwe kupata kazi kwenye kampuni kubwa. Kampuni kubwa na kazi za usafi wasizipe kampuni nyingine kubwa ila wawape akina mama ili mitaji yao ikue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanapata mikopo kwenye halmashauri, pesa zile zinapotea. Siyo kwamba wanagawana au zinapotea makusudi, hakuna mtu mwenye ndoto ya kushuka chini. Kila mtu ndoto yake ni kupata mtaji na kukua, lakini tuwaoneshe ni wapi wawekeze ili mitaji hii iweze kuzaa matunda na fedha hizi ziweze kuzunguka zikasaidie wanawake wengine ili kila mmoja anufaike na hii keki ndogo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pale tuna Kiwanda cha Bakhresa, wanawake wa Dar es Salaam hatulimi, lakini tuna uwezo wa kutafuta mazao na kuyaleta kwenye kampuni, tukapewa hizo *tender*, Wanawake wa Dar es Salaam tunaweza. Tunawaomba *TIC,* wawekezaji wakubwa, kampuni na viwanda vilivyopo ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam tuwatafutie kazi wanawake wawekezaji wa kwenye vikundi, wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kukopeshana wenyewe kwa wenyewe tayari wanazo, kiu yao kubwa ni kuona sasa wanapata mahali pa kuwekeza miradi mikubwa. Tumeona ndugu zetu wa *TIC* mnasaidia mpaka upatikanaji wa ardhi. Dar es Salaam kikundi kimoja kina uwezo wa kununua ardhi hata shilingi milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke kliniki waoneshwe wakawekeze wapi? Wafanye nini? Wajenge viwanda gani? Tutainua ajira, tutaongeza ajira hata kwa vijana wetu, na ajira

kwetu sisi akina mama. Siyo kwamba tunafurahi sana kundi la 80% kuwa wajisiriamali, tutengeneze ajira. Hata hao 20% ambao wameajiriwa nyingine tutengeneze wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu kubwa kwa watu wa *TIC* kuhusu hii kliniki ambayo nimeiomba sana, ianzie Dar es Salaam, pia ijikite kwenye kutoa programu mbalimbali za mafunzo ya uwezeshaji. Wajasiriamali wengi wadogo hawakui sababu ya kukosa elimu na maarifa. Mtu anakopeshwa pesa, akishapata pesa ndiyo anaanza kujifunza afanye nini? Tubadilishe huu utaratibu na kliniki hizi ziwashirikishe halmashauri zetu, Bibi Maendeleo, Maafisa Mipango na Maafisa Biashara wa Halmashauri. Kule halmashauri wanavijua vikundi ambavyo vimenufaika na fedha nyingi. Kwa hiyo, kupitia mikopo ile ambayo tunajua halmashauri fulani ina vikundi labda 20 wamepewa fedha ambayo ni kubwa, waingizwe kwenye mpango huu wa kliniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuone viwanda na kampuni za wawekezaji za wanawake ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam na hili linawezekana; na kama wasiwasi ni kujua kwamba watavipata wapi hivi vikundi, mimi nipo muda na wakati wote. Nitawaweka pale, tutakaa mezani, kwa sababu nimeshakaa mezani na watu wa *TIC* muda mwingi sana, tumeshakaa sana vikao vingi, mimi binafsi nimeshajifunza, nimeshapeleka akina mama wengi sana, lakini sina uwezo wa kubeba vikundi vyote, ila tukitangaza hii kliniki tutawasaidia wanawake wengi sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, programu hizi ziende mpaka kwenye redio, *TV* na *social media,* kwa sababu tumeona elimu ya mlipakodi unaisikia kwenye redio, unaisikia kwenye *TV,* watu wanajifunza. Mtu anaweza asielewe leo, lakini akarudia mara mbili, mara ya tatu akaelewa. Watumie media kutangaza programu mbalimbali, watu wajue faida wanazoweza kuzipata kupitia Kituo hiki cha Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanawake wa Dar es Salaam ni wanufaika wakubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth, muda wako ulishakwisha.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Janeth. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuata Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, kisha Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KAKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Wizara hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia wasaa huu, na pili niwape pole Wakatoliki wa Tanzania na Dunia nzima kwa kuondokewa na Baba na Mlezi wa Kanisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara, namshukuru Rais wetu, aliyeliona hili na kuanzisha hii Wizara muhimu sana. Nadhani Mheshimiwa Prof. Kitila pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, watakuwa wamekisoma kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisome, ingawa imeandikwa kwa Kingereza, Mwandishi Daron na James Robinson katika Kitabu cha *Why Nations Fail: The Origin of Power, Prosperity and Poverty,* wameandika maneno yafuatayo: "*Most economist and policy markers are focusing on getting it right while what is really needed is an explanation for why poor nations get it wrong.*" Naishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzisha Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji, ni maelezo tosha ni wapi tulikuwa tunakwama, nina hakika kwa kuanzisha Wizara hii mambo ambayo yalikuwa na mkanganyiko katika kukuza uchumi wetu, sasa yatapata suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Kimei, wakati anachangia hapa, alisema kuna eneo utakuta wanalundika miradi na sehemu nyingine hakuna miradi. Nadhani

suluhu ni Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji, sasa waje kutoa suluhu ya wapi panahitaji uwekezaji mkubwa na ni wapi panahitaji aina fulani ya uwekezaji upelekwe sehemu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mpya, naishauri Serikali yetu iipatie watendaji wa kutosha wenye weledi mkubwa ili wakatusaidie kuweka mipango na kufanya uwekezaji. Itusaidie Taifa ni wapi pa kupeleka pesa? Ni wapi pa kupeleka vitu gani na wapi pa kupeleka vitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi ambayo wamefanya, na nitajikita kwenye Ofisi ya *TR*. Ofisi ya *TR* ndiyo *engine* ya kusukuma uchumi wetu mbele, lakini nimechangia zaidi ya mara tano hapa Bungeni. Ofisi ya *TR* inaanzishwa na Sheria ya Msajili wa Hazina, Madaraka na Majukumu Sura ya 370. Kazi za Ofisi ya *TR*: inaanzisha ofisi, lakini madhumuni yake ni utoaji *(acquisition),* umilikaji *(holding),* usimamizi *(management)* ya mashirika yote ya umma ambapo Serikali imewekeza trilioni za pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya mwisho hapa Bungeni inaonesha kwamba uwekezaji katika mashirika ya umma ulikuwa umefikia shilingi trilioni 75.79. Ni trilioni, siyo bilioni; ni trilioni za pesa na kwa mwaka ripoti hiyo inaonesha ongezeko la faida kwenye hizo shilingi trilioni 75.79 ni asilimia tatu tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mtaji na uwekezaji ambao umefanywa na Serikali ya Awamu ya Sita na Serikali zilizoitangulia ni mkubwa mno ukilinganisha na faida tunayoipata. Tuna tatizo, ninalirudia, nimeshawahi kuchangia, na leo ninalirudia. Sheria inayoanzisha Ofisi ya *TR* ni kongwe, haiendani na uchumi wa sasa. Hatuwezi kutengeneza faida kwa sheria kongwe namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wajibu wa kulisaidia Taifa hili, na kuisaidia Wizara hii changa. Tuletewe hii sheria, tuifanyie marejeo na kama itawezekana tuifute na kutunga sheria mpya itakayoendana na ukuaji wa uchumi wa sasa wa Taifa letu, ili haya mashirika ambayo Serikali imewekeza trilioni za walipakodi wa Tanzania iweze kutupatia faida kubwa ambayo tutaitumia

sasa kujenga vituo vya afya, kujenga zahanati, kumalizia maboma ya shule za msingi na sekondari na kulipa mishahara mizuri ya wafanyakazi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba hiyo haitoshi, tumewekeza pesa nyingi kwenye mashirika ya umma, lakini ukiangalia yale mashirika ya umma ambayo tunayamiliki zaidi ya 51% na yale mashirika machache ambayo tumewekeza kupitia *PPP* (ubia) yale ambayo sisi tunayamiliki kwa 100% utengenezaji wa faida ni mdogo sana, ukilinganisha na yale machache ambayo tunashirikiana na sekta binafsi katika kuyaendesha. Hii inatupa picha kwamba kuendesha mashirika ya umma ni hasara na ni mzigo kwa Serikali. Kwa hiyo, kwa hii sheria ambayo mimi naipendekeza, mashirika yote tungekaribisha sekta binafsi, tukaendesha na sekta binafsi ili tukatengeneze faida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, nimesikia na wakati wa semina ya watu wanaolima parachichi, Mheshimiwa Waziri Bashe alituambia pale kwamba Serikali inao mpango wa kuanzisha benki ya ushirika ili ikatoe mikopo kwa wakulima hasa wakulima wale wadogo wadogo ambao ni vigumu sana kupata mikopo kutoka kwenye Benki za Biashara. Hiyo ni hatua kubwa sana na ninaomba hiyo benki ifungamanishwe na Wizara hii iweze kutusaidia hasa sisi tunaotoka vijijini kuwasaidia, kuwapatia mikopo hawa wakulima wenye kipato kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ambako tunalima kahawa, na ninadhani Wilaya ya Muleba, inaongoza katika ulimaji wa kahawa kwa Mkoa wa Kagera na kwa Taifa hili. Tatizo kubwa na kilio kikubwa cha Wakulima na Wafanyabiashara wa Muleba ni mikopo. Kila mara nikienda jimboni wanakuja kunililia, tunapata wapi mikopo? Mazingira ya kupata mikopo kupitia benki za biashara ni magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali yangu, namshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa kuliona hili. Wanapoanzisha benki ya ushirika itakuwa suluhu kwa mikopo ya wafanyabiashara na wawekezaji

kwenye sekta ya kuongeza mnyororo hasa kwa mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye wilaya yangu pekee, nina kampuni zisizopungua tano ambazo zinaongeza thamani kwenye zao la kahawa. Kwa ufupi, naomba niyataje, hata Waziri anapokuwa anapokuja kuhitimisha, atupatie neno, hawa watapewaje kipaumbele katika kupata mikopo kupitia benki yetu ya ushirika? Tuna Kampuni inaitwa Atadars pale Muleba wanafanya kazi kubwa na nzuri ya kununua na kuongeza thamani kwenye zao la kahawa. Tunao *Kyeju's Coffee,* tunayo *Hakika Coffee*, *Johansen Coffee* na kampuni nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kampuni zote zinahitaji kupewa mikopo zikakue, yakachakate kahawa, yakaongeze thamani, lakini zaidi, yakaajiri watoto wetu na vijana ambao tulikuwa tunalia na ajira kwenye Wizara iliyotangulia na ndiyo suluhu pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiziwezesha hizi kampuni changa, ambazo ni za wananchi wa kawaida wazawa wa Kitanzania, Wananchi wa Muleba na kwingineko, tunatengeneza *base* kubwa ya kupata ajira, kodi na pesa ya kigeni. Mheshimiwa Waziri, naomba tukayaangalie haya, tukawasaidie hawa ambao wamejitoa mhanga kujenga uchumi kupitia kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao ambayo yanalimwa na wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Taasisi yetu ya Tume ya Ushindani, kama tunataka kujenga uchumi sawia na uchumi jumuishi, tuna matatizo katika nchi, lakini Tume ya Ushindani ilianzishwa kwa ajili ya kuchochea ushindani katika viwanda na katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri Tume ya Ushindani ingeletwa kwenye hii Wizara ya Mipango na Uwekezaji ikatusaidia kuchochea na kuchagiza ushindani katika mizania ya uwekezaji na mipango yetu ya kujenga uchumi wa Taifa hili. Ikalinde ubunifu, ikalinde hatimiliki za kibiashara na kuwekeza katika mizania ya kibiashara sawia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru viongozi wetu wa Wizara hii changa na ninaunga mkono hoja. Nawatakia kazi njema ya kubuni mipango sahihi na kuleta uwekezaji ambao utainua uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Oscar. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

**MHE. NGW'ASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na watumishi wote wa Wizara hii kwa utekelezaji mzuri au uwasilishaji mzuri wa mpango uliyofanyika hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu tangu mwaka 2021 mpaka mwaka 2024 tunapozungumza sasa hajatekeleza tu mipango ile ambayo ilikuwa imepangwa, lakini ameenda mbele zaidi kutekeleza hata ile ambayo hatukuwa tumeipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napongeza kwa sababu uwekezaji ndani ya nchi yetu umeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Tunavyozungumza sasa hivi uwekezaji huu kutoka nje kuingia ndani, umeongezeka na umeonesha *impact* yake katika ajira kwa vijana. Mwaka 2021, uwekezaji wa nje ulikuwa unazalisha ajira takribani 53,000 kwa mwaka, lakini tunavyozungumza sasa mwaka 2024 tunazungumzia zaidi ya ajira 212,000 kutokana na uwekezaji wa nje. Kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uwekezaji huu haujafanyika tu au haujaletwa tu kutoka nje kuingia ndani, lakini pia uwekezaji wa Serikali ndani ya nchi yenyewe katika kila sekta umeongezeka mara dufu. Kuna msemo unaosema, *"Ambaye hakumwona mama yake akiwa kijana, atahisi baba yake alipoteza ng'ombe,"* kwa sababu wale wanaobeza yanayofanyika katika Serikali sasa

hivi, labda tuwakumbushe kwamba kule tulikotoka, tumetoka katika hali ambayo kwa sasa tuko mbele kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu ni wa kipekee zaidi kwa sababu moja, tunatimiza ule Mpango wa Miaka Mitano tuliopanga kuanzia mwaka 2021 mpaka mwaka 2015 wakati Bunge hili likiwa linaanza. Mbili, tunatimiza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu tukajitafakari kwamba katika mipango hii wapi tulipotoka na wapi tulipo ili twende mbele. Naipongeza sana Serikali kwa sababu tumetafakari kwa kina hasa katika utengenezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia maendeleo ya nchi, hatuwezi kuacha kuwazungumzia vijana na bahati nzuri hivi karibuni tumefanya sensa na imetuonesha zaidi ya 60% ya wananchi katika nchi hii ni vijana kwa maana ya kwamba Taifa hili ni Taifa changa, na changamoto namba moja ya kijana yeyote wa Kitanzania ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele yetu itabaki pale pale. Tunajua kwamba hili ni janga la kidunia, lakini katika nchi yetu naipongeza sana Serikali kwa sababu kwa kipindi hiki cha tangu mwaka 2021 mpaka tunavyozungumza sasa, jitihada zimefanyika na vijana tumeziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa kupitia diplomasia ya Kiuchumi iliyojengwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Taifa letu limeweza kuwapeleka nje na kuwatafutia nafasi ya kazi vijana zaidi ya 7,000 tunapozungumza sasa, lakini ajira zinazozalishwa kutokana na uwekezaji huu unaofanywa na Serikali ni nyingi na ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya ajira 40,000 zimetangazwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamshukuru. Hata zile ajira zisizo za moja kwa moja zinazozalishwa na uwekezaji katika sekta binafsi, kupitia mazingira bora yanayoendelea kutengenezwa, bado ni nyingi na kwa kweli tunaipongeza Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bado tuna mengi ya kushauri. Kuna *article* moja inaitwa, *Unemployment Crisis in Tanzania, should the Government be Blamed; or are the Youth a Burden to the Nation?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Kitila nitakutumia hii pia uipitie, ni nzuri sana. Mimi najaribu kusema, tukizungumzia changamoto ya ajira kwenye nchi hii, wengi wetu tunazungumzia zaidi tatizo la mifumo iliyopo kwenye elimu. Naipongeza Serikali kwa sababu, tumefanya mapitio makubwa sana ya mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tulilalamika juu ya mfumo wetu kuwa *more theoretical,* sasa tumebadilisha na mfumo wetu umeenda kuwa *more practical,* kumuandaa kijana kwenda kupambana na changamoto, lakini tunazidi kutoa changamoto kwamba, je, tulivyobadilisha hii mifumo yetu ya elimu maana yake tatizo la ajira ndiyo litakwisha katika nchi yetu? Je, hiyo ndio ilikuwa changamoto pekee katika nchi yetu kwenye ukosefu wa ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hii changamoto nikitoa vitu vingine vitatu ambavyo naamini pamoja na kwamba, mabadiliko katika mfumo wa elimu au elimu bora itamrahisishia kijana kuweza kupata ajira au kujiajiri, lakini haitam-*guarantee* kwamba, atajiajiri au kuajiriwa. Kwa vile haim-*guarantee,* kuna vitu ambavyo pia ni lazima twendenavyo pamoja kwenye mipango yetu, ili tuweze kutengeneza mazingira bora ya kijana wa Kitanzania kujiajiri au kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, uchumi wa nchi. Kijana hata akipata elimu iliyo bora kiasi gani, kama uchumi wa nchi haupo *stable,* maana yake yule kijana hawezi kubadilisha ujuzi au elimu yake kuwa rasilimali. Maana yake ni muhimu tukaendelea kuchanganya akili zetu, kuendelea kuhakikisha kwamba, tunakuza uchumi wa nchi hii ili kufikia viwango ambavyo tunafikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinasema, ili nchi iweze kuwa na uwezo wa kuhudumia au kutoa huduma zile muhimu

kwa wananchi wake, ni lazima makusanyo ya kodi yachangie *GDP* ya Taifa zima kwa kuanzia 15% na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zetu za Afrika, bado nyingi zipo kwenye 7% – 12%, hatujafikia hata hiyo15%. Maana yake ni uwezo wa nchi nyingi wa Serikali kuhudumia wananchi kikamilifu, bado ni mdogo. Leo hii kwenye sensa tumeambiwa, Watanzania tupo zaidi ya 61,000,000 lakini tulikuwa tuna *tax base* ya watu 3,000,000 tu, na juzi Mheshimiwa Makamu wa Rais ametoka kutuambia kwamba, *tax base* hiyo inazidi kushuka, maana yake tupo kwenye 2,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani *tax base* ya watu 2,000,000 ikahudumia watu 61,000,000 hawezekani. Ni lazima Serikali yetu ije na mipango ya kuhakikisha tunaongeza *tax base,* watu walipe kodi, ili nchi hii iweze kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kushauri katika hili Bunge na nitashauri tena kwamba tuondoe mfumo wa fedha za makaratasi, tuweke mfumo wa fedha za kidijiti *(Cashless Economy)*. Mheshimiwa Waziri, wewe umetembea nchi nyingi zilizoendelea, hawatumii fedha za makaratasi, ni kwa nini? Kwa sababu, Serikali inatakiwa itambue *transactions* zote zinazofanyika katika nchi yake. Hii itasaidia kupunguza kiwango cha kodi na kutoa elimu kwa kila mmoja kuweza kuchangia katika keki ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi nina hii kalamu hapa, Serikali haijui nimenunua wapi? Kwenye mifumo iliyo thabiti, Serikali inatakiwa kujua hata hii kalamu nimeinunua wapi? Kwa shilingi ngapi? *VAT* imelipiwa kiasi gani? Hiyo ndiyo mifumo ambayo itatusaidia kukusanya fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, hata jana Waziri wetu wa Utumishi amezungumza kwamba vijana wengi wanalalamika pamoja na kwamba, uchumi wa nchi umekua nao wanauona, lakini kwa nini ajira haziongezeki? Ni kwa sababu, hatuja-*translate* kukuza uchumi wetu kuingia kwenye *wage bill* yetu. Tukiongeza makusanyo, maana yake tutakuwa na uwezo wa kuhudumia

wananchi na kuajiri vijana walio wengi. Kwa hiyo, hii itasaidia sana kuondoa vijana wengi mtaani, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni mahitaji ya soko dhidi ya maarifa aliyonayo kijana. Hata kama kijana ana elimu bora kiasi gani, kama ile elimu yake haipo *marketable* kwa wakati huo, haiwezi kumfaa. Nitoe mfano mdogo, *let say* kuna fundi, ambaye ni *excellent* kabisa kwa kutengeneza feni, lakini dunia imebadilika sasa hivi, kila mtu anatumia *AC,* ufundi wake hautusaidii. Ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *statistics* zinazoonesha kwamba, sekta binafsi inasema, vijana tunaowatoa kwenye vyuo vyetu maarifa waliyonayo siyo yale wanayohitaji wao kwenye ajira. Maana yake ni kwamba, tutakuwa na vijana wengi, lakini sekta binafsi haiwezi kuwameza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mwingine. Naishukuru sana Serikali yetu, tulipata nafasi ya kupeleka vijana madereva zaidi ya 200 kwenda katika nchi nyingine kwa ajili ya kufanya kazi. Tena tumepeleka vijana walio *cream,* waliopata elimu kupitia *NIT,* vyuo vyetu, lakini kufika kule imebidi wapewe elimu nyingine. Kwa nini? Ni kwa sababu, elimu waliyonayo imekuwa *outdated*. Wanatakiwa kupewa elimu nyingine kwa ajili ya *ku-operate* vyombo vilivyokuwa na teknolojia iliyo juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake, ni lazima *tu-update* mifumo yetu. Kama ni *VETA* maana yake ni elimu ya ufundi tunayoitoa iendane na mazingira. Leo hii tunatakiwa pia, *tu-invest* kwenye *career guidance*. Naweza kuhoji kwamba, Mheshimiwa Waziri, katika kutengeneza mipango yetu, je, tukianza kuwahoji wanafunzi wote waliopo vyuoni kwamba, wewe unasoma ualimu, kwa nini umechagua kusoma ualimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio wengi wanaoweza kutuambia ni kwa nini amechagua *career* aliyochagua. Wengi watakwambia ni kwa sababu kulikuwa na mkopo, au kwa sababu, niliambiwa nikasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa *ku-invest* kwenye *career guidance* ili katika mipango yetu ya Taifa tujue kwamba, kwa sasa sekta ambazo zipo *booming,* labda kuna sekta ya *logistics,* kuna masuala ya gesi na utalii, ili vijana wajiandae wakiamini kwamba, sekta hizo ndipo maendeleo ya nchi yanapoelekea. Hata kijana akipata elimu bora, iwe bora na *relevant* kwa mazingira yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, jambo la tatu ambalo tunatakiwa tuliangalie, pamoja na kuwa na elimu bora, ni fursa za ajira. Kama kijana akiwa na elimu bora, lakini hakuna fursa za yeye kujiajiri kwenye eneo husika, maana yake ni kwamba elimu yake haiwezi kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Keki ya Taifa hili ni ndogo, wote tunajua, na tunaigawana hivyo hivyo kwa udogo wake. Vijana wa Tanzania wanajua fika kwamba, Serikali haiwezi ikawaajiri wote, hilo wanajua, lakini wanachohitaji ni matumaini ya kesho kwamba, kama sijapata leo, basi nitapata kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna mifumo mizuri sana ambayo Serikali imeianzisha, inayosaidia watu kuomba tenda za kazi mbalimbali kwenye halmashauri zetu. Wote tunajua kwamba, hii bajeti tunayoipitisha hapa zaidi ya 60% inarudi kwa wananchi kupitia halmashauri zetu kwenda kwenye miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hizo *tendering* utakuta kuna kampuni iliyopo Dar es Salaam ina tenda Njombe, Mbeya, Mwanza, karibu barabara 20 kwenye nchi moja. Unajiuliza, leo hii Chama cha Mapinduzi na Serikali yetu imetoa elimu bure, kuna wasomi kila sehemu. Ni kwa vipi kampuni inayotoka sehemu moja ikaenda ikatenda zote hizi? Kwa nini tusiweke ukomo ili hii keki ndogo ya Taifa hili tugawane wote? Kama barabara ipo Mwanza, basi sisi vijana wa Mwanza tunufaike nayo? Kama barabara ipo Mbeya, vijana wa Mbeya wanufaike nayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kila sekta tukizungumza hapa, kama ni umeme *REA* unapelekewa kila sehemu. Maana yake ni kwamba kuna *engineers* wa umeme kila sehemu,

wafanye kazi wahusika wa eneo hilo, ili hii keki inayosambazwa na bajeti hii ya leo, mtu au kijana awe amekaa nyumbani anajua anafuatilia kwamba, Mwanza imepangiwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waanze kufuatilia jamani, Mwanza imepangiwa kwenye barabara ni shilingi bilioni tano. Maana yake anaanza kujiandaa kwamba, nimeshajua kwa mwaka huu nijiandae ku-*bid,* tutapata hiki na hiki. Watu wagawane keki hii kwa usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi au vijana wote ndani ya nchi hii wamewakilishwa na Wabunge ndani ya nchi hii. Ni nani ambaye atakubali wananchi wake yeye wakose ile keki wakati wananchi wa sehemu nyingine wanapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutengeneze mifumo ya kugawana keki hii kwa usawa. Vijana wasomi wapo kila sehemu, wapo tayari kufanya kazi, basi waweze kupewa nafasi au fursa za kufanya kazi hizo. Tuwaamini vijana wetu, tumewaelimisha kwa gharama kubwa, wanayo ari na uzalendo wa kufanya kazi. Ninaamini tukipanga mipango vizuri tunakwenda kupunguza kabisa changamoto ya suala la ajira kwa vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Mipango. Niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wale wote ambao wanafanya kazi kwenye Wizara hii. Kipekee kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakwenda mbali na wachangiaji waliotangulia. Nianze kwenye lile jukumu la *coordination* ambalo watu wengi wameliongelea kwamba, Wizara hii tulitegemea

ndiyo inaweza ku-*coordinate,* kwa maana ya kwamba, mipango ya Wizara moja na nyingine, mipango ya Halmashauri na taasisi moja na nyingine iweze kuleta matokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna mzungumzaji alisema, badala ya kuwa na idara tu yenye Mkurugenzi, ambayo itajumuisha mpaka ufuatiliaji, ni vizuri kabisa ingekuwa na mamlaka hiyo ya *coordination*, ufuatiliaji na ninadhani ingefanya kazi na Ofisi ya *CAG* kwa karibu, hata zile hoja za kikaguzi zingepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ukiliangalia kwa undani zaidi, kwenye eneo la *monitoring and efficiency,* wenzetu kule Marekani wametafuta hata mtu wa kusimamia *Government efficiency.* Sasa ni vizuri Wizara hii ipewe meno kwenye eneo hilo, la kwanza, kupanga na pia kufuatilia. Natoa mfano wa maeneo ambayo nimeenda *physically* na nimeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunatoa fedha ya kujenga madarasa, bei ya kutengeneza darasa moja hapa Dodoma, Moshi Mjini, Tanga Mjini na Dar es Salaam inakuwa sawa na kule Ulanga na Visiwa vya Mafia ambako vifaa vyote vinakuja na meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, inakuwa sawa na eneo kama Mvuha, kule Morogoro ambapo, ili ufike kule, ukiacha milima, kuna madaraja ambayo gari zaidi ya tani 10 haliwezi kupita. Sasa huyu anaweza akaagiza *cement* tani 30 na maeneo mengine ambayo yapo *remote,* sasa inakuwaje bei ya darasa moja inakuwa sawa kote? Ni vizuri hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna maeneo ambayo yamekuwa na changamoto. Kwa mfano, kuna miradi imeenda imefika mahali imekwama na haiwezi kwenda. Naweza kutoa mfano wa Ifakara ambapo tulienda tutakuta Mlimba walishajenga Ofisi ya Halmashauri kwa fedha zao za ndani, imekamilika wamepaua, lakini Serikali ikasema sasa Ofisi za Halmashauri lazima ziwe kule kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile jengo lipo pale mjini, lakini hawa nao wameanzisha kujenga jengo la halmashauri kwa hela zao na lile la Mlimba limeshapauliwa, ni mali ya Mlimba. Kwa nini Serikali isiwaambie hawa wamalizie, halafu Mlimba warudishiwe ile fedha au lile wanalojenga wao waweke kitega uchumi cha pamoja? Unaona kwamba, kuna mikwamo kama hiyo ambayo ni vizuri Serikali ikiwa na watu wa *coordination* ipewe *manpower* mpaka ngazi za mikoa na wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Moshi Mjini tuna ahadi ya kujenga Soko la Manyema, wamesema viongozi wakuu wengi sana, lakini tunasubiri fedha hiyo haijaja. Wakati tunasubiri, sisi tuna mpango wa kujenga vibanda vya kuzunguka Soko la Mbuyni. Ni kipi kina tija kwa haraka? Ni lile Soko la Manyema, tupeleke ile fedha au tuendelee kujenga vibanda Mbuyuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibanda ni 50, ni wafanyabiashara 50, Soko la Manyema lina watu 1,400. Kungekuwa na hicho kitengo cha *coordination* hili lingeweza kufanyika na likawa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kiwanda cha Ngozi, kila mara nakisemea, ni bilioni za fedha zimewekezwa, lakini hakuna muunganiko wa kiwanda kile kifanye kazi na sekta ya ngozi. Nilitoa tena mfano hapa, sekta ya ngozi nchini…

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Asenga.

**TAARIFA**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kumpatia taarifa mzungumzaji kwamba, jambo analolisema ni sahihi kabisa na tulikuwa tunaishauri Wizara kwamba, Halmashauri ya Mlimba na Halmashauri ya Ifakara zimegawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mlimba imeacha majengo yake yote ya Serikali pale Ifakara na imetembea kilometa 90 kwenda kujenga majengo mapya, kama anavyosema mzungumzaji. Yale majengo ya Serikali yamebaki pale, bado yanamilikiwa na Halmashauri ya Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Ifakara inaomba fedha tena kwa Serikali hiyo hiyo moja kujenga majengo, kumbi nyingine na kila kitu ikiwemo hilo jengo la ghorofa. Kwa hiyo, taarifa yake ni sahihi, nilitaka kumwongezea nyama hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo, kwa sababu nilikwenda ziara kule na nikaona kitu kama hicho. Kwa hiyo, hii Wizara ikifanya kazi, nadhani mambo yatakuwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongelea sekta ya ngozi. Tuna Kiwanda kile cha Ngozi, Moshi ambacho ni zaidi ya shilingi bilioni 150 zimewekezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, utangazie umma kwanza ulichopokea, halafu tuendelee.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikishazidi shilingi bilioni 200 ndiyo nitatangaza. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ngozi Nchini, tunaambiwa sisi ni nchi ya pili, kama siyo ya tatu kwa wingi wa mifugo, lakini ubora wa ngozi hauendani na hitaji la soko. Matokeo yake ni zaidi ya 90% ya ngozi ya Tanzania inachunwa ovyo ovyo, nyama inaachwa kule inauzwa *West Africa* kwa ajili ya matumizi ya chakula kwa bei ya chini, wakati hivi viwanda vya ngozi vipo hapa na vya ku-*export* vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kunatakiwa kuwe na *coordination*. Hii Wizara ya Mifugo inawezaje kuhakikisha kwamba, ngozi inayopatikana ina kiwango kwanza, cha kutumika kwenye viwanda vyetu, na kwa ajili ya *export* au *manufacturing,* badala ya hiyo inayoenda kwa ajili ya chakula ambayo inatusababishia mapato yetu yanapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Juzi tu nimeona kwenye magazeti, *LATRA* wamepitisha sheria yao na utaratibu wa kuweka *cable cars*. Sasa nafikiria *LATRA* wameweka *cable cars* kwa ajili ya matumizi ya wapi? *Cable cars* za wapi zinatengenezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kilimanjaro walipotakiwa kuweka au kulipotokea uwekezaji wa *cable car,* ulipingwa sana na *tour companies* kwa sababu, waliamini ile *cable car* inaenda moja kwa moja kileleni, kwa hiyo, wale ma-*porter* na *tour operators* watakosa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hii *cable car,* sheria walizopitisha *LATRA,* ni kwa ajili ya wapi? Mlima? Yale matatizo yote, *tour operators* walisema yangeleta vikwazo, yamesharekebishwa? Je, hii *cable car* inaweza kutumika kule Lushoto kama usafiri wa kawaida au wa kitalii? sasa ni vizuri kuwe na *coordination,* ili vitu vikifanyika viweze kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, lipo suala la *SGR* kuelekea Kaskazini. Nafikiria pia, *coordination* iende pale. Nilivyosema hii inatakiwa i-*coordinate beyond* nchini kwetu. Kwa mfano, wanasema usafiri wa reli hauna tija chini ya kilometa 1,000. Je, tunatengeneza reli itakayoishia wapi kwa Kaskazini? Haiwezi kwenda mpaka Nairobi? Je, itakuwa ina tija na ile *connection* ya kwenda mpaka Mombasa, tunaona inafaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, barabara hii inayotakiwa kuanzia Holili kwenda Singida, ambayo muda mrefu imeachwa bila kurekebishwa, kiuchumi kwa Afrika Mashariki kwa sababu ni barabara inapitisha magari yanayokwenda Rwanda na Burundi, je, ipoje? Kwa nini isipewe kipaumbele kwa sasa? Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiri hiyo *coordination* ni suala la kwanza ambalo ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni vitu ambavyo vinagusa watu wa kawaida ili kuongeza *tax base,* ambayo mzungumzaji aliyepita amesema ni watu 2,000,000. Asilimia kubwa ya waendesha bajaji na boda boda hawana leseni. Ni kwa nini hawana leseni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kupata leseni ya udereva tumeiangalia kwa mtu mwenye gari tu. Gharama ya chini kabisa ni shilingi 340,000; gharama ya shule, *learner* kila daraja na *TRA* hapo wanachukua shilingi 70,000 tu. Gharama ya madaraja haya makubwa ni shilingi 582,000, unaanzia huko huko *learner* na shule ya udereva. Hivi kweli, hawa madereva wa bajaji na bodaboda wanaogongwa, saa nyingine hawana makosa, wanashindwa kupata haki zao kwa sababu, hawana leseni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna tunaweza tukatafuta namna wakapewa leseni kwa bei nafuu, hata kama ni 50,000 hizo nyingine zote zikawa *waived* kwa sababu, bajaji na pikipiki hazifundishwi kuendesha kwa kutumia shule *(driving school)*. Watu wanafundishana tu, wanaendesha. Sasa, wakiwa na leseni hawa, kwanza tumewa-*protect,* kwenye *insurance* wanaweza kulipwa, pia tutakuwa tumewaweka *safe* na tumeongeza mapato. Ni watu wengi wamejiajiri kwenye hii hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuja wawekezaji hapa wanataka kuanzisha vituo vya kuweka *LPG (Liquid Petrol Gas)* kwenye magari. Hii ni tofauti na ile ambayo inawekwa kule Dar, ambayo ni *CNG*. *LPG* ni kama hii ya kupikia. Kwanza kubadilisha huu mfumo ni bei rahisi zaidi. Pia, gesi yake ni kama ile ya nyumbani, magari yatatumia hiyo gesi na tutapata unafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaangalia kwamba, tutapoteza hela ambayo tunapata kwenye kuagiza petroli. Sasa, Serikali inaonaje kwamba, itapoteza fedha ile ya kodi ya petroli wakati tunamwacha mwananchi na hela nyingi mkononi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni tumeongeza *spending power* ya mwananchi ambayo ita-*multiply* kwa sekta

nyingine zote. Sasa watu hawa, tena Watanzania, wameambiwa hizo *story* za porojo, wameenda Kenya wanafungua vituo vya *LPG*. Hii ya *CNG* haiwezi kusafirishwa mpaka lile bomba lifike hapo kwenye hiyo mikoa, lakini *LPG* inabebwa kwenye *tank* kama petroli na italeta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, labda niishie hapo kwa sababu, kengele imelia, lakini kuna umuhimu mkubwa wa ku-*coordinate* na kugusa hawa watu wa chini bila kuangalia hizi sheria tu kwamba, leseni sasa hivi ni shilingi 350,000/=, lazima mtu aende *driving school* wakati watu wetu wanakufa kwa kukosa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuunga mkono hoja ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri sana ambazo wamefanya katika kipindi hiki chote. Tumeona wamesimamia mipango mingi, wamesimamia uwekezaji na kuhamasisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali, lakini wamesimamia pia Mashirika ya Umma yote kupitia Msajili wa Hazina na wamesimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji (*EPZA)*. Kazi hizi ni nyingi, na ni kubwa, na wamefanya vizuri sana, tunawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali maoni yetu ambayo tumekuwa tukiyatoa muda mrefu kwamba tuwe na Wizara maalum inayosimamia mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuliposhauri kwamba iondolewe mipango kutoka kwenye Wizara ya Fedha halafu iundwe Wizara na Mheshimiwa Rais alisikia hicho kilio na akaunda hii Wizara, nampongeza sana kwa hilo na uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaendelea kushauri zaidi ya hilo, pamoja na kazi nzuri ambayo ameifanya, tunadhani kwamba Wizara ya Mipango ingesimama yenyewe, isisimamie mipango. Badala ya kuweka na uwekezaji, kuweka maeneo maalum ya uwekezaji, kusimamia Mashirika ya Umma, bado lile tatizo la kutoipa uzito mipango linabaki bado lipo palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulishauri kwamba itoke Wizara ya Fedha iwe Wizara ya Mipango. Sasa hapa nguvu utaona hata ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia masuala ya uwekezaji walivyofanya, amezungumzia masuala ya maeneo maalum ya uwekezaji nguvu nyingi inapelekwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunatamani Wizara ya Mipango iwe ni *thinktank,* kufikiria kwa niaba ya Taifa letu ili waweze kuwa na uratibu wa maendeleo ya nchi yetu. Tukiwa na uratibu wa maendeleo ya nchi yetu, ndipo tutakuwa sasa na uwezo wa kutengeneza dira ya miaka hata 100 ijayo, miaka 50, miaka mingapi na hiyo dira ndiyo itaweza sasa kuunganishwa na vipaumbele au Ilani ya Chama ambayo inakuwa imetolewa. Wataunganisha pamoja na dira ile, tunaweza tukawa na uwezo mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ya Mipango ikisimama yenyewe itakuwa na uwezo wa kuratibu sasa vipaumbele vya Kitaifa, kuratibu vipaumbele mbalimbali na kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi hii zinaelekezwa katika maeneo ambayo tumekubaliana kama Taifa kwamba haya ni maeneo mahususi yaende hapo, ndipo tutakuwa na maendeleo. Zaidi ya hapo, itajikita katika kufanya tathmini na ufuatiliaji katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini napendekeza hayo? Hayo nayaona ni muhimu kwa sababu ukiangalia malengo ya

maendeleo endelevu yaliyotolewa na Umoja wa Mataifa ambayo yako 17 nchi ya Tanzania ni *signatory* wa hayo, na tumekubaliana tutayatekeleza hayo. Umoja wa Mataifa ulikuja na maendeleo endelevu ambayo una mambo yafuatayo: -

(i) Kutokomeza umasikini;
(ii) Kukomesha njaa;
(iii) Kuwa na afya njema na ustawi;
(iv) Kuwa na elimu bora;
(v) Kuwa na usawa wa jinsi au jinsia;
(vi) Kuwa na maji safi, salama na usafi;
(vii) Tuwe na nishati mbadala na kwa gharama nafuu;
(viii) Tuwe na kazi zenye staha na ambazo zitasaidia katika kukuza uchumi;
(ix) Kuwa na viwanda, ubunifu na miundombinu inayotosheleza;
(x) Kupunguza tofauti *(inequalities)*;
(xi) Tuwe na miji na jamii endelevu;
(xii) Tuwe na matumizi na uzalishaji bora;
(xiii) Kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi;
(xiv) Kulinda uhai katika maji;
(xv) Kulinda uhai katika vitu vinavyopatikana ardhini;
(xvi) Tuwe na amani, haki na taasisi madhubuti na;
(xvii) Kuwe na ushirikiano ili kufanikisha malengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiyaangalia haya malengo endelevu 17 na ukiangalia shabaha zake ziko zaidi ya 167, maana yake tunahitaji kuwa na Wizara peke yake ambayo inashughulikia haya maendeleo endelevu. Tunakumbuka Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema ili nchi iendelee tunahitaji vitu vinne; akataja watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ukiangalia kwenye maendeleo endelevu, wanasema kutokomeza umasikini; na sisi tunaliona hili ndiyo adui ambao hata Mwalimu Nyerere alisema ni adui, na bado mpaka leo ni adui; na kukomesha njaa. Watu wakiwa masikini, wakawa na njaa, hakuna kinachoweza kufanyika. Watu lazima wawe wameshiba ndiyo wanaweza wakafikiri na kufanya maamuzi yaliyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu bado Mheshimiwa Rais akaendelea kulitazama zaidi huko tunakokwenda ili Wizara hii ya Mipango iwe ni *thinktank* itakayoweza kusimamia vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji vipaumbele vijikite katika maeneo kadhaa. Kwa mfano, tunahitaji uwekezaji wa kutosha kwenye sekta za uzalishaji. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais katika kipindi chake ameweka rasilimali nyingi sana kwenye sekta za uzalishaji kuliko kipindi kingine chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za uzalishaji kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini ni maeneo muhimu sana na ndiyo yameajiri Watanzania wengi kuliko maeneo mengine. Zaidi ya 70% ya Watanzania wako kwenye maeneo haya, na ukiwekeza hapo, uzalishaji ukawa wa kutosha, njaa tutaitokomeza, umasikini utatoka na sasa umasikini ukitoka ndipo uchumi utakua na maendeleo yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba ni muhimu lazima tuwekeze zaidi kwenye sekta ya uwekezaji. Ushauri wangu, napendekeza 50% ya uwekezaji tuwekeze kwenye sekta za uzalishaji. Tukiwekeza pale 50%, fedha itakayopatikana tutaipeleka kwenye huduma za jamii, tutapeleka kwenye maeneo mengine na tutaweza kufanya mambo mengine, lakini usipozalisha, inakuwa ni kazi sana kuweza kuwa na maendeleo endelevu kwenye sekta za jamii kwa sababu utashindwa kumudu gharama ya namna ya kuendesha. Huku ndiko kunaweza kukatupatia fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la uzalishaji ambalo ninaliita mimi ni eneo la uzalishaji ni kwenye utalii. Uwekezaji ni mkubwa na Mheshimiwa Rais amefanya vizuri sana kwenye utalii. Sasa tunataka tuwekeze zaidi ili vitu vyote vizuri tulivyonavyo kwenye utalii viweze kuleta manufaa makubwa katika Taifa letu tutatue umasikini, tuondoe ujinga na mambo mengine yote na tuweze kuhakikisha kwamba hatuna njaa. Hilo ni eneo la kwanza ambalo nafikiri mipango yetu ikijikita kwenye eneo hilo itakuwa ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ni muhimu sana lazima tulipe nguvu ni ujenzi wa viwanda. Ujenzi wa viwanda tuliweka kwenye Ilani yetu kwamba ni kipaumbele muhimu sana. Kwa nini viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ndivyo vitaongeza thamani ya malighafi zote zinazopatikana kwenye nchi hii. Nchi hii sasa hivi tunajivunia kuzalisha malighafi, tunauza nchi za nje ikiwa malighafi, maana yake tunahamisha uchumi wote kutoka kwetu tunapeleka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na viwanda hapa vya kuongeza thamani tutakuwa tumetengeneza ajira, tutakuwa tumepunguza umasikini, tutaweza kujenga uchumi ambao ni imara na endelevu na kwa namna hiyo ndiyo nchi itaweza kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilifanya maamuzi ya namna hiyo. Hatuwezi kuacha kwamba eti unauza kahawa nje, unauza chai nje, unauza mahindi nje; haya tuongeze thamani ndipo maendeleo ya nchi yatakuwa mazuri. Ndiyo maana nasema ni kipaumbele muhimu kuwa na viwanda, viwanda, viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tatu ni kufanya biashara. Biashara ni muhimu sana. Nchi yetu iko *strategically located,* imekaa mahali pazuri panapoiwezesha kufanya biashara. Tunaweza tukawa sisi ndio *center* ya biashara hapa katika Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote bidhaa zinazotoka nchi za nje; zinazotoka China na kwingineko zinazokuja; nchi za huku Zambia, Zimbabwe, na nyinginezo zikaja kuchukulia bidhaa zao hapa kwetu. Kariakoo tukaiendeleza vizuri, mikoani huko tukaendeleza, pale Tunduma tukajenga bandari kavu, mambo yatakuwa vizuri kabisa na utakuta kwamba maendeleo yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tufanye biashara za ndani na biashara za nje na hizo ndiyo zitasaidia nchi kuwa na

walipakodi ambao ndiyo wataleta mapato mengi kwenye Taifa letu na hivyo Serikali itaweza kupata mapato makubwa. Bila biashara, hatuwezi kufika. Hicho ni kipaumbele cha tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha nne, kuendeleza rasilimaliwatu na huduma za jamii. Rasilimaliwatu ambao tunayo ndiyo mtaji wetu. Watu tuko zaidi ya milioni 63 sasa. Huu ndiyo mtaji ambao unaweza ukatumika tukawekeza kwa watu hawa. Hawa watu wakizalisha kwenye kilimo, wakazalisha kwenye madini, wakafanya biashara na nchi ikapata maendeleo makubwa na ikaweza kujitegemea ndiko ambako tunakotakiwa twende tujitegemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umeisha, basi naunga mkono hoja na ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga. Tunaendelea na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, na mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa Wabunge atakuwa Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwanza kwa hotuba yao nzuri na kwa kazi nzuri ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli huwa na-*enjoy* kumsikiliza kwa sababu huwa akizungumza natamani aendelee kuongea. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa ku-*master* sana eneo hili na hotuba yake nimeisoma yote na nitatoa tu ushauri maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza pia kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Rais katika maeneo yote ambayo yametajwa kwenye hotuba hii, lakini katika hotuba nyingine ambazo tumeshachangia, tumeeleza vizuri mafanikio makubwa ya Serikali. Naipongeza Serikali nzima kwa namna ambavyo inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *website* ya *NBS* utagundua kwamba ziko takwimu zinatuambia jambo. *Demographic dividend* ambayo imeelezwa mle ndani inasema kati ya Watanzania milioni 60, Watanzania wenye umri wa kuanzia mwaka mmoja mpaka 19 wanakadiriwa kuwa 56%; halafu 65+ ni kama 4.2%. Hapo ukijumlisha unapata 60% lakini taarifa zinasema watu wenye ulemavu wa aina tofauti wapo kama 3.1%, tayari hiyo 63%. Wenye umri kati ya miaka 19 mpaka 24 ni 9.5%, uki *sum-up* hizi *percentage* unapata *approximate* 75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba unakuja kupata *working group* hapa watu ambao wako kazini na wako *active* ni kama 30%. Sasa ukiwa na Taifa la watu takribani 70% kwa mujibu wa takwimu ambao wana sifa mbalimbali, lakini hawazalishi, maana yake unatakiwa kwenda mbali zaidi kuhakikisha kwamba mipango yako inaangalia namna bora ambavyo hili kundi kubwa la watu ambao hawazalishi linaendelea ku-*survive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambayo wazungumzaji wengine wamezungumza, nami nitazungumza kidogo maeneo hayo, ni kuweka mikakati kwenye kuongeza uwekezaji na mikakati kwenye kuongeza biashara. Nchi yetu inafanya vizuri sana kwenye eneo la uwekezaji, nami wala sina tatizo. Ukiangalia kwenye vile vigezo ambavyo vinavutia watu kuja kuwekeza, kwa mfano uwepo wa ardhi ya kutosha na upatikanaji wa malighafi, nadhani eneo hilo tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni utawala labda wa kisheria. Eneo hilo liko vizuri. Sera zinazotabirika maana yake kama mna sera ambazo ziko *unpredictable,* watu pia wana tabia ya kutopenda kwenda maeneo hayo, tuko vizuri. Miundombinu iliyoboreshwa ikiwemo barabara, umeme, mawasiliano, tuko vizuri na vivutio vya kikodi mbalimbali tumeendelea kutoa tuko vizuri, usalama tuko vizuri. Sasa yale maeneo mawili ya uwekezaji na biashara yanapata changamoto kwenye maeneo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kwenye upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu. Unapofikiria kuongeza wigo wa kodi *(tax base)*, unapofikiria kuongeza upatikanaji wa ajira, lazima ufikirie

pia namna ambavyo wawekezaji unaowahitaji wa ndani na nje ya nchi wanaweza kupata mitaji yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto sana kwenye eneo hilo, tumelizungumza kwa muda mrefu. Nadhani ni *high time* ambapo siyo lazima tufikirie ku-*source* ndani. Mimi kila ninaposoma kwenye maeneo mengine, naona upo uwezekano wa ku-*syndicate* na mashirika mbalimbali yaliyoko nje, tukaona namna ambavyo tunaweza tukakaribisha mitaji na fedha ambazo watu watawekeza kwa riba nafuu. Maeneo ya kuwekeza yapo, uwezo wa kuwekeza upo, lakini shida imekuwa ni mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kutoa ruzuku na mitaji kwenye maeneo ambayo yanaajiri Watanzania wengi. Unajua kila nikisikiliza hotuba za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanatamani mashirika yasiyopata faida yafutwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza jambo ambalo nitatofautiana nao kidogo. Shida ya *unemployment* haijaanzia Tanzania, dunia nzima huko kuna tatizo la ajira. Ziko nchi ambazo kukabiliana na hilo zimeweka *unemployment benefits,* wanalipwa watu mwisho wa mwezi ili waweze kujikimu. Ziko nchi zimetengeneza fungu la kutengeneza mitaji ili watu wasio na ajira waende nje wakatafute ajira kwa ajili ya kuleta ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tukubali kwamba yapo mashirika Tanzania ambayo Serikali inatakiwa iwekeze kwa ajili ya kupeleka watu wakaajiriwe. Jambo hili waliliona sana viongozi wa zamani. Palikuwa na mashirika hayazalishi, lakini walikuwa hawayafuti, walikuwa wanahakikisha kwamba haya mashirika yanaweza kuwa ni *service industry;* yapo yanafanya kazi na yanapewa ruzuku ya Serikali kwa ajili ya kutoa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala siyo dhambi kwa sababu ukiwa na fedha umeweka akiba, halafu una watu huku mtaani ambao wanaweza kufanya kazi na hawafanyi kazi, ni jambo ambalo watu wote watakushangaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri maeneo haya mawili, moja; upatikanaji wa mitaji ambayo ina

ruzuku nafuu, na pili, tufikirie vitu ambavyo tutavifanya ambavyo vitawafanya watu wengi waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, kuna maeneo tumefanya, kwa mfano bomba la mafuta, ni dalili ya miradi kama hiyo, miradi mikubwa kama ya *railway* na mingine. Huwezi kusema sasa tuache kuwekeza eti tutunze pesa, Hapana, haiwezekani. Tatizo la ajira litakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linanikumbusha pia kwamba Tanzania tuna *square kilometer* 947, tuna-*comparative advantage* nyingi ukilinganisha na *strategic location* yetu ambayo tunayo kwa nchi za *East Africa*. Tuna mikoa yetu ya Tanzania Bara 26. Ambacho ninatamani kuona, hawa majirani zetu wote wanaotuzunguka ambao kwa ukubwa wa nchi yetu wanazama ndani na akiba inabaki. Hivi ni vitu gani ambavyo tunaweza kuwekeza, tukawekeza kwa nguvu ili kusudi hawa watu kila wanapoamka wavipate kutoka Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo machache amesema Mheshimiwa Hasunga kwenye kilimo, *very good* amesema Mheshimiwa Hasunga kwenye utalii, *very good.* Tumezungukwa na bahari na maziwa, nami nataka niseme tu, kama tutaweka nguvu peke yake, bahari na maziwa, tuna uwezo wa kuwafanya majirani zetu wote wakatutegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tumeanzisha ufugaji wa vizimba. Tatizo bado liko kubwa tu, kila kitu kinatoka nje; *cages* zile zinatoka nje, *fingerlings* zile zinatoka nje. *Fingerlings* ni watoto wale wa Samaki, wanatoka nje na chakula cha samaki kinatoka nje. Sasa unategemea hii sekta ambayo kwa ukubwa wa Ziwa Victoria ambao tungekuwa na maelfu ya *cage,* unategemea itakua kwa kiwango kipi? Haiwezi kukua kwa sababu kimsingi hatujawekeza kuifanya ikue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kusema Mheshimiwa Waziri, tuangalie *comparative advantage* ambazo tunazo kama nchi na ni rahisi sana kwa sababu majirani zetu wengi wanatutegemea kama mlango na wanatutegemea kama

nchi ambayo ni kubwa, lakini tuna maeneo mengi ambayo yanaweza kufanya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ni mikoa yetu hii 26. Amezungumza mchangiaji mmoja kuhusu *issue* ya viwanda. Unaona sasa hivi viwanda vingi viko *centered somewhere* lakini kila mkoa una sifa ambayo haifanani na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ipo Mikoa kama Dodoma wana zabibu, hebu tu-*capitalize* na *quality* ya zabibu ambayo ni *international* na *accepted*. Twende kwenye Mkoa kama Singida kuna alizeti, tuje Geita ambako sisi tunajivunia uchimbaji wa dhahabu, tunayo *Geita Gold Refinery* ambayo sasa hivi *almost* inasaga, haipati dhahabu na haifanyi nini, mikoa yote hii tuangalie ni vitu gani ambavyo vinaweza vikawekezwa vikatengeneza ajira kwenye mikoa hiyo na kila mkoa ukawa na vitu ambavyo ni kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosumbua sasa hivi ni kwamba tuna vipaumbele kwenye karatasi, lakini kwenye mikoa huku ambako pengine tungeweza kuweka *assignment* hiyo ya kwamba kila mkoa maeneo ya viwanda tuliyoyaanzisha miaka fulani huko nyuma tuliweka maeneo ya viwanda tukasema, maeneo ya uwekezaji yamebaki kuwa mashamba, na ni kama sera inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani haja ya kuona hawa watu ambao ni 70% ya Watanzania ambao ni tegemezi kutafuta namna ambavyo nchi nzima inaweza kuingia kwenye uzalishaji, ni kutokana na mipango ambayo Wizara hii inaweza ikafanya na upatikanaji wa mitaji, tuhakikishe kwamba kila rasilimali tuliyopewa tunaitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Tutahitimisha na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, tafadhali.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye Enzi na Utukufu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili la mwisho wa ukomo wetu wa Ubunge. Ninaamini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu nitarudi na kuendelea kusimama katika Bunge hili Tukufu na ninawaombea heri Wabunge wenzangu wote wenye mapenzi mema na Taifa letu, Mungu awajaalie warudi tuweze kusimama katika Bunge hili Tukufu na tuweze kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wote waandamizi katika Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji wakiongozwa na mtu bingwa kabisa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Hakika Wizara hii anaimudu na viatu vyake vimembana sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, siachi kumpongeza Katibu Mkuu pamoja na Naibu Waziri kwa utendaji uliotukuka kuhakikisha Taifa hili linapata watu sahihi ambao ni ma-*thinktank* kuweza kuhakikisha mipango yetu imekaa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mageuzi makubwa ya mipango ya Taifa letu, hakika Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Mama ambaye ameamua kuji-*brand* kwa namna bora na ya pekee kuhakikisha Taifa letu linaweka mipango yake sawasawa kwa kuwa na Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika msemo kupanga ni kuchagua, limetamalaki vizuri kwa uongozi wake makini na mahiri. Kwanza, Mama yeye mwenyewe, Rais wetu ameamua kupanga kuwa Rais mwanamke mwenye *brand* ya aina yake. Ameamua kupanga, kuchagua na kutokuogopa kufuata kivuli cha mwingine, bali kusimama kwa *brand* yake

kama Rais mwanamke aliyekuwa na utulivu na kaliba ya aina yake katika kusikiliza wataalamu kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sifa nzuri ambayo ninaamini Rais wetu amepanga kuichagua kuwa kiigizo chema kwa wanawake wengi wa Taifa hili. Nao ni mpango mzuri ambao unapelekea wanawake wengi kwenye Taifa hili, nao kujiangalia vizuri. Unapokuwa kiongozi unavisha vazi gani? Vazi la utulivu, usikivu na kaliba njema katika kujiweka sawasawa kukitumikia kiti anachokitumikia Rais wetu, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Mheshimiwa Rais ametupa fahari wanawake wenzake kwa namna ambavyo ametuheshimisha kuwa Rais aliyepanga ku-*brand* kaliba ya mwanamke vizuri na uwezo wa mwanamke vizuri katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia mambo yasiyopungua matatu katika Wizara hii. Kwanza ni elimu. Mimi nimekuwa nikijifunza humu ndani, niliwahi kujifunza kupitia Mheshimiwa Prof. Mkenda, Waziri wa Elimu, tuliwahi kushauriana tukazungumza kwamba Taifa lolote lile ili litambuliwe kwamba limeendelea au linaloendelea, kigezo muhimu ni kiwango cha elimu cha watu wake. *One of the critical factors* ya nchi yoyote kuweza kuwa *categorized* kama ni *developed or underdeveloped* elimu ni *factor* muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeliona hilo, pia wanaamini katika kuwekeza kwenye elimu kama kigezo cha Taifa letu kuongeza kiwango chake cha kujulikana kama ni Taifa linaloendelea au lililoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ilani ya CCM katika elimu imeweka wazi malengo yake kwamba ni ili kuzalisha rasilimali watu bora kwa maendeleo ya watu. Serikali yetu kuwekeza katika elimu inaelezea matamanio yake ya kuamini katika *human capital* kama kifaa muhimu katika kuongeza uwezo wa nchi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakubaliana na jambo hilo kwamba Serikali wamefanya yote hayo kwenye elimu ili kuzalisha rasilimali watu bora na kama ni kigezo muhimu kwenye *production capacity* ya nchi yetu. Serikali imefanya mengi kwenye elimu katika maeneo mbalimbali kwenye Taifa letu, mimi sitaki kurudia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, tumeona shule zimejengwa, tumeona mikakati ya kuweka elimu ya amali na tumeona mambo mengi ambayo Serikali imeonesha dhamira yake ya kuongeza *production capacity* kwa kutumia kigezo cha kuwekeza kwenye *human capacity* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali yangu Tukufu iamue kupanga, licha ya kwamba wamegawanya madarasa na vyote vile wanavyotamani kwenye elimu sawasawa maeneo yote nchini, lakini kwa kuangalia vigezo vya Kimataifa, tunaambiwa kwamba yeyote asiachwe nyuma katika maendeleo endelevu. *No one should be left behind in sustainable development. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu Tukufu iamue kupanga, kuweka mkazo maalum katika maeneo ambayo kiwango chake cha elimu hakiridhishi bila kuathiri maeneo ambayo kiwango chake cha elimu kinaridhisha. Hili ni muhimu sana, la sivyo, *return* ya *investment* ambayo Taifa letu imeweka kwenye elimu inaweza isizae matunda sawasawa, na bado baadhi ya jamii zikaendelea kubaki nyuma na wengine wakaendelea kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *distribution* iwe ya madarasa kote, na elimu kote, ni wazo zuri kuhakikisha pia kunakuwa na mpango maalum kusaidia maeneo ambayo yako nyuma kielimu bila kuathiri maeneo ambayo yako mbele kielimu ili maana halisi ya kurudisha thamani ya tulichowekeza kwenye elimu iweze kuleta maana kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba kuchangia kuhusiana na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.

Taifa letu au Serikali yetu imewekeza kwenye Kiwanja cha Ndege cha Msalato.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. *ENG.* MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ipange kuona namna ambayo Kiwanja cha Ndege cha Msalato hakitakuwa '*Vingungutilised'* kwa sababu tumeona viwanja vinatangazwa kule maeneo ya *Airport* Msalato, ni namna gani Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji imeingiza miguu yake kwa kushirikiana na sekta hiyo ya anga pamoja na sekta ya uchukuzi kuhakikisha kunakuwa na *good land use plan* katika eneo lote la Msalato ili kuhakikisha tunaleta haiba nzuri ya kiwanja kile cha ndege cha Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ambayo tunaiona Dar es Salaam...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako ulishaisha.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe! Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza kwa nafasi ya Makamu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema, na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Katika kipindi chake akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi tisa, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, imesimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ikiwemo miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mwendelezo mzuri wa utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa umeme Mto Rufiji; mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Umeme, reli na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wa Tanzania na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, wakati dunia inapambana na athari za vita vya Urusi na Ukraine na pia janga la *Corona Virus (Covid-19),* tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kutokana na nchi nyingi tunazoshirikiana kibiashara na kiuchumi kukumbwa na mtikisiko wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Msajili wa Hazina, anapaswa kuendelea kuimarisha mitaji kwa mashirika ambayo yatachochea ukuaji wa uchumi ikiwemo Benki za *TADB, TCB, TIB* na *ATCL* ili iweze kusimama kibiashara ikiwa ni nguzo muhimu hata kwa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hatua ya Serikali kwa kurudisha Tume ya Mipango na hata maboresho ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Tume ya Mipango ni nguzo muhimu katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu hasa katika kipindi hiki tunapotekeleza miradi mingi ya kimkakati. Upangaji na utekelezaji wa miradi unahitaji kuwa na chombo madhubuti kinachoweza kusimamia miradi Kitaifa badala ya kusimamiwa kisekta. Msajili wa Hazina anapaswa kupewa nguvu zaidi ili asimamie mashirika ya umma ili yaendeshwe kibiashara na kwa tija ya kiushindani kwa hapa nchini na hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa tija kwenye mashirika ya kibiashara itapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa mapato ya kikodi na hata mikopo kwa Serikali. Napendekeza kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea hata kwa kutafuta vyanzo

mbadala vya fedha kugharamia ujenzi huo, kwa vile kutakuwa na fursa kubwa za usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa *SGR,* napendekeza kuendelea na kuboresha reli ya *TAZARA* na uboreshaji wa bandari zetu ikiwemo ujenzi wa bandari kavu ikiwemo ya Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki ili kupunguza gharama za kusafirisha pembejeo na mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija. Kuna umuhimu mkubwa kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ulenge kupunguza gharama za usafirishaji mizigo kwa wateja wa bandari kutoka Zambia, *DRC,* Malawi na hata kwa kupunguza gharama za usafirishaji wa pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa muda unahitajika haraka wakati Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na jitihada za kurekebisha mikataba ikiwemo wa uendeshaji wa *TAZARA*. Pia katika kipindi hiki cha mpito, napendekeza Serikali iwapatie *TAZARA* vichwa *(engine)* vya treni vya ziada vinavyomilikiwa na Shirika la Reli *(TRL)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha mapato ya fedha za kigeni yanaongezeka kupitia mazao ya kilimo, madini na utalii. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatasaidia kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa na pia kuendeleza utulivu wa shilingi yetu dhidi ya sarafu kuu za kigeni na hata kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ihakikishe kipaumbele cha kuwekeza kwenye kilimo ikiwemo pembejeo na umwagiliaji

kwa lengo la kuongeza tija na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kulinda mfumuko wa bei.

MHeshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali inashauriwa kuchukua hatua zaidi za kuimarisha sekta za kilimo, utalii na madini ili kukabiliana na athari za kiuchumi wa kidunia. Kutokana na athari za kiuchumi ulioikumba dunia nzima ikiwemo changamoto za upatikanaji wa fedha za kigeni, hatua za kuimarisha sekta hizo hapo juu, inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, viwanda vya mbolea kutokana uwepo wa malighafi za madini ya *calcium carbonate, lime* na *phosphate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye Mradi wa Madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha Ferroniobium *(FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa Kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani, ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi nyingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo inapatikana milima ya Pandahill Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya Ferroniobium *(FeNb end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahitaji kujiwekea mikakati ya haraka *(Quick Wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kuboresha urari wa biashara, kukabiliana na athari za *Covid-19* na sasa vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa Niobium na Kiwanda cha Ferroniobium, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwekezaji mkubwa kwenye miradi, napendekeza Serikali kuharakisha uwepo wa Sera na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini *(Monitoring and Evaluation)*. Kuna umuhimu wa kuboresha miongozo na pia kuangalia upya muundo wa Kitaifa wa ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda kwa dakika 10 tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu na kwa muktadha wa hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametujalia hii leo kujadili hotuba hii mihimu kwa ajili ya maendeleo ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye aliona maono haya makubwa ya kuanzisha Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawashukuru sana viongozi wetu wakubwa wa Taifa katika nchi hii kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Waziri Mkuu pamoja na viongozi wengine wote

ambao wanatuongoza katika kuendeleza sekta za maendeleo katika nchi hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Prof. Kitila, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, kwa kuwasilisha bajeti hii muhimu katika Bunge hili Tukufu. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wote chini ya ofisi hii pamoja na Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na viongozi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naushukuru sana uongozi wa Bunge hili chini ya Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wengine wa Bunge letu na Wabunge wenzangu ambao wamechangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa kuendelea kunipa nafasi na kunipa uwezo wa kuwawakilisha hapa Bungeni na kunipa ushirikiano ambao kwa kweli ninaamini bila wao nisingeweza kufanya kazi nzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, ameeleza mengi, nami niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hasa kwenye eneo au sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, Wabunge wengi wamechangia umuhimu wa kuendelea kuweka mazingira bora na wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji hapa nchini. Ni ukweli usiopingika kwamba kulingana na maono haya muhimu ya Mheshimiwa Rais wetu, sasa kwenye eneo hili, mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji yameboreka zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, kwa takwimu tulizonazo katika sekta ya uwekezaji, kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 Tanzania imeweza kuvutia wawekezaji kwenye miradi zaidi ya 2,175 na katika miradi hii sekta zinazoongoza katika miradi ya

uwekezaji kwanza ni sekta ya viwanda ambayo imevutia miradi 917, sawa na asilimia 50.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta inayofuata ni sekta ya usafirishaji ambayo imevutia zaidi ya uwekezaji wa miradi 348, ambayo ni 19%. Sekta inayofuata ni sekta ya majengo na biashara ambayo imevutia uwekezaji wa zaidi ya miradi 204, ambayo ni sawa na 11%, inayofuata ni utalii 10.5%, inayofuata ni kilimo asilimia tisa na mingine inafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Nataka kusema jinsi ambavyo Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imewezesha hasa kwenye sekta ya viwanda na biashara kuweza kuvutia uwekezaji mkubwa na kuongeza viwanda vingi, lakini zaidi kama ilivyosemwa na Wabunge kuwezesha ajira na kipato zaidi kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya viwanda, moja ya maeneo ambayo yamesemwa ni namna gani ya kuhakikisha tunalinda wawekezaji au viwanda vya ndani. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha tunawalinda wawekezaji hasa kwenye sekta ya viwanda na wafanyabiashara. Hii kazi kubwa inafanywa ili kuhakikisha ukuaji na kama wengine walivyosema tuzalishe matajiri ambao ndio watakaoweza kuendeleza maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo ambayo yametajwa na Waheshimiwa Wabunge ni namna gani kutakuwa na maeneo mahsusi ya uzalishaji kwenye viwanda, kwa maana ya *comparative advantage* au Mheshimiwa Mbunge alisema "*niche*". Tayari Serikali imeshakuwa na mipango hiyo. Kwanza, tulianza kwenye maeneo mahususi. Kuna kitu kinaitwa *One District One Product (ODOP)* kwamba tunasema katika wilaya au mikoa mahsusi izalishe zao fulani au bidhaa fulani ambayo yenyewe ina faida zaidi *(comparative advantage)* katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hilo ndilo tunaloenda nalo pia kama nchi kuhakikisha tunafikia maono ya Mheshimiwa Rais ya kutaka Tanzania iwe ni ghala la kuzalisha chakula na bidhaa

zinazotokana na mazao ya kilimo. Kwa hiyo, Wizara ya Viwanda na Biashara tunaendelea kufanya kazi hii kutekeleza maono haya ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi katika kuhakikisha mazingira ya ufanyaji biashara yanaendelea kuboreka, tunahakikisha ile miradi ya kimkakati kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwamba tuilinde na tuiwezeshe, lakini zaidi ni namna gani ambavyo tunaendelea kuhakikisha tunasaidia wajasiriamali ili nao waweze kufaidika na fursa zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamesema kuhusiana na Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki ambacho kinajengwa pale Ubungo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba 90% ya nafasi zinazotolewa pale, zimetolewa kwa Watanzania wazawa, tuitumie nafasi hii. Asilimia chache ambazo hazizidi tano ndiyo labda wageni ambao watakuja kuwekeza pale. Kwa hiyo, fursa hiyo ipo, na hili ni lengo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba tuhakikishe *local content* katika maeneo yote kwa maana ya Watanzania wazawa waweze kufaidika na fursa zilizopo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya taasisi za umma kujiendesha kibiashara. Tayari sisi kama Serikali tumeanza kuliona hilo, na kwa uratibu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, baadhi ya taasisi kwa mfano katika Wizara ya Viwanda na Biashara kama *SIDO* ambayo ni shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo, tunasema sasa waanze kujiendesha kibiashara, pamoja na kutoa huduma, lakini bado tunadhani wanaweza kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari tunachukua hoja hizi na nyingine za Waheshimiwa Wabunge ambao wameishauri Serikali kuhakikisha tunaboresha kwanza sekta ya uwekezaji, lakini zaidi ufanyaji biashara na sekta ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tunamkaribisha mtoa hoja kwa dakika zisizozidi 30 ahitimishe hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa jinsi ambavyo umeendesha mjadala huu. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kunipa *company* ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru tena Kamati yako ambayo tumefanya nayo kazi vizuri sana; nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote hususan Wabunge 17 ambao wamepata nafasi ya kuchangia na Wabunge watatu ambao walipata nafasi ya kutoa taarifa hapa mbele. Muhimu ni kwamba wote wamekiri umuhimu wa Wizara hii, na ninashukuru sana kwamba wote wame-*appreciate* kazi ambayo tunaifanya na wametupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki Mbunge ukipongezwa ni jambo zuri sana kwa sababu ni kipindi muhimu. Kwa hiyo, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zenu hizo na tunazichukua kama sehemu muhimu sana ya kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu neno moja la utangulizi kwamba maoni mengi sana ya Waheshimiwa Wabunge yamejikita kwenye mipango, na kwa kweli wamejadili mipango vizuri sana na Mheshimiwa Japhet Hasunga ameonesha kwamba hotuba yangu imejaa zaidi uwekezaji kuliko mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, leo nilikuwa nawasilisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambayo ina mafungu matatu. Hapa Bungeni, kwa Bunge hili kabla halijaisha mtaniona mara tatu nikiwa nimesimama hapa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama nikiwasilisha bajeti ya ofisi yangu hii, lakini tarehe 05 mpaka 10 Juni, nitarudi hapa kuwasilisha Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo na Waheshimiwa Wabunge watakuwa na siku zisizopungua nne, tunajadiliana tu kuhusu Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 nitarudi hapa tena kuwasilisha Hali ya Uchumi wa Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026, tutakuwa na siku zisizopungua tano tukijadiliana mambo yote haya ambayo nilikuwa nasema hapa. Kwa hiyo, ndiyo maana umeona kwamba, nime-*base* zaidi kwenye uwekezaji kwa sababu, ninazo siku takribani kumi za kuhangaika na mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mipango kwa umuhimu wake Bunge letu lina utaratibu wa kuipangia siku yake maalum na kwa mwaka tunakutana nayo mara tatu; tunakutana nayo kwanza Novemba, Machi na Juni, pale Msekwa. Kwa hiyo, mipango imepewa nafasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba niseme kwamba, kimsingi mengi ambayo tumepokea hapa ni maoni na ushauri. Sisi tunapokea na tutazingatia katika utekelezaji wa bajeti hii mkitupitishia leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu ufafanuzi wa mambo machache sana. Kwanza, kwa upande wa Kamati yetu, wametupa ushauri kwenye maeneo 17, maeneo ya jumla saba na maeneo mahususi 10. Niseme kwamba, yote haya tutayazingatia. Kweli sina sababu ya kupitia moja moja, yote tutazingatia, labda moja tu hili la kwa nini tulikuwa na bajeti ya shilingi bilioni nane kwenye mradi wa 2,229 na tumepatiwa shilingi milioni 300 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, baada ya kuanza kutekeleza shughuli hii, tulikuja kupata fedha kutoka kwa wadau. Kwa hiyo, fedha nyingi ambazo zimetoka kutekeleza hii kazi ilifanywa kwa kiasi kikubwa na wadau wetu wa maendeleo, ndiyo maana Serikali imeweza ku-*save* fedha nyingi zaidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge, yapo maeneo matatu mahususi ambayo ningetaka kuyatolea ufafanuzi. Kwanza, ni hili ambalo linahusu miradi ya uwekezaji, mingi kusemekana kwamba ni ya watu wa nje. Hii ilitolewa na Wabunge kadhaa, akiwepo Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kitakwimu utaona kwamba, katika miaka miwili iliyopita tumesajili miradi 2,175, miradi 743 ni ambayo inamilikiwa na Watanzania. Hii ni sawa na asilimia 34.2. Miradi 493 inamilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na wageni, sawasawa na 22.7%. Kwa hiyo, utaona takribani 57% ya miradi yote nchini ama inamilikiwa na Watanzania wenyewe moja kwa moja ama inamilikiwa kwa ubia kati ya Watanzania na wageni. Kwa hiyo, miradi ya wageni ni takribani 43%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatoa kipaumbele sana kwa wawekezaji wa ndani. Pia, niseme, siyo kila mwekezaji anapitia *TIC*. Kwa hiyo, ipo miradi mingi ya uwekezaji ambayo inaendelea katika nchi yetu ambayo haijapitia *TIC,* na hivi tumefanya hamasa kubwa, ndiyo maana tunajiona kwamba, Watanzania wengi wameanza kupitia *TIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia hapa, ni nafasi ya tume katika maeneo mawili. Kwanza, suala la *Monitoring and Evaluation;* na Mheshimiwa Kwagwilwa ameliongelea kwa msisitizo wa hali ya juu. Pia, amezungumzia suala la uhusiano uliopo kati ya Wizara hii, Tume ya Mipango pamoja na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, ukisoma majukumu ya tume kwa kweli, suala la tathmini na ufuatiliaji wa miradi, Tume ya Mipango imepewa hili jukumu. Ukienda kusoma kwenye Sheria yetu ya Mipango, Kifungu cha 6(2), (t), (e) na (f) yote yanahusu suala la ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kisheria tayari Tume ya Mipango inalo jukumu hilo, ina mamlaka yote kisheria. Tume ya

Mipango inaruhusiwa kuitisha mpango wowote, sera yoyote, mkakati wowote, kuupitia na hata kuusimamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kweli Bunge lilitunga Sheria nzito sana ambayo Tume ya Mipango hakuna mwanya wa kisheria ambao upo ndani ya Sheria ya Tume ya Mipango. Kwa hiyo, hili nadhani halina shida, tunaendelea kuibadilisha Tume ya Mipango kwa maana ya Watumishi na kimuundo, lakini kwa maana ya kisheria tayari, kwa maoni yangu na kwa maoni ya Serikali iko *covered* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, ni suala la muundo. Kimuundo, Tume ya Mipango Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wajumbe ni akina nani? Pamoja na wajumbe wengine, mle ndani anaingia Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Waziri mwenye dhamana ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari tukitoka pale tunatoka tukiwa kwenye lugha inayofanana. Pia, Makatibu Wakuu wanaohusika na fedha na wanaohusika na mipango ni waalikwa wa kudumu wa Tume ya Taifa ya Mipango. Kwa hiyo, inamaanisha pia, hata watendaji tayari wapo kwenye tume pale ambapo tumejadili na kupitisha mambo, wanakuwa ni sehemu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nilitaka kulitolea ufafanuzi kidogo sana; kwanza, nikubaliane na Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya, maoni yake na maoni ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa ni ya msingi na ni muhimu tukaendelea kuyazingatia. Napenda tu hii dhana yake ya *niche* kwamba, sisi ni bora katika nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, ni muhimu sana tujipambanue. Utaona kwenye mapendekezo ya dira kuna maeneo kadhaa ambayo tunasema tunataka tuwe *top* katika Afrika, tuwe wangapi duniani, na kadhalika. Kwa hiyo, hili tunalichukua kwamba, ni eneo muhimu na tunapokea changamoto yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo hii isichukuliwe kwamba, kwa sasa Tanzania haina maeneo ambayo tunajipambanua nayo katika Ukanda wa Afrika ama duniani. Niwape mifano, nchi yetu inajulikana duniani kwa uzuri wa asili na wanyama, inajulikana kwa suala la amani na utulivu, inajulikana kwa Kiswahili chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajulikana kwa ushawishi katika ukanda huu wa Afrika. Tazama mbuga yetu ya Wanyama ya Serengeti imeshinda tuzo, *Leading National Park* kwa Afrika kwa miaka sita mfululizo tangu 2019 mpaka 2024, Mbuga ya Wanyama ya Serengeti ndiyo mbuga bora kabisa Afrika, miaka sita mfululizo. Mbuga hiyo pia imeshinda kuwa Kivutio Bora cha Watalii Afrika kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari yako maeneo ambayo tunajipambanua, lakini hii haidhoofishi hoja yake kwamba, tuendelee kuangalia maeneo ambayo, kama nchi, tunakuwa tunajiweka vizuri mara zote. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo ningetaka kulitolea ufafanuzi, kwa maana ya maeneo mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize na maeneo ya jumla mawili, makubwa, yanajitokeza kisera na wakati mwingine kiitikadi. Kwanza, nini nafasi ya Serikali katika maendeleo ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengi sana katika eneo hili na kuna mjadala mpana duniani, hasa katika ulimwengu ambao umefilisika kiaidiolojia. Hutasema kuna mabepari hapa, ama wajamaa; wakomunisti wanasema kabisa kwamba, dunia kiitikadi inaelekea kufilisika. Kwa hiyo, katika maeneo hayo, nafasi ya Serikali ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi zipo kazi za msingi ambazo hazibishaniwi duniani kwamba, hizi ni kazi za dola, usalama wa nchi ni kazi ya dola. Suala la usimamizi wa sheria *(Law and Order)* ni kazi ya msingi ya dola. Suala la utawala na huduma, elimu, afya maji, utumishi wa umma, haya ni mambo ya msingi ambayo lazima yafanywe na dola. Ndiyo maana hatubishani hapa, tutaweka fedha kwenye afya, tutaweka fedha kwenye elimu.

Hata nchi zilizobobea kwenye ubepari, bado maeneo haya Serikali itabeba jukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaifahamu nchi moja tu duniani hapa na ipo Afrika, sitaitaja, ambayo yenyewe imeamua ku-*privatize* mpaka elimu. Elimu yote imekabidhiwa sekta binafsi. Lakini kwa kweli, dunia inakubaliana kwamba, maeneo haya ni maeneo ambayo kimsingi, duniani, inabidi dola ichukue nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa miundombinu, hili duniani kote, Serikali inajenga barabara. Kwa hiyo, dola ina nafasi kubwa sana katika eneo hilo. Vilevile, *management* ya uchumi kwa ujumla wake, mambo haya ya mfumuko wa bei, mambo ya sarafu, na kadhalika, bado yanakuwa ni sehemu muhimu sana ya Serikali. Mambo ya hifadhi ya jamii, mambo ya mahusiano na diplomasia ni maeneo ambayo hayabishaniwi duniani kwamba, ni kazi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali linakuja, nini nafasi ya Serikali kwenye ujenzi wa uchumi? Hapo ndipo ambapo kazi kubwa na mjadala mkubwa unaendelea duniani na wataalam, wanauchumi, na kuna vitabu vingi vimeandikwa vikizungumzia suala hili. Hapa tunazungumzia nafasi ya dola, na nafasi ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko tunapotoka nje, zipo nchi ambazo zinadhani kwamba, Serikali ama dola ikae nje ya suala la ujenzi wa uchumi, siyo kazi yake ya msingi, yenyewe ishughulikie hayo mambo ambayo nimeyataja, lakini iachane na habari za ujenzi wa uchumi, kazi hiyo ifanywe na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mwelekeo unaosema kwamba, hapana, Serikali lazima imiliki na kuendesha uchumi kwa niaba ya umma, ndipo tulipotoka. Tulipotangaza Azimio la Arusha, tukasema kwamba, uchumi unamilikiwa na dola kwa niaba ya umma. Huko tumeshaondoka kuanzia miaka ya 1980, miaka ya 1990. Sasa tupo kwenye eneo ambalo tunasema, Serikali ina nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kazi ambazo nimezitaja na nafasi ya *management* ya uchumi, lakini bado nafasi ya Serikali katika maeneo ya kimkakati kiuchumi, lazima nafasi yake iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana ukisoma Taarifa zote za Benki ya Dunia, Taarifa za *IMF*, moja ya eneo ambalo tunakosolewa sisi kama nchi, ni kwamba, ndiyo uchumi wetu umekua sana, lakini ukuaji wa uchumi wetu umeendeshwa, wanasema ni *public investment driven* kwamba, unatokana na uwekezaji wa sekta ya umma. Ni kweli, miundombinu ya reli, Bwawa la Mwalimu Nyerere, barabara zote kubwa zimejengwa na dola, ndiyo maana uchumi wetu upo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tunachosema hapa ni suala la kufanya biashara, imeshajulikana kitafiti kwamba, Serikali zote duniani hazipo vizuri kwenye kufanya biashara. Kwa hiyo, kufanya biashara iachiwe sekta binafsi, kazi ya Serikali iwe ni kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara. Mazingira mazuri maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, lakini mawili ya msingi ni kwamba, Serikali isibandike tozo na ada zinazokwaza biashara. Serikali iweke sera nzuri za kikodi ambapo inapata mapato yake, pia, inahakikisha kwamba, sera za kikodi zinasaidia kukuza biashara na kukuza sekta binafsi na hapo ndipo Serikali ambapo imejikita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye kazi ya kujenga miundombinu ya msingi, kwamba, mwekezaji akija hapa asifikirie habari ya maji, habari ya umeme, habari ya barabara, Serikali iwekeze katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hapo ndipo tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo eneo la tatu ambalo ni muhimu. Serikali lazima iweke sera za msingi za kuchochea, kuongeza thamani ya rasilimali ambazo zinapatikana ndani ya nchi, kuzuia na kupunguza kusafirisha nje ya nchi bidhaa ambazo haziongezi thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo ambalo ni muhimu sana likaangaliwa kwa sababu, udhaifu wa ukoloni ulikuwa ni katika

maeneo mawili; ukoloni tuliulaani kwa sababu ulikuja hapa ukachukua maliasili zetu ukaenda ukajenga viwanda kwao, ukaja hapa ukachukua watu wetu, ukachukua nguvu kazi, ukaenda kujenga viwanda Ulaya. Hayo ndiyo maeneo mawili mabaya sana ambayo ukoloni ulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuendelea kusafirisha rasilimali za nchi bila kuongeza thamani ni kufanya matendo ya ukoloni. Kwa hiyo, ni eneo ambalo lazima, kama Serikali, tumeamua kuweka sera ambazo zitahakikisha kwamba, tunaongeza thamani bidhaa hapa ndani ya nchi kabla hazijasafirishwa. Tumesema na Rais wetu ameweka msimamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Waziri wa Madini anafahamu, Mheshimiwa Rais ameweka msimamo kwamba, kwenye madini ya kimkakati mambo mawili; moja, hayatasafirishwa nje ya nchi bila kuongezewa thamani ndani ya Tanzania. Ndiyo maana kule Kabanga tunajenga kiwanda cha kuchakata Nickel, hivyo hivyo Rukwa, hivyo hivyo Lindi, *Graphite* wanakuja kuweka viwanda hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunataka tuongeze kwamba, madini haya muhimu yachimbwe na Watanzania ama Watanzania kwa ubia na wageni, isitokee wageni tupu wakamiliki madini haya kwa sababu, ni madini muhimu sana. Lengo ni kwamba, badala ya kusafirisha *Lithium, Nickel,* wasafirishe kutoka Tanzania betri ambazo zinatokana na madini haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni jukumu la Serikali kuweka sera za namna hii ili kuhakikisha kwamba, uchumi unakwenda vizuri. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inajitambua na inaelewa nafasi yake ni nini na nafasi ya sekta binafsi ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, tumeaswa vizuri hapa kwamba, tuwe makini na wageni kuingia hapa kuja kumiliki uchumi wetu. Hili ni eneo ambalo limezungumzwa sana na tunalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme jambo moja, mtu mmoja amesema hapa, tujifunze kutoka nchi nyingine na nchi moja ya kujifunza ni China, ambayo imepiga hatua kubwa sana katika miaka ya 40 kuondoa watu wake kwenye umaskini kupitia viwanda. Waligundua nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Xi Jinping, Rais wa China, ameandika Kitabu kinaitwa Kupambana na Kuondokana na Umaskini. Mle ndani ameandika mambo mengi, lakini anasema tujifunze mambo makubwa mawili, la kwanza, anasema tusiogope wala kuona aibu kutumia mitaji na teknolojia kutoka nje ya nchi katika kuendeleza rasilimali zetu. Na hiyo ndio ilikuwa falsafa ya Xi Jinping ya kufungua China, *opening up China*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma walijifungia, nchi kubwa, ina watu wengi, wakajifungia, wana rasilimali nyingi, lakini wako ndani ya umaskini. Xi Jinping miaka ya 1970 akasema, hapana, akaamua kuifungua China, akakaribisha wawekezaji kutoka dunia nzima wakajenga viwanda ndani ya China, ndiyo imewatoa kwenye umaskini wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Xi Jinping anatuambia tusiogope wala kuona aibu kutumia mitaji na teknolojia kutoka nje ya nchi katika kuendeleza rasilimali za nchi. Kwa hiyo, muhimu hapa ni tukaribishe wawekezaji, lakini tuwe na sera nzuri, waje hapa tujenge viwanda. Hii ndiyo hoja ya msingi na ndiyo mwelekeo ambao sisi kama Serikali, tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Xi Jinping anasema, hakuna jamii yoyote inayoweza kuendelea yenyewe kwa kutegemea nguvu zetu pekee, lazima tufungue milango ya kiuchumi kutoka kwa wageni. Hili ndilo eneo ambalo lazima tuwenalo na ni siri kubwa sana ya ushindi wa China dhidi ya ubeberu duniani. Muhimu wakawekeze kwa sababu, akishaweka kiwanda hapa, atakipeleka wapi? Kitakuwepo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokaribisha wawekezaji hapa, haimaanishi kuwakandamiza Watanzania. Serikali yetu inatambua nafasi ya Watanzania. Nchi hii ni ya Watanzania, lazima wawe juu ya nchi yao na lazima wafaidike na

matunda yote ya uwekezaji kwa sababu, hii ni nchi yao. Hilo jambo tutaendelea kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tena kwa kuwashukuru. Nakushukuru wewe mwenyewe, pamoja na Mheshimiwa Spika kwa jinsi ambavyo mmesimamia uendeshaji wa hii bajeti yetu. Muhimu ni kwamba, tuendelee kuwa sauti moja. Sisi ni timu moja, lazima tucheze kama timu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tushukuru Bunge lako kwa sababu linafanya kazi na Serikali. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge pia kwamba wananchi wapo na sisi, kwa sababu katika utafiti ambao tuliufanya katika Dira ya Taifa ya Maendeleo, tuliuliza maswali mengi lakini mambo yafuatayo yalijitokeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, 76% ya Watanzania waliohojiwa walisema kwamba katika miaka 25 iliyopita nchi imekwenda vizuri, 70% walisema kwamba wana matumaini makubwa na miaka 25 ijayo.

Mheshimwia Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Serikali, Bunge na wananchi walio wengi na Watanzania wapo na sisi kisera, wapo na sisi katika haya ambayo tunayafanya. Nakushukuru sana, na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri ahsante sana, tunakushukuru.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.....Sh. 8,679,218,780
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Division*.......Sh. 1,250,402,624
Kifungu 1003 – *Planning, Research & Development Division*..............................................Sh. 4,361,390,760
Kifungu 1004 – *Legal Services Division*.....................Sh. 1,550,861,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 400,380,000
Kifungu 1006 – *Inform. & Comm. Tech. Division*......Sh. 3,545,975,520
Kifungu 1007 – *Public Relations and Comm. Unit*......Sh. 519,116,000
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 714,324,020
Kifungu 1009 – *Risk Management Unit*.......................Sh. 811,818,000
Kifungu 1010 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,390,060,000
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*...........Sh. 0
Kifungu 2002 – *Funds Management & Investment Division*..............................................Sh. 1,310,362,016
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*…………………….....Sh. 0
Kifungu 4001 – *Management Service Division*.........Sh. 7,725,049,000
Kifungu 4002 – *Performance Management Comm. Entities Division*................................Sh. 24,578,214,040
Kifungu 4003 – *Performance Management Non-Comm. Ent. Division*.....................................Sh. 3,747,959,040

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*....................................Sh. 4,531,188,832
Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit*..................Sh. 551,383,200
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Department*.......................................Sh. 1,775,470,600
Kifungu 1004 – *Legal Unit*………………………………...Sh. 520,904,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*.....Sh. 773,784,000

Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…………..………......Sh. 589,252,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*….....Sh. 609,376,000
Kifungu 1008 – *Information & Comm. Tech. Unit*…....Sh. 695,232,000
kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 895,100,000
Kifungu 2001 – *Public Sector Investment Division*....Sh. 1,851,302,000
Kifungu 2002 – *Private Sector Investment Division*...Sh. 7,880,477,569
Kifungu 2004 – *Business Environment Unit*.................Sh. 1,318,714,799

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..............................Sh. 6,051,984,600
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............Sh. 1,242,500,000
Kifungu 1003 – *Planning & Budgeting Division*.........Sh. 2,361,068,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*.....Sh. 953,800,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 866,480,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*.........Sh. 939,720,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*...............................Sh. 835,920,000
Kifungu 1008 – *Information & Communication Technology Unit*..................................Sh. 966,600,000
Kifungu 1009 – *Risk Management and Quality Assurance Unit*.....................................Sh. 754,000,000
Kifungu 1010 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh. 819,740,000
Kifungu 2001 – *National Planning Division*................Sh. 7,257,656,000
Kifungu 2002 – *Trade and Private Sector Eng. Division*..............................................Sh. 3,811,022,000
Kifungu 2003 – *National Key Results Areas Division*.............................................Sh. 3,967,880,000
Kifungu 2004 – *Perform. Monitoring & Evaluation Division*.............................................Sh. 5,715,968,400
Kifungu 2005 – *Innovation, Research and Development Division*..............................................Sh. 2,601,030,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Division*............Sh. 80,000,000
Kifungu 1003 – *Planning, Research & Development Division*……………………………………Sh. 218,600,000
Kifungu 1006 – *Information & Communication Technology Division*.............................Sh. 300,000,000
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*…...............................Sh. 90,000,000
Kifungu 1009 – *Risk Management Unit*..........................Sh. 96,860,000
Kifungu 2001 – *Public Investment Management Division*............Sh. 0
Kifungu 2002 – *Funds Management & Investment Division*...................................................Sh. 98,590,000
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring*................................Sh. 0
Kifungu 4001 – *Management Service Division*............Sh. 204,291,000
Kifungu 4002 – *Performance Management Commercial Entities Division*.....................................Sh. 251,230,000
Kifungu 4003 – *Performance Management Non-Commercial Entities Division*…..................................Sh. 331,120,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*...................................Sh. 1,746,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Department*.......Sh. 300,002,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 849,998,000
Kifungu 2001 – *Public Sector Investment Division*....Sh. 350,000,000
Kifungu 2002 – *Private Sector Investment Division*………………………………...Sh. 4,436,746,000
Kifungu 2004 – *Business Environment Unit*................Sh. 7,792,562,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango**

Kifungu 1003 – *Planning & Budgeting Division*.........Sh. 9,361,277,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi, mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi kujadili Makadirio na Mapato ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2025/2026. Sasa naomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana, na sasa nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki. Baada ya kuwahoji na ninyi kusema ndiyo wote kwa ujumla wenu, sasa nitumie nafasi hii kutangaza rasmi kwamba Bunge limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pia na Naibu aliyekaa karibu nawe hapo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, tunawatakia utekelezaji mwema wa yale ambayo mmewaahidi Watanzania kupitia Bunge hili.

Pia nitumie fursa hii kuwapongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Ofisi hii. Tunaamini kwamba wataendelea kuisuka ofisi hii ili mambo yaendelee kuwa mazuri zaidi, hasa kipindi hiki ambacho tunatarajia mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wanachangia yaingie kwenye dira yetu ya miaka 25 ijayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ambayo inaisimamia ofisi hii, Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii tunawashukuru sana kwa kazi nzuri; na Waheshimiwa Wabunge wote mmetoa mmetoa michango yenu mingi kabisa hapa ndani na kama walivyokuwa wakihitimisha hapa michango yenu wameipokea na bila shaka wataendelea kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pengine kwa upekee kabisa Mheshimiwa Waziri uko hapa na nimefurahi pia Waziri wetu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia yuko hapa. Mchango alioutoa Mheshimiwa Vuai Nahodha ni muhimu sana utiliwe mkazo na ufuatiliwe. Kwa nini? Kwa sababu kama nchi tunawaza hiyo dira ya miaka 25, sawa, lazima tuwe tunawaza mbali zaidi, na ni vizuri kwa sababu tukishakuwa na ile dira ya miaka 25 tutakuwa sasa

na ile mipango ya miaka mitano mitano, tayari tunaweza kuanza kufanyia kazi mawazo aliyoyatoa.

Nafikiri nchi yetu itapiga hatua kwenye eneo hilo la elimu, hasa katika kutoa elimu ambayo ni bora kabisa, lakini pia siyo elimu bora tu, lakini elimu inayoweza kutusaidia na kututoa hapa tulipo kama Taifa.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika kuyafanyia kazi mawazo waliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge. Nimeona nitaje mchango huo maalumu kabisa, kwa sababu wenyewe umehusu eneo hili la mipango yetu kama Taifa kwenye eneo la elimu. Kwa sababu bajeti ya elimu bado, basi Waziri najua bajeti itakuwa imeshakamilika, lakini bila shaka kunaweza kukawa na maneno mawili matatu kutuonyesha Watanzania tunaweza kuelekeaje kwenye hilo eneo.

Waheshimiwa Wabunge, basi baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.36 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 25 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*